

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 15 AprilI, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report and Accounts of Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the year ended 30th June, 2007*)

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 68

**Fedha za Misaada**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa, fedha nyingi zinazotolewa na *TACAIDS, Global Fund* na Mashirika mengine kupitia Hal mashauri za Wilaya bado haziwafikii walengwa kama waathirika wa UKIMWI, Watoto Yatima hasa wanaoishi vijijini kama ilivyothibitika katika ripoti ya CAG kwa baadhi ya Wilaya hapa nchini; na kwa kuwa fedha hizo bado zinatumika kwa semina, makongamano hasa maeneo ya Wilayani:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hizo fedha zinawafikia walengwa?

- (b) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kutumia *Special Audit Report* ya CAG iwe kama mwongozo wa kusahihisha makosa ambayo bado yanaendelea kwenye Halmashauri nyingi za Wilaya hapa nchini?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati ambapo ni lazima watoe mwongozo thabiti kama ule wa *Basket Fund* ili fedha zisiendelee kutumiwa na Wilaya zaidi kwa kulipana posho, nauli na vitafunwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU NA BUNGE alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, walengwa wa fedha za UKIMWI ni Watanzania wote, wale ambaa wana maambukuzi kwa maana ya kupatiwa huduma ya ushauri nasaha, tiba kwa magonjwa nyemelezi pamoja na dawa za kurefusha maisha (*ARVs*), na Watanzania ambaa hawajaambukizwa kwa maana ya kupatiwa elimu kuhusu kinga dhidi ya maambukizi mapya.

Serikali kuitia *TACAIDS* na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutoa miongozo mbali mbali kuhusu utengenezaji wa mipango na bajeti zinazohusu harakati za kupambana na janga la UKIMWI kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo pia wafadhili.

Halmashauri zote huwajibika kuandaa mipango yao kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na pia mahitaji yaliyopo na yanayoendelea kuibuliwa kwenye maeneo husika kuanzia ngazi za vijiji kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani kuitia mifumo iliyowekwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

Mipango hiyo hupaswa kuzingatia na kutoa kipaumbele katika masuala ya kinga na pia kupunguza athari za maambukizi ya UKIMWI. Kwa kuitia utaratibu uliopo sasa wananchi wengi zaidi wameweza kufikiwa.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huzingatia na hutumia ushauri unaotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika taarifa zake za ukaguzi. Serikali pia huzitumia taarifa hizo katika kurekebisha kasoro mbali mbali ambazo zinakuwa zimejitozea kwenye utekelezaji wa shughuli hizo na kuchukua hatua kwa kuzingatia mazingira na mahitaji halisi.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo inayotumika katika kuandaa mipango ya kupambana na janga la UKIMWI ni ile ile inayotumika katika utaratibu wa fedha za *basket fund*. Aidha, fedha za *basket fund* hutumika pia katika masuala ya UKIMWI.

Kwa kuwa Watanzania walio wengi (zaidi ya 90%) hawajaambukizwa UKIMWI, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba kuna mikakati madhubuti ya kinga dhidi ya janga hili na ambayo kwa utaratibu uliopo kutekelezwa kwa kupitia njia ya elimu na uhamasishaji hasa kwa kuhamasisha wananchi kuacha tabia hatarishi ikiwemo kuwakinga watoto wachanga wasipate maambukizi kutoka kwa akina mama wajawazito, kutibu mapema magonjwa ya zinaa, kuelimisha umma juu ya kutumia kondomu wakati wa kujamiihana. Elimu kwa kuhusu kuepuka ngono zembe, kupima afya mara kwa mara na kadhalika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa, hili suala nimeliuliza nikiwa na ushahidi kamili; Serikali itakubaliana na mimi kwamba ni muhimu ifuatilie na kuhakikisha Madiwani na Watendaji wengine wa Kata wanahuishwa kwenye mpango huu ili kusiwe na utata unaotokea sasa?

Kwa kuwa mpango wa basket fund unaeleza wazi juu ya zile fedha zinazoingia kupitia basket fund, lakini fedha za UKIMWI hapajawa na mwongozo sahihi; Waziri atakubaliana na mimi waende wafuatilie na kusahihisha hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA NA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika kuna ufuatiliaji wa karibu sana wa fedha za UKIMWI katika ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba katika kila Halmashauri kuna Kamati nzito inayoongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ikimhusisha pia Mbunge ambaye hufuatilia masuala ya UKIMWI na pia fedha za UKIMWI zikiwepo hizi za *Global Fund*. Utata unaotokea pengine kwa vile ukaguzi wa fedha za Global Fund hufanyika mara mbili; kwanza, kuna ukaguzi ambao unafanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, lakini pia kuna ukaguzi unaofanywa na Wakala wa *Global Fund* hapa nchini ambao ni *Price Water House Coopers Lybrand*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *basket fund* unaelewaka vizuri kama nilivyoelezea katika jibu la (a) hapo awali kwa vile ni fedha za Serikali na utaratibu wake wa ukaguzi uko wazi, unafanywa na chombo kimoja ambacho ni Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitiza kwamba, kwa kuunda ile Kamati Muhimu ya UKIMWI katika ngazi ya Halmashauri, ni ishara wazi kwamba kuna juhudhi thabiti za Serikali, kwanza kuhakikisha kwamba suala la UKIMWI katika kila Wilaya linazingatiwa na kupewa umuhimu wa pekee ikiwa ni pamoja na kufuatilia kwa karibu sana fedha za Wafadhili ambazo ni kodi ya watu kutoka maeneo mbali mbali duniani kutusaidia. Ahsante sana!

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Kwa kuwa hakuna sheria inayolazimisha *NGOs* walioko Mikoani na Halmashauri kuripoti kwenye Halmashauri, hii ni pamoja na *NGOs* zinazoshughulikia UKIMWI; na kwa kuwa hela za UKIMWI zinazotolewa na Marekani zinakwenda moja kwa moja kwenye *NGOs*, kusababisha hata *TACAIDS* wanashindwa kudhibiti. Je, kuna utaratibu gani wa kufanya hizi hela nyingi ambazo tunazisherehekea ziweze kudhibitiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA NA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika kupambana na janga la UKIMWI katika ngazi ya Wilaya, taasisi zisizo za kiserikali (*NGOs*) katika kupewa fedha zimegawanyika katika maeneo mawili:- Kuna zile ambazo hupata fedha kutoka *TACAIDS* kupitia Halmashauri.

Napenda kusisitiza hapa tena kwamba fedha hizi lazima zifuatiliwe kwa karibu sana na Halmashauri kwa sababu ni fedha za Serikali, zimepitia katika mkondo wa Serikali, zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mchangiaji mkubwa sana katika mapambano dhidi ya UKIMWI hapa nchini kwetu ni Serikali ya Marekani na Serikali ya Marekani inatoa fedha nyingi sana kupitia taasisi zisizo za kiserikali katika kupambana na vita dhidi ya UKIMWI. Serikali ya Marekani hutumia taasisi zake na Ubalozi wake uliopo hapa nchini kufuatilia fedha hizi.

Tunaamini wanafanya kazi hii kwa umahiri na wanahakikisha kwamba zinawafikia walengwa na zinakaguliwa mara kwa mara na sisi hatuna uwezo wa kuwaingilia Wamarekani katika eneo hili.

Na. 69

### **Ubovu wa Barabara za Dodoma**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Dodoma haikunufaika na mradi wa Benki ya Dunia wa kujenga uwezo na kuboresha barabara za mijini kama ilivyofanyika katika miji mingine kutokana na kuwa na chombo muhimu kwa kazi hiyo (*CDA*); na kwa kuwa chombo hicho kilikuwa hakitengewi kabisa fedha za maendeleo ya barabara hadi hivi karibuni, hivyo barabara za mji huo kuwa mbaya sana na zisizostahili kuwepo katika mji wenye hadhi kama Dodoma:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha mradi maalum wenye fedha za kutosha kuendeleza barabara za Dodoma ili zifanane na Manispaa nyingine badala ya kutegemea mgao mdogo inaopatiwa *CDA*?

- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuijengea uwezo Manispaa ya Dodoma ili iweze kumudu kukarabati na kutunza barabara zake kama ilivyozifanyia Manispaa nyingine?
- (c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kwamba barabara za Dodoma Mjini zinazojengwa hivi sasa zitakidhi mahitaji ya usafiri wa umma (*Public Transportation*) ya siku za usoni ili matatizo yaliyoko Dar es salaam yasije yakarudia tena Dodoma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma haikunufaika na mrafi wa *Urban Sector Rehabilitation Project* uliotekelizwa katika Manispaa nane za Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Tabora na Mwanza kwa ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami kwa fedha za Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Dodoma haikuingizwa kwenye mpango huo kwa vile kipo chombo maalum cha Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (*CDA*) ambacho kinashughulikia ustawishaji na maendeleo ya Makao Makuu ya Serikali kikiwa na *Master Plan* ya Mji wa Dodoma iliyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha miundombinu, jukumu la *CDA* ni kujenga barabara mpya katika maeneo mapya. Baada ya kujenga barabara hizo, *CDA* hukabidhi kwa Manispaa ambayo huzitunza. Hivyo, Manispaa ya Dodoma imepunguziwa jukumu la kujenga barabara mpya na kubakiwa na jukumu la kuzitunza. Ili kuwezesha ujenzi wa barabara katika Manispaa ya Dodoma, Serikali imeanza kutenga fedha kama ilivyoelezwa katika jibu la swali Namba 1 la Mheshimiwa Felister A. Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lililojibowi katika Mkutano huu tarehe 8 Aprili, 2008.

Hivyo, kwa sasa hakuna haja ya kuanzisha mradi mpya, isipokuwa *CDA* itaendelea kupewa fedha kwa ajili ya kujenga barabara na Manispaa itaendelea kupewa fedha kwa ajili ya kutunza barabara hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali ni kuijengea uwezo Manispaa ya Dodoma ni pamoja na kuipatia fedha za matengenezo ya barabara kila mwaka. Fedha za matengenezo ya barabara zilizopelekwa katika Manispaa ya Dodoma kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni; mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga shilingi milioni 394.6, mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga shilingi milioni 226.9 na mwaka 2007/2008 Serikali ilitenga shilingi milioni 805.4 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mji wa Dodoma.

Pia, kwa mwaka 2007/2008, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imeipatia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma fedha za kukarabati barabara zeny urefu wa kilomita 1.3 za mjini katika kiwango cha lami na kujenga madaraja ya Kikuyu Kaskazini na Mlimwa kwa gharama ya shilingi 531,400,000/=. Vile vile kwa sasa Manispaa imehakikisha kuwa inaa jiri Wahandisi na Mafundi Mchundo wa kutosha ili ku-*Maintain* barabara hizo.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, brabara za Dodoma mjini zinajengwa kulingana na *Master Plan* ya Mji wa Dodoma. *Master Plan* ya Mji wa Dodoma imeandalisha na kusimamiwa na *CDA*. Ili kukidhi mahitaji ya usafiri wa umma na kuepuka matatizo ambayo yamejitokeza katika jiji la Dar es salaam.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri. Hata hivyo, naomba uniruhusu niulize swalii moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mgawo mdogo wa fedha za matengenezo ya barabara, Manispaa ya Dodoma imeshindwa kabisa kujenga madaraja muhimu kwenye Kata ya Chamwino na pia kwenye Kata ya Nzuguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja haya ni muhimu hasa wakati wa mvua na wananchi wengi wanapata adha kubwa na hata watoto wao mara nyingine wanashindwa kufika shulenii wakati makorongo haya yanafurika wakati wa msimu wa mvua; Je, Serikali iko tayari kutenga fedha maalum katika bajeti ijayo ili madaraja hayo yajengwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunafahamu kwamba kuna madaraja ambayo ni muhimu katika mji wetu wa Dodoma.

Lakini, fedha hizo zimeteengwa katika Halmashauri. Halmashauri ndiyo yenyewe uwezo wa kupanga vipaumbele vyta kujenga madaraja hayo. Kwa hiyo, Serikali inachofanya ni kuwapangia fedha. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Manispaa ya Dodoma imeongezewa fedha takriban asilimia 160, kwa hiyo, ni Manispaa yenyewe kuipa kipaumbele kujenga madaraja hayo hasa ya Chamwino na Nzuguni. Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kuhakikisha kwamba barabara hizo zinaimarishwa na pia madaraja muhimu yanajengwa.

Naomba tu Mheshimiwa Mbunge kama ameliona kwamba hilo ni muhimu sana, angeomba maombi maalum katika Wizara yetu ili tuangalie kwamba tutasaidiana namna gani katika kuimarishe madaraja hayo mawili.

Na. 70

### **Migogoro wa Ardhi na Mashamba**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na matatizo yanayohusu kero za wananchi katika maeneo ya Vijiji na Kata ya migogoro ya ardhi na mashamba:-

- (a) Je, ni kwa kiwango gani Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata yamefanikisha utatuzi wa migogoro hiyo?
- (b) Je, kuna tofauti gani kati ya Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Kata?
- (c) Kwa kuwa kazi ya utawala katika Wilaya na ngazi za chini ni pamoja na kutatua migogoro ya kijamii, lakini sasa kila mgogoro unaelekezwa kwenye Baraza la Ardhi. Je, utawala sasa ufanye nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas P .Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Kata (*Ward Tribunal*) ni chombo ambacho kimeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura ya 206, Rejeo la Mwaka 2002. Mabaraza ya Kata pamoja na kushughulikia migogoro mbali mbali ya kijamii, Mabaraza hayo kwa mujibu wa Sheria ya Migogoro ya Ardhi na Nyumba, Sura ya 216, Rejeo la mwaka 2002, yamepewa uwezo wa kushughulikia pia migogoro ya ardhi. Kwa mantiki hii, Baraza ni moja linalofanya kazi mbili ambazo ni zile za Baraza la Kata na zile za Baraza la Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji yameonyesha ufanisi mkubwa katika kutatua migogoro ya ardhi katika kata na vijiji. Uzoefu unaonyesha kwamba migogoro mingi ya ardhi imetatuliwa katika ngazi za vijiji na kata. Aidha, ipo migogoro ya ardhi ambayo inakwenda kwenye rufaa ikiwa imeanzia kwenye Mabaraza hayo ya chini.

Kwa mfano; katika Wilaya ya Babati, rufaa zinazopelekwa ngazi ya Wilaya kutoka katika vijiji na kata zimeitungua kutoka 114 mwaka 2007 hadi 45 mwaka 2008. Kimsingi, mafanikio ya utendaji kazi wa Mabaraza haya ni kwamba yanapunguza au kumaliza utatuzi wa migogoro ya ardhi na mashamba katika vijiji au kata husika, hivyo, kuwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Usuluhishi yalifutwa kwa Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura 206 ya mwaka 2002 na majukumu yake yamekasimiwa kwa Mabaraza ya Kata. Tofauti kati ya Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Kata inajionyesha katika muundo, majukumu na maamuzi. Kimuundo, Baraza la Kata linaundwa na Wajumbe wasiopungua 4 na wasiozidi 8 ambao hupendekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (*WDC*) kutoka kwenye kata husika. Wakati Baraza la Ardhi la

Kata linatokana na wajumbe waliunda Baraza la Kata wasiopungua 4 na wasiozidi 8, lakini mionganii mwao ni lazima wawepo wanawake 3. Majukumu ya Mabaraza ya Kata ni kutatua migogoro mbali ya kijamii kama vile masuala ya ndoa, makosa madogo madogo ya jinai na pia migogoro ya ardhi. Kwa mujibu wa kifungu cha Na. 11 cha sheria ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba, sura ya 216, Baraza hilo linapokaa na kushughulikia migogoro ya ardhi linaitwa Baraza la Ardhi la Kata iwapo tu kutakuwa na wajumbe wanawake wasiopungua watatu.

Maamuzi yanayotolewa katika Baraza la Kata huthibitishwa na Mahakama ya Mwanzo ambayo pia ni mamlaka ya kusikiliza rufaa zote kutoka kwenye Baraza la Kata. Kwa upande wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata maamuzi yake huwa yamekamilika isipokuwa kama kuna rufaa hupelekwa na kusikilizwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya utawala katika Wilaya ni pamoja na kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinapatikana. Si kweli kwamba katika Wilaya kila mgogoro unaelekezwa kwenye Baraza la Ardhi kwani kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba sura 216, kazi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ni kushughulikia migogoro ya Ardhi tu. Kimsingi vyombo vyote hivi ni vya kisheria na vinafanya kazi kwa kushirikiana na kwa mujibu wa sheria.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa ya ufanuzi kuhusiana na swali hili. Lakini, swali langu ni kwamba, kwa kuwa Mabaraza haya yanafanya kazi kitaalam kwa sababu yanatoa maamuzi muhimu kabisa, lakini hayajawezeshwa, kwa mfano; makatibu wake hawajaajiriwa. Kwa hiyo, kujiendesha kwa Mabaraza haya kunategemea zaidi ada ambazo zinatozwa kwa mashauri yanayoletwa pale kwenye Mabaraza.

Je, ni lini Serikali sasa itaamua kuwawezesha au kuwezesha Mabaraza haya, lakini zaidi kwamba makatibu wa Mabaraza haya waajiriwe mara moja ili kazi hizi zifanyike kwa ufanisi ambao unatarajiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hayo Mabaraza ya Kata mpaka sasa hivi hayajawezeshwa vizuri na ni kweli kwamba inategemea zile faini ambazo zinatozwa katika kuendesha au kusuluhiha migogoro mbali mbali. Ni nia ya Serikali ya dhati kabisa kuyaimarisha hayo Mabaraza ili yaweze kuimarka na yaweze kujitegemea. Kwa hiyo, natoa wito tu kwa Halmashauri, kwa kuwa hicho chombo kiko chini ya Halmashauri, ni kuyawezesha hayo Mabaraza ya Kata hasa tunajiimarisha kwa ujenzi wa ofisi za Kata ili kuwe na ofisi maalum ambayo inaweza kushughulikia masuala hayo ya migogoro ya ardhi na masuala mbali mbali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Mabaraza ya Ardhi na pia kwenye Mabaraza ya Kata.

**MHE. DR. WIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali fupi la nyongeza kama ifuatavyo:- Kwa kuwa Mabaraza haya yamefanya kazi nzuri na

yameonyesha mafanikio; na kwa kuwa katika Mabaraza haya kwa hatua tuliyofikia, walalamikaji na walalamikiwa ndio wanaochangia gharama; na kwa kuwa gharama hizi zinafikia maeneo mengine kati ya 10,000/= na 45,000/=; Suala ambalo ni kubwa kuliko hata mahakama ya kawaida. Je, Serikali haioni kwamba hali hii inafanya mahakama haya yashindwe kutekeleza haki hasa kwa walalahoi wa kawaida?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba Mabaraza hayo yanafanya kazi nzuri na kweli wanaoendesha sasa hivi au wanaosaidia shughuli za pale ni wale walalamikaji na walalamikiwa, yaani zile fedha za faini. Faini mpaka sasa hivi kwa *level* ya Kata ni shilingi 10,000/= tu, haizidi hapo.

Kama inazidi hapo, kama ni mgogoro wa ardhi, inaenda mahakama ya Wilaya. Kama ni mgogoro wa kawaida, inaenda kwenye mahakama ya mwanzo.

Kwa hiyo, kwa sheria ya sasa hivi haijambana mlalahoi. Faini kuwa sana ni shilingi 10,000/= tu.

Na. 71

### **Mpango wa Afya ya Msingi – MMAM**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa kipindi cha miaka kumi (2007 – 217):-

- (a) Je, MMAM imejiwekea mikakati gani ya utekelezaji ili kufikia malengo yake?
- (b) Je, ni mambo gani yanayotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo na mpango huo?

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wizara yangu ina Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambao umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka kumi kuanzia 2007 – 2017.

Lengo kuu la MMAM ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya afya ya msingi kwa wote ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi yanafikiwa, Wizara yangu ilipanga na kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- (i) Kuwasilisha mpango kwenye mamlaka husika ili kupata ridhaa ya Serikali.
- (ii) Kufanya tathmini ya upungufu uliopo hivi sasa katika sekta ya afya. Zoezi hili litatuwezesha kupanga vipaumbele vya utekelezaji wa mpango.
- (iii) Kuwaelimisha wananchi na Halmashauri kuhusu mpango huu kwa kutambua kuwa wao ndiyo watekelezaji wakuu wa mpango wenyewe.
- (iv) Kuwashirikisha wadau wetu mbali mbali wa maendeleo.

Aidha, mpango huu umejadiliwa katika Baraza kuu la wafanyakazi wa sekta ya afya ambao unahusisha sekta nyingine, wahisani, mashrika yasiyo ya kiserikali, taasisi binafsi, mashirika ya kimataifa na taasisi za kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wizara yangu iko katika maandalizi ya kuandaa mpango wa mkakati wa tatu wa sekta ya afya utakaoanza mwaka 2009/2010 ambapo mpango wa maendeleo wa afya ya msingi ni sehemu ya mkakati huo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wananchi inakusudia kutekeleza mikakati mbalimbali na baadhi yake ni kama ifuatavyo, kwanza ni kujenga vituo vya kutolea huduma za msingi 4910, kukarabati hospati za Wilaya 50 na kupanua vyuo vya afya 131. Pili kujenga vyumba vya upasuaji mdogo katika vituo vya afya 2100 na kuipatia nyenzo za kutosha za kufanya kazi. Tatu kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kawaida, vifaa tiba, dawa na vitendea kazi vya kutosha katika vituo vya kutolea huduma 3857, Nne ununuzi wa magari ya wagonjwa 1974, magari ya ufuataliaji 7, kliniki za mkoba 70 na pikipiki 1955, uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano kwa wilaya 64 ambazo bado hazina mfumo bora wa mawasiliano, kukarabati na kuvipatia nyenzo za kutosha vyuo Vinne vilivyokuwa vimefungwa vya Tunduru, Kibondo, Nachingwea na Nzega ili kuongeza idadi ya udahili wa watalaamu wa afya, ufundishaji wa watoa huduma ya akina mama na watoto wachanga 5100, walimu wa vyuo 500, ununuzi wa vifaa muhimu vya akina mama na watoto katika Wilaya 114 na uanzishwaji wa huduma

za akina mama nyumbani katika wilaya 69, na mwisho ni kuongeza kasi ya kudhibiti malaria, kifua kikuu na *UKIMWI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa utekelezaji wa mikakati hii pamoa na mingine minge ambayo sijaitaja hapa itasaidia kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya nchini.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kujua kwamba (a ) Je, mpango mzima utagharimu fedha kiasi gani katika utekelezaji wake? (b) Je, fedha hizo ni za ndani au ni za nje?

**NAIBU SPIKA:** Hayo ndiyo maswali ya nyongeza. (*Makof/ Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Omar Ali Mzee, ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niweze kumwandikia Mheshimiwa Mbunge kiasi cha fedha ambazo amezihitaji kwa maandishi kwa sababu sitaweza kukariri idadi ya fedha kwa tarakimu.
- (b) Fedha hizi zitakuwa za ndani ya nchi na zingine toka kwa wahisani.

Na. 72

#### **Malalamiko Juu ya Madaktari na Wauguzi**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI K.n.y. (MHE. RICHARD S. NYAULAWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu huduma isiyoridhisha kutoka kwa Madaktari na Wauguzi katika mahospitali; na kwa kuwa uzembe wa wafanyakazi hao husababisha vifo na ulemavu kwa wagonjwa husika lakini hawachukuliwi hatua zozote hata pale zinapoundwa Tume kuchunguza mienendo yao:-

- (a) Je, kumekuwepo na malalamiko na kesi zilizofunguliwa na wananchi kwa kipindi cha miaka 2005/2006 na 2006/2007?
- (b) Je, Serikali imechukuliwa hatua gani kuwafunza wananchi waelewe haki yao ya kuwachukulia hatua Madaktari na Wauguzi pale uzembe unapotokea?

- (c) Je, Serikali inaweza kuunda chombo huru kitakachosimamia mwenendo na hatua za kinidhamu dhidi ya uzembe wa Madaktari na Wauguzi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna malalamiko mengi toka kwa wananchi kuhusu huduma zisizoridhisha kutoka kwa madakatari na Wauguzi.

Kwa usahihi wa taarifa na kumbukumbu naomba kulifahamisha Bunge lako tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa wanaolalamikiwa ni baadhi tu ya Madakatari na Wauguzi na siyo wataalamu wote katika fani hizo. Wapo pia Madaktari, Wauguzi na wataalamu wengine wa fani za afya wanaotambuliwa, husifika na kuheshimiwa kwa utoaji wao wa huduma bora na za kitalaam kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge lenye vingele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/2006 hakukuwa na malalamiko yoyote yaliyori potiwa kuwahuusu madaktari na kuwasilishwa kwenye Baraza la Madaktari. Mwaka 2006/2007 kulikuwa na malalamiko yaliyowahuusu Madaktari wawili.

Kufuatia uchunguzi uliofanywa na Baraza la Madaktari juu ya malalamiko hayo, iliamuliwa kwamba Daktari mmoja aliye husika katika malalamiko hayo arudie mafunzo kwa vitendo kwa mwaka mmoja na Daktari wa pili alisimamishwa kazi kwa muda wa miezi sita (6).

Kwa upande wa Wauguzi mwaka 2005/2006 kulikuwa na malalamiko manne yaliyori potiwa na kushughulikiwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga. Malalamiko hayo yaliwahuusu jumla ya Wauguzi wanane na matokeo ya uchunguzi ni kama ifuatavyo:-

1. Wauguzi watatu walipatiwa adhabu ya onyo kali na kufanya kazi chini ya uangalizi.
2. Wauguzi wawili walipewa adhabu ya kusimamishwa kazi kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu.
3. Muuguzi mmoja alifutwa kwenye daftari la orodha ya Wauguzi na wakunga nchini.

4. Wauguzi wawili hawakuchukuliwa hatua yoyote baada ya kuonekana hawana shauri la kujibu.

Mwaka 2006/2007 jumla ya malalamiko sita dhidi ya Wauguzi yaliripotiwa na kushughulikiwa na baraza la Wauguzi na Wakunga. Matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo; wauguzi watano (5) walismamishwa kazi kuanzia miezi (6) mpaka miaka miwili, Wauguzi watatu walipewa onyo kali, Wauguzi watatu walionekana hawana hatia na hawakupewa adhabu yoyote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia programu ya maboresho katika sekta ya umma awamu ya kwanza iliwaelimisha na kuwaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya juu ya kuandaa mkataba wa huduma kwa mteja (*Client Service Charter*) ambao kimaudhui zinaainisha haki na wajibu wa mteja kuhusu huduma zinazotolewa.

Pia unatoa taarifa ya jinsi ya kutoa malalamiko endapo mteja hajaridhika na huduma itolewayo. Aidha Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa wanakumbushwa kila mwaka wakati wa mikutano yao, kuhusu kuwaelimisha wananchi juu ya haki na wajibu wao mara wanapobaini kutoridhishwa na huduma wanazopewa au uzembe wa aina yoyote unapotokea.

Hii ni pamoja na kuishirikisha *TAKUKURU* kufika katika hospitali kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwakumbusha Waganga wa Wilaya na Mikoa wahakikishe wanaandaa mkataba wa huduma kwa mteja na kuwaelimisha wananchi kuhusu mikataba hiyo. Aidha naomba wananchi kutoa taarifa kwa uongozi wa hospitali moja kwa moja au kutumia masanduku ya maoni yaliyowekwa katika hospitali mara uzembe unapotokea au kama hawaridhiki na huduma inayotolewa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, Baraza la Madaktari la Tanganyika (Tanzania Bara) na Baraza la Wauguzi na Wakunga ni vyombo huru vya kisheria vyenye mamlaka ya kushughulikia makosa ya kitaaluma ya Madaktari na Wauguzi. Makosa mengine ya kinidhamu hushughulikiwa na mamlaka zao za ajira kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza; nataka kujua kama kuna sheria ambayo inawalinda wagonjwa ambao wanaweza wakapata madhara kutohana pengine na uzembe ambao unaweza ukasababishwa na Madaktari au Wauguzi na kama haupo. Je, Serikali haitaona umuhimu wa kuileta hapa Bungeni ili tupitishe?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kumpongeza Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa majibu mazuri aliyotoa, ningependa nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sheria mahususi ambayo inatamka kwamba wagonjwa wasiporidhika walalamike kwenye vyombo, kuna sheria ya wananchi katika fani mbalimbali katika Wizara mbalimbali ambazo kama hutaridhika na ulivyonendewa katika Wizara mbalimbali basi kuna vyombo ambavyo unaweza kwenda ili kupata haki yako. Lakini kwa sasa hatujaona sababu kwamba itungwe sheria maalum kwa ajili ya wagonjwa peke yao.

Na. 73

### **Sheria ya Kulinda Haki za Mtoto**

#### **MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O aliuliza:-**

Kwa kuwa, mchakato wa utayarishaji wa Muswada wa sheria ya watoto ulifanyika muda mrefu na hadi leo hakuna sheria iliyotungwa kulinda haki za watoto:-

- (a) Je, ni sababu gani za msingi zilizofanya Muswada usiletwe Bungeni ili kuwezesha kuwepo na sheria ya Watoto?
- (b) Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Muswada huo Bungeni ili kuwezesha kuwepo na sheria ya watoto?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO aliibuu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, Ningependa kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa nichukue fursa hii na kwa niaba wananchi wa wanawake wa Morogoro ambao ndiyo wapiga kura wangu, kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa majukumu ya ziada kuwatumikia wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) na kabla ya jibu napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria ya watoto umechukua muda mrefu. Mchakato huo umeenda sambamba na maandalizi na marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Muswada wa Sheria ya Mirathi na Urithi ya mwaka 2002 *chapter 352 (RE)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Waheshimiwa Wabunge watakulaliana nami kwamba wa asili yake sheria hizi tatu zinahusu masuala yanayogusa maisha ya kawaida pamoja na mila na desturi za jamii. Masuala hayo ni pamoja na haki za watoto, haki za

mzazi, haki za wanawake, haki ya kupata na kumiliki mali, utaratibu wa kuandika wosia na taratibu za kurithisha mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na unyeti wa masuala niliyoeleza, umakini mkubwa na muda wa kutosha unahitajika katika mchakato mzima wa maandalizi. Aidha Serikali inaamini kwamba wananchi wengi zaidi wanastahili kuhusishwa katika mchakato wa maandalizi.

Hivyo basi, hizi sasa Serikali inaendelea na mchakato utakaowezesha wananchi wengi kutoa maoni yao katika maeneo mahususi yaliyoainishwa katika muswada wa sheria ya watoto (*whitepaper*) mchakato wa *white paper* huu unaratibiwa na kuendeshwa na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za msingi zilizosababisha muswada wa sheria ya watoto kutowasilishwa Bungeni ni kutokamilika kwa mchakato wa maandalizi kama ukusanyaji wa maoni ya wananchi. Wizara ya Katiba na Sheria inafanya maandalizi ya mchakato wa *White paper*

(b) Mheshimia Naibu Spika, Serikali itakuwa tayari kuuleta Muswada wa sheria ya watoto Bungeni mara tu baada ya Wizara ya Katiba na Sheria kukamilisha hatua zote zilizobakia za utayarishaji wa Muswada huo.

Muswada wa sheria ya watoto ni moja ya miswada ya sheria ambayo imepewa kipaumbele kuwasiliashwa Bungeni mapema iwezekanavyo baada ya kukamilisha mchakato wa kukusanya maoni ya wadau kuititia zoezi la *White paper*.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambapo ni mara yake ya kwanza kujibu hapa Bungeni.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kukosekana kwa sheria hii watoto wengi hasa wale watoto amba ni wakuu wa kaya, watoto amba wanalelewa na wazee na amba wanalelewa na amba wanalelewa na wagonjwa wamekosa haki zao za msingi.

Je, Serikali itakuwa tayari kuanza kuwasaidia watoto hawa kupata mahitaji yao muhimu, kwa sababu wamekuwa wakitegemea jamii pamoja na watoa huduma amba hawana uwezo?

(b) Kwa kuwa, shirika la umoja wa mataifa la kuhudumia watoto la *UNICEF* kila mwaka linatoa taarifa ya hali ya watoto Duniani na hapa nchini je, Wizara itakuwa tayari kuleta taarifa hii ya hali ya watoto nchini ili iweze kujadiliwa hapa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mng'ong'o kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na janga la *UKIMWI* na matatizo mengine tumekuwa na watoto wengi sana ambao wanahudumia wenzao katika familia na hao tunasema kwamba wamekuwa ni wakuu wa kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi Serikali imeanzisha mpango wa kuwa na Kamati za kuhudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zinaitwa *MVCC* katika kila kijiji na kupitia Kamati hizi Serikali inahakikisha kwamba hawa watoto wanapata msaada kwanza kutoka katika jamii wanakoishi na pili kupitia kwa mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kupitia mpango wa *Global Fund* ambao sasa umetapakaa katika Wilaya zilizo nyingi.

Mwisho kabisa ni kwamba hizi *MVCC* ziko chini ya Kamati za kudhibiti *UKIMWI* za Wilaya ambazo Mwenyekiti wake ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, hivyo basi Halmashauri zetu zimeshirikishwa katika kuwasaidia hawa watoto kupitia kwenye Kamati za *MVCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu taarifa ya *UNICEF*, mimi napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu hii taarifa ya *UNICEF* itakuwa imeletwa katika Wizara yetu naomba nimshukuru kwamba tutahakikisha kwamba hii taarifa itakapoletwa kwetu na sisi tutafanya mpango wa kuileta Bungeni ili Wabunge waweze kujua hali ya watoto katika nchi hii kwa sababu Wabunge ni wadau muhimu ambao ninaamini kwamba kama kweli wataamua kulivalia njuga tatizo la watoto basi watoto wa nchi hii wote watakuwa wanapata huduma zilizo bora na za uhakika.

Na. 74

#### **Tatizo la Ukeketaji Nchini**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la ukeketaji linaendelea kwa baadhi ya Mikoa kama Dodoma, Singida, Manyara na kadhalika.

Kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa tatizo hilo linaongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 43 Mkoa wa Singida:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo hilo kama siyo kulimaliza?

## **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbune kuwa tatizo la ukeketaji linaendelea kwa baadhi ya Mikoa kama vile Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro na kadhalika.

Aidha, ni kweli kuwa takwimu za ukeketaji zilizopo zinaonyesha kuwa katika Mkoa wa Singida tatizo la ukeketaji limeongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 43. Katika utafiti uliofanywa na *DHS* wa mwaka 2004/2005 ukeketaji Kitaifa umeshuka kutoka asilimia 18 hadi 15. Baadhi ya Mikoa imeonekana kuwa ukeketaji umeshuka na Mikoa mingine umepanda, kwa mfano katika Mkoa wa Mara ukeketaji umeshuka kutoka asilimia 44 hadi asilimia 38.

Mkoa wa Kilimanjaro umeshuka kutoka asilimia 37 hadi asilimia 25.4, Morogoro ukeketaji umeshuka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 18, Mkoa wa Iringa umeshuka kutoka asilimia 27 hadi kufikia asilimia 22.7 Mkoa wa Arusha kabla haujtanganishwa kuwa Mikoa ya Arusha na Manyara ulikuwa unaongoza kwa asilimia 81. Baada ya kutenganisha Mkoa wa Manyara ndio unaongoza kwa asilimia 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukeketaji limekuwapo tangu muda mrefu na bado lipo katika baadhi ya jamii kuendelea kuzikumbatia mila ambazo ni potofu. Hivyo kulipunguza au kulimaliza tatizo hili kunahitajika juhudzi za pamoja na ni mchakato utakaochukua muda mrefu ili kuutokomeza kabisa ukeketaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mikakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali ni pamoja na kuunda Idara ya Maendeleo ya Watoto mwaka 2003 yenye sehemu kuu mbili; maendeleo ya Familia na Maendeleo ya Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya familia ndiyo yenye jukumu la kuandaa Sera ya Maendeleo ya Familia ambayo moja ya majukumu yake ni kuondoa mila zenye kuleta madhara kwa wanawake na watoto wa kike kama vile ukeketaji, ndoa za utotoni na ukatili dhidi ya wanawake.

Serikali imetunga Sheria ya Makosa ya Kujamiana mwaka 1998 sehemu 169 (I) inayokataza ukatili dhidi ya watoto, yakiwemo ukeketaji. Sheria hiyo kwa kifupi inasema kwamba mtu ye yeyote atakayepatikana na kosa la kumkeketa mtoto wa kike chini ya miaka 18, anaweza kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka 5 na sio zaidi ya miaka 15 au kulipa faini isiyozidi laki tatu au vyote na anapaswa kulipa fidia kwa muathirika kwa maamuzi ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ndiyo inayosajili na kuratibu Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali *NGOs* ambayo ndiyo yanayosaidia kuondoa mila zenyenye kuleta madhara kama ukeketaji na inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa *NGOs* hizo kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Serikali imeweza kuandaa mpango wa Taifa wa miaka 15 (2001 – 2015) wa kutokomeza ukeketaji. Wadau mbalimbali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka katika Mikoa inayoendelea na ukeketaji mwaka 2002 walipatiwa mafunzo kuhusu Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 Wizara yangu ilizindua Tawi la mtandao wa Kanda ya Afrika ya Mashariki wa kutokomeza ukeketaji na iliunda Sekretarieti ya Taifa ya kutokomeza ukeketaji yenye wajumbe 15 kutoka Serikalini na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine, Wizara yangu imeandaa programu ya kuelimisha na kuhamasisha mahakimu wa Wilaya, Polisi Wilayani, Madaktari wa Wilaya na wataalam wa maendeleo ya jamii Wilayani na Mikoani kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998. Tarehe 17 – 19 Januari, 2007 Wizara yangu iliendesha warsha kwa wataalam walijotajwa kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Aidha, ilitoa mafunzo ya kutokomeza ukeketaji kwa Maafisa wa Polisi, wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Mahakimu wa Wilaya ya Simanjiro, Babati, Arumeru, Ngorongoro, Manispaa ya Moshi na Rombo na wajumbe wa Sekretarieti ya Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Wizara inaendelea kutoa mafunzo haya kwa awamu katika maeneo ambayo mafunzo haya hayajatolewa.

Wizara yangu ina mpango wa kuendelea na mchakato wa kuhamasisha viongozi wa kimila na Mashirika ya Dini katika maeneo yanayoendeleza ukeketaji ili washiriki kikamilifu katika kupinga na kukemea ukeketaji, Kuendelea na mchakato wa kuzifanya marekebisho Sheria ya Makosa ya Kujamiana ili kosa la ukeketaji na adhabu yake iwekwe wazi zaidi na kuwepo na uzito unaostahili.

Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kupambana na tatizo la ukeketaji nchini kwa kushirikiana na umoja wa Mashirika yanayopinga ukeketaji Tanzania. Naomba nichukue nafasi hii niweze kuyashukuru mashirika haya, Serikali inatambua na kuthamini mchango na juhudhi za mashirika ya kiraia yanayopinga ukeketaji hapa nchini. Hivyo ninapenda kuyashukuru Mashirika yafuatayo: Baadhi ni AFNET, DIAL, LHRC, NAFGEM, TAMWA, TAWLA, World Vision, WOWAP na CCT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, viongozi wa Serikali ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata, Vijiji, Waheshimiowa Madiwani, viongozi wa kimila na vyama

vya siasa kuunga mkono juhudzi zinazofanywa na Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika vita vya kutokomeza ukeketaji nchini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Huu ndiyo mfano mzuri wa maswali na majibu marefu, Mheshimiwa Chilolo, kanuni inaniambia nimwite tu Chilolo kwa sababu sina namna. (*Kicheko*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili mafupi sana.

- (a) Kwa kuwa watu wanaoendeleza ukeketaji wamejificha sana. Je; Serikali itakuwa tayari kuruhusu jamii kupiga kura ili watu hawa waweze kujulikana?
- (b) Kwa kuwa, Mkoa wa Singida kuna mashirika yasiyokuwa yakiserikali yalikuwa yanasaidia sana kutokomeza ukeketaji, na masharika haya yamepungukiwa na fedha kwa mfano AFNET. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia mashirika hayo ili yaweze kutokomeza ukeketaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hao wakeketaji wamejificha sana hata wale ambao wanapeleka watoto wao kufanyiwa hilo zoezi wanalifanya kwa siri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kusema kwamba ni vema tukafanya juhudzi za kuweza kuelimisha jamii kwamba hilo ni tatizo ambalo linawanyanyasa wanawake na jambo la pili hata kama tutapiga kura ni kwamba tutaanza kuweka hali ya kuwa na uhasama ndani ya jamii lakini ni vema jamii ikajua kwamba ni kitendo kibaya wazazi wakaacha kuwapeleka watoto wao kwa Mangariba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili amezungumzia NGO'S ambazo zimepungukiwa na fedha. Ni kweli shirika la AFNET limetoa taarifa kwamba halina pesa za kutosha kufanya kazi katika Mkoa wa Singida ndiyo sababu walipunguza ile kasi ya kuhamasisha kampeni yao dhidi ya ukeketaji. Kwa sasa hivi kuna mtandao ambao ni kati ya *World Vision*, *AFNET* na *CCT* ambao utakuwa unafadhiliwa na shirika la *Norwegian*

Christian Aid, ambao watawapa pesa kufanya kazi kwa muda usiopungua miaka saba katika Mkoa wa Singida na mpango huu utaanza mwezi wa mei, 2008.

**NAIBU SPIKA:** Nakupongeza Mheshimiwa Waziri ni kwa kuwa ni mara yako ya kwanza kujibu maswali.

Na. 75

### **Kiwanja cha Ndege cha Songea**

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLO (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kiwanja cha ndege cha Songea kimeshindwa kutoa huduma ya usafiri wa ndege, moja ya sababu ikiwa ni kukosekana kwa kisima cha kujazia mafuta ya ndege.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa inakosa mapato ambayo yangeingizwa kupitia abiria na utalii wa Ruvuma kama vile mbuga za Selous?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA K.N.Y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imekuwa ikikosa mapato kutokana na kusitishwa kwa huduma za usafiri wa ndege katika Kiwanja cha ndege cha Songea hasa ikizingatiwa kwamba kiwanja hicho kipo karibu na vivutio vya utalii kama vile mbunga ya wanyama ya Selous ambapo kiwanja kingeweza kutumika kwa safari za watalii kwenda mbugani.

Kusitishwa huku kulitokana na kukosekana kwa abiria wa kutosha na pia kutokana na ukosefu wa huduma za mafuta ya ndege katika kiwanja . Aidha, Kuwapo kwa usafiri unaoaminika kwa njia ya barabara kati ya Dar es Salaam na Songea, kumefanya wasafiri wengi wakiwemo wafanyabiashara kutumia usafiri wa mabasi kwenda na kurudi Dar es Salaam badala ya usafiri wa anga. Hata hivyo ndege binafsi za kukodisha na zile za mashirika ya dini zimekuwa zikitumia kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiyashawishi makampuni binafsi ya ndege kutumia kiwanja hicho. Hata hivyo mafanikio yamekuwa madogo kutokana na kukosekana kwa kituo cha mafuta katika kiwanja cha ndege cha Songea. Ukosefu wa kituo cha mafuta unalazimisha ndege zinazokwenda Songea kubeba mafuta ya kutosha

safari ya kwenda na kurudi na hivyo kupunguza uwezo wa ndege kubeba abiria au mizigo.

Serikali pia imekuwa ikiyashawishi makampuni binafsi kuanzisha huduma ya mafuta ya ndege katika kiwanja cha ndege cha Songea; na kwa sasa mchakato wa kumpata mfanyabiashara ambaye ameonyesha nia ya kuanzisha huduma hiyo muhimu ya mafuta unafanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*) kulingana na sheria na kanuni zilizopo za kutoa huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaamini kwamba mara baada ya huduma ya mafuta itakaporejeshwa katika kiwanja cha ndege cha Songea, makampuni binafsi yatarejesha huduma za usafiri katika kiwanja hicho na yale ya kitalii yaendayo katika mbuga ya wanyama ya seleous, yataongezeka na hivyo kuiongezea Serikali mapato.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa majibu mazuri ambayo Waziri ameyatoa. Mheshimiwa Naibu Spika nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma sasa wamekuwa wakililia sana huduma ya usafiri wa ndege na ahadi ya Serikali imekuwa ya muda mrefu, tungependa kusikia kauli kutoka kwa Waziri kwamba ni lini sasa huduma ya ndege itaanza kwa Mkoa wa Ruvuma.

(a) Kwa kuwa, watu wa *Precision Air* walishaahidi kufanya kazi zao kuanzia mwaka 2006 na tayari walishafika katika Mkoa wa Ruvuma na wakaanza michakato mbalimbali ya kuanzisha huduma hiyo.

Lakini ghafla bila maelezo yejote kwa wananchi shirika hili la *Precision Air* halijaendelea na mchakato wake, tungependa kujuu kwa nini shirika hili limeacha mchakato wake wa kuanza safari za ndege katika kiwanja cha Songea.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda nijibu maswala mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Likokola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la Msingi, mashirika ya ndege yapo tayari isipokuwa hakuna kituo cha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama tunavyojua kwamba maswala ya ku-supply mafuta tumeyachia sekta binafsi ifanye shghuli hizi.

Kwa hivyo nimwombe Mheshimiwa Likokola kwa kushirikiana na uongozi watusaidie kupata mtu ambaye yupo tayari kuwekeza katika kuendesha masuala ya

mafuta. Hapo suala la mafuta litakapopata ufumbuzi *Precision Air* na ndege zingine zitafanya huduma zake Songea ipasavyo.

Na. 76

### **Barabara ambazo hazijakamilika Mkoani Mbeya**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Zelezeta-Isansa-Itaka; hakuna barabara kati ya Kijiji cha Magamba na Iporoto (na ile barabara ya Msangano-Utambalila – hakuna barabara kabisa) zinaonekana kuwa zimekamilika lakini ukweli ni kwamba hazijaunganishwa:-

- (a) Je, ni lini Serikali kupitia *TANROADS* itaziunganisha barabara hizo kama zilivyoonyeshwa kwenye mtandao wa barabara za Mkoa wa Mbeya?
- (b) Kwa kuacha kuunganisha barabara hizo. Je, Serikali haioni kuwa inachangia katika kudidimiza uchumi wa maeneo hayo na usafiri kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Wenston Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki, lakini kabla ya kujibu swalii hili naomba nitoe maelezo yafuatavyo:-

Barabara za Selezeta-Isansa-Itaka na ile ya Igamba-Msangano-Utambalila ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Ni kweli kuwa barabara hizi hazijakamilika, kwa maana ya kuwa zina vipande katikati ambavyo havipitiki wakati wa mvua na vinahitaji matengenezo makubwa ya kunyanya tuta la barabara na kujenga madaraja. Hali ya barabara hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Zelezeta-Isansa-Itaka: Barabara hii ina jumla ya kilometra 39.44 na inapitia vijiji vya Zelezeta, Isansa, Magamba, Iporoto, Hangomba, Iseche hadi Itaka.

Sehemu ya barabara hii kuanzia Zelezeta hadi Hangomba (*NAFCO*) na Iporoto hadi Itaka zilifanyiwa ukarabati kupitia Mradi wa *CRRRP (Core Rural Roads Rehabilitation Programme)* ambao ulikamilika mwaka 1999. Kipande chenye urefu wa jumla ya kilometra 8 kuanzia Hangomba (*NAFCO*) hadi Iporoto hakikuhusishwa kwenye mradi huu. Barabara katika sehemu hii inapitia katika tambarare tepetepe hususan wakati wa mvua.

Hivyo ujenzi wake unahitaji kunyanya tuta na kujenga makalvati. Gharama za ujenzi wa sehemu hii kwa sasa kwa kiwango cha changarawe zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 290.

(ii)Barabara ya Igamba – Msangano – Utambalila. Barabara hii ina jumla ya kilometa 87.21 na inaonekana haijakamilika kwa kuwa sehemu ya barabara hiyo kati ya Msangano na Tindingoma yenye urefu wa kilometa 25 inahitaji matengenezo makubwa yanayogharimu fedha nyingi.

Kipande hiki pia hupitia sehemu za mbuga ambayo hujaa maji wakati wa mvua na hivyo kuifanya barabara hiyo kutopitika kabisa wakati wa masika. Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe katika eneo hili unahitaji kunyanya tuta la barabara kwa kina kisichopungua mita moja na kujenga madaraja makubwa matatu katika mkondo wa maji. Gharama za ujenzi wa sehemu hiyo kwa sasa zinakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi milioni 1,425.

Kutokana na gharama za kujenga sehemu hii kuwa kubwa, *TANROADS* kwa kushirikiana na wadau wengine wa eneo hilo (akiwemo pamoja na Mheshimiwa Mbunge) inaangalia uwezekano wa kuchepusha (*re-alignment*) barabara hiyo ipitie eneo la mwinuko na kuunganisha moja kwa moja na Kijiji cha Msangano na Tindingoma. Kwa kufanya mchepuo, gharama za kujenga sehemu hiyo zinakadiriwa kupungua hadi kufikia nusu ya gharama ya matengenezo kwa kufuata barabara iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya napenda sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Wenston Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kutounganishwa kwa barabara hizo, kuna athari kiuchumi na usafiri na maeneo husika, hata hiviyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea na jitihada ya kuhakikisha kuwa barabara hizi zinaunganishwa na kuimariswa kadri bajeti itakavyoruhusu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tatizo ni bajeti na kwamba barabara hii itawekwa katika mpango kadri ya pesa zitakavyoruhusu au bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

Sasa kwa sababu tuko kwenye bajeti ya Serikali. Je Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vizuri wakaweka pesa kwa ajili ya kuanza matengenezo ya barabara hizi?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Spika, hapajawa na barabara kabisa katika maeneo haya ambayo nimeyataja kwenye swali la msingi katika maeneo hayo kwa maana ya kijiji cha Magamba na Iporoto na Kijiji cha Msangano mpaka Tinding'omba na baadaye Utambalila. Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza akatueleza nini mpango wa Serikali madhubuti kabisa wa kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapitika? Ningependa pia Serikali ijue kwamba maeneo hayo hayapitiki kabisa kinyume na Mheshimiwa Waziri ambavyo anataka kuwaeleza wananchi kwamba yanapitika.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**(Kn.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi barabara hizo hazipitiki kutokana na mvua na zinahitaji hela nyingine kutengeneza.

Lakini nafikiri Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara za *TANROADS* za mikoa tunakaa tunapitisha kwenye Halmashauri zetu na Halmashauri ya Mkoa wa Mbeya tarehe 8 mwezi ujao itakutana. Bodi ya Barabara itakutana na tunachosubiri pale ni kupata ruhusa ya Halmashauri ikubali ili tufanye *design* ya kuleta mchipuo, huo uliozungumza mapema. Hivi sasa tunachokifanya tumetenga shilingi milioni 90 kwa matengenezo ya muda maalum na shilingi milioni 83 matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Zambi nikuombe katika Kikao hicho tarehe 8 mwezi wa tano uwepo ili uweke msisitizo. Sisi Wizara ya Miundombinu tunashukuru kwa dhati kabisa kwa juhudhi yako unayofanya katika kufuutilia masuala ya barabara ambazo ndiyo kiungo cha mawasiliano nchini.

Na. 77

#### **Idadi ya Wanawake katika balozi zetu**

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO (K.n.y. MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mkakati wa kuweka usawa wa kijinsia katika Bunge (asilimia hamsini kwa hamsini):-

Je, katika Balozi za Tanzania kuna wanawake wangapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbii, Mbunge wa Chake Chake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wanawake katika balozi zetu ni hamsini na nane (58), kati ya hao kuna mabalozi wanawake wawili wanaotuwakilisha katika balozi za Tanzania London, Uingereza na Nairobi, Kenya. Aidha, kuna mabalozi wanawake wawili wanaotuwakilisha katika Ofisi za kimataifa ambao ni Balozi Liberata Mulamula Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Maziwa Makuu yenye Makao Makuu yake Mjini Bujumbura, Burundi na Balozi Mary Mushi Naibu Balozi, Ubalozi wa Tanzania Nairobi anayeshughulikia Mashirika ya *UNEP* na *UN HABITAT* yaliyopo Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hiyo ya wanawake ni kati ya watumishi 179 walioko ubalozini ambayo ni sawa na asilimia 32.4.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mabalozi wawakilishi katika nchi wanawake ni wawili. Je, mkakati wa kuongeza mabalozi wa *fifty fifty* Wizara iko tayari sasa kuhakikisha mabalozi wa nchi za wawakilishi wa Tanzania wanawake wanapatikana *fifty fifty?* (*Makofî*)

Swali la pili, kwa kuwa mkakati wa *fifty fifty* ni mkakati ambao umeonyeshwa katika Bunge la Jamhuri wa Muungano la Tanzania kuelekea katika *fifty fifty*. Ningependa kujua je katika mkono wa pili wa Serikali, Mahakama, Mahakimu na Majaji je ni lini watafikiwa *fifty fifty* ili kuhimiza swali hili?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri unajibu swali la kwanza tu. Lingine limekwenda nje. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni azima ya Serikali ya kuleta uwiano wa *fifty fifty*. Pamoja na kwamba ni nia ya Wizara yangu kutekeleza azma hiyo. Lakini uteuzi wa Mabalozi hauko chini ya Wizara yangu moja kwa moja isipokuwa chini ya Mamlaka husika.

Kwa hivyo, tumechukua azma hii na kadri tutakavyohitaji kuteuliwa mabalozi nje ya nchi wazo hilo totalizingatia kwa kushauriana ipasavyo. Ni azma ya mamlaka husika pia kuona kwamba wanawake wengi wanatoa huduma zao katika taasisi mbalimbali za Serikali kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanaajiriwa katika taasisi mbalimbali za Serikali ikiwa pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Na. 78

#### **Askari wa JWTZ kukagua leseni za uvuvi**

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA (K.n.y. MHE. HAFIDH ALI TAHIR)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kuwa askari wa JWTZ wana kazi ya kilinda nchi wakati wa vita na vile vile kusaidia shughuli za dharura za kitaifa pale inapohitajika. Na kwa kuwa, kila ifikapo mwezi Oktoba askari wa JWTZ hufanya doria katika fukwe za Ununio, Kunduchi, Mbweni na sehemu zingine kwa madhumujni ya kuangalia leseni za uvuvi na ambapo askari hao kuwapiga wavuvi wenyenye leseni zilizotolewa Zanzibar na kuacha leseni za Tanzania Bara:-

- (a) Je, Sheria gani inayowapa ruhusa askari hao wa JWTZ kuangalia Leseni za uvuvi na kuwapiga wavuvi hao?
- (b) Je, mvuvi akiwa na leseni iliyoolewa Tanzanua Zanzibar au Tanzania Bara haruhusiwi kuvua katika upande mwingine wa muungano?
- (c) Je, Serikali haioni kama mtindo huo unawanyanyasa na kuwanyima haki wananchi wa Tanzania kutumia rasilimali zao?

#### **NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Jimbo la Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone (EEZ)* ya mwaka 1989 kifungu cha 13(a) – (f) na kifungu cha 14 (1) – (5), zinatoa uwezo kwa vyombo mbalimbali vya dola ikiwemo JWTZ (Tanzania Bara) na KMKM (Zanzibar) kusimamia na kukagua shughuli za ki-uchumi zinazoendeshwa baharini ukiwemo uvuvi.

Wizara yangu haina taarifa za askari wa JWTZ kuwanyang'anya leseni pamoja na kuwapiga wavuvi kutoka Zanzibar. Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi pamoja na taasisi nyingine za kiserikali kupambana na uvuvi haramu nchini.

Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) haihusiki moja kwa moja katika kukagua leseni za uvuvi bali husimamia shughuli hiyo ambayo hufanywa na Maafisa Uvuvi walioteuliwa kisheria (*Authorized Officers*).

Kazi hii hufanyika wakati wa operesheni maalum za kupambana na uvuvi haramu pamoja na kudhibiti biashara ya magendo ya mazao ya uvuvi. Endapo Mheshimiwa Mbunge ana ushahidi wa askari kuwapiga wavuvi wenyenye leseni za Zanzibar, tutaomba atufikishie ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi sio la muungano. Kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unayo Sheria ya Uvivi inayosimamia shughuli zote za uvuvi katika maeneo yake. Kwa upande wa Tanzania Bara, Sheria ya Uvivi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2005 ndiyo inayosimamia shughuli za uvuvi na kwa upande wa Tanzania Zanzibar, pia wanayo Sheria ya Uvivi inayotumika kusimamia shughuli za uvuvi Zanzibar. Mvuvi akiwa na leseni iliyotolewa Tanzania Bara au Visiwani anapaswa kuwa na barua ya utambulisho toka mamlaka alikotoka kama ni Bara au Visiwani ili afanye shughuli za uvuvi upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibuwa leseni za uvuvi kutoka upande mmoja wa Jmhuri kutoruhusiwa kutumika kuvua kwenye upande mwingine wa Jamhuri hauwanyanyasi wala kuwanyima haki wananchi wa Tanzania kutumia rasilimali ya uvuvi, kwa sababu endapo wavuvi wa upande mmoja wanaouhitaji kuvua upande wa pili hutolewa barua ambayo hutumika kama kibali cha kuruhusiwa kuvua upande mwingine kama nilivyojibu katika sehemu (b) hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hasa la kuwepo Sheria hizi ni kuzuia uvuvi haramu na biashara za magendo na siyo kuwanyanyasa wananchi.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ni jambo la kawaida linalofanywa na baadhi ya maaskari walioko Kunduchi na ninakubaliana naye Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hakuna hata sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano inayoruhusu uvuvi haramu. Je, unyanyasaji huo ambao wao hawana taarifa, anatoa tamko gani kwa baadhi ya askari wanaofanya hivyo pamoja na wananchi wafanye nini wanaofanyiwa vitendo hivyo?

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leseni ni chombo kilichokubalika katika pande zote mbili za Mungano, inayolipwa Zanzibar ni halali na inayolipwa Bara ni halali. Lakini wavuvi wanaotoka Bara kwenda Zanzibar wao wanaangaliwa tu vifaa vyao, leseni yao, usajili wao na kama hawana vitu vya gharama vya uvuvi lakini tofauti na wanaotoka Zanzibar kuja Bara wao wanapata matatizo na wanatakiwa wakate leseni nyingine. Je, hiyo ndiyo sahihi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali la pili sina hakika ni la kwako. Kwa hiyo, jibu la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyojema katika jibu langu la msingi. Serikali haina taarifa za manyanyaso hayo na kwa kweli kwa kuwa hatuna taarifa tamko pekee tunaloweza kutoa ni kwamba kama kuna mtu mwenye ushahidi alete ushahidi tutaufanya kazi. Lakini askari wetu wataendelea kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa na kufuata nidhamu ya jeshi na kupenda raia wa Tanzania. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyouliza kwamba wavuvi kutoka Zanzibar wanatakiwa kukata leseni mara mbili, ni kwamba nchi mbili hizi zimejiwekea utaratibu wa uvuvi kwamba ambapo mtu kama mtu anatoka Zanzibar anatakiwa aje, anaruhusiwa kuvua kwa miezi mitatu, lakini aonyeshe leseni na utambulisho kwamba sio mvuvi haramu aliyefukuzwa toka Zanzibar halafu vyombo vyake hukaguliwa na zana zingine, baada ya hapo huruhusiwa kuvua, tena mara ya pili tena kwa miezi mitatu huruhusiwa kuvua.

Lakini baada ya hapo ndiyo hutakiwa kukata leseni na nataka kukuhakikishia kwamba hakuna mvuvi kutoka Zanzibar anayekuja hapa na kunyanyaswa na kama mtu yoyote akinyanyaswa tunaomba atuletee ripoti kwenye Wizara yetu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na hatua zitachukuliwa kwa hawa watu amba wananyanyasa ndugu zetu kutoka Zanzibar. (*Makofi*)

Na. 79

#### **Mafao ya Wanajeshi waliostaifu**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa wako askari wa jeshi la wananchi waliostaifu kwa kipindi kirefu kilichopita bila kulipwa mafao yao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya waliokuwa watumishi wa Jeshi ili wajulikane na hatimaye walipwe haki zao na kuondoa malalamiko?

(b) Inapotokea hali kama hiyo ya ucheleweshaji wa kosa la Serikali na kwa kuwa mishahara hubadilika kila mara. Je, hao askari waliosumbuka kwa kutolipwa watafidhiwa vipi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Jimbo la Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa malipo ya mafao ya askari wastaaifu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania umefafanuliwa wazi kwenye Kanuni za Jeshi la Wananchi wa Tanzania na elimu kutolewa kwa maafisa na askari hao kuhusu wastaaifu wenyewe kuititia semina mbalimbali na vitabu vya elimu ya pensheni. Hatua hii imesaidia kuimarkika kwa uelewa wa wastaaifu juu ya haki na wajibu wao. Hivyo kuwezesha maandalizi ya mafao kufanyaika kwa wakati na usahihi zaidi ili Hazina iweze kutoa malipo kwa urahisi.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya waliokuwa wanajeshi yamefanyika na takwimu za waliolipwa na wasiolipwa zinajulikana. Idadi ya wastaaafu wasiolipwa ni ndogo sana na malalamiko yanazidi kupungua kutokana na kuimarika kwa uelewa wa wadau juu ya masuala ya pensheni. Hata hivyo, ucheleweshwaji mdogo wa malipo ya mafao yao ambao ilitokea kabla ya utaratibu wa kutoa elimu ya pensheni kwa wadau, kwa kiasi kikubwa ilitokana na wastaaafu wenyewe kutotimiza taratibu husika zifuatazo:-

(i) Mstaafu kutoelekeza anwani ya mahali anapotarajia kuishi baada ya kustaafu ili mafao yake yaelekezwe huko.

(ii) Picha za mstaafu kutotimia idadi inayohitajika.

(iii) Mstaafu kutochukua hundi ya mafao mpaka inapochacha.

(iv) Mstaafu kufariki hivyo malipo yake kugeuka na kuwa mirathi na ambayo taratibu zake ni ndefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi limekuwa likiwasiliana na washauri wa Mgambo wa Wilaya ili kuwajulisha wastaaafu kasoro zilizopo ili waweze kuzitatua. Tunaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa mstari wa mbele kupeleka ujumbe huu wanapotembelea majimbo yao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio yaliyofanyika hayajabainishi ucheleweshwaji kuwa kosa la Serikali.

Aidha, kanuni ya ukokotoaji wa mafao kama inavyoelekezwa katika taratibu za pensheni na viinua mgongo inatumia mshahara ghafi wa mwisho wa mstaafu, hivyo suala la kubadilika mshahara kila mara baada ya kustaafu haliathiri mafao ya mstaafu.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Katika maelezo yake ameeleza kuwa wastaaafu ambao hawajalipwa ni kidogo sana inaweza kuwa ni hivyo. Lakini hao kidogo watalipwa lini, kwa sababu wako watu wana miaka 10 hadi 15 wako wanaendelea kuteseka hawapati pesa zao. Sasa japo ni kidogo walipwe kwa sababu vinginevyo wataendelea kuteseka mpaka watakufa ibidi hilo la warithi sasa, ambalo limekuwa likisumbua sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Washauri wa Mgambo wako ndani ya Ofisi. Hawa wastaaafu wako mitaani na wengine wako vijijini mbali sana sijui mnaandaa

utaratibu gani kuwafanya hawa walioko vijijini wapate hiyo taarifa ya kuwa labda mafao yao yako tayari ili waweze kuja kuchukua? Vinginevyo wataendelea kuteseka. Naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, wastaifu ambao hatujawalipa ni wachache sana. Naomba kuitia Bunge lako tukufu ili nitoe wito kwa askari wote ambao bado hawajalipwa sehemu yoyote nchini waende wakaripoti mara moja Ofisi za Washauri wa Mgambo katika Wilaya wataelekezwa utaratibu wa kufuata.

Na. 80

### **Shule ya Msingi ya Lohila kupatiwa Umeme**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Msingi Lohila Wilayani Songea, inafundisha watoto wasioona na haina umeme wakati kuna vifaa vyta gharama kubwa ambavyo vinahitaji umeme ili vitumike:-

Je, kwa nini umeme usifikishwe kwenye Shule hiyo hasa, ikizingatiwa kuwa kuna transforma jirani kabisa na shule hiyo ambayo inatumika kurushia matangazo ya Radio Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Msingi ya Walemvu Lohila iko chini ya Manispaa ya Songea. Hadi saasa Shule hiyo haina umeme, Transforma aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge katika swali lake iko umbali kama wa mita 500 hivi kutoka shule hiyo na iko katika eneo la Kituo cha Redio cha *Tanzania Broadcasting Corporation* kilichopo Songea. Umeme unaotoka katika transforma hiyo unatosheleza mahitaji ya kituo hicho tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya *TANESCO* Mkoa wa Ruvuma ilipokea maombi ya kuunganisha umeme katika shule hiyo Julai mwaka 2007. Baada ya kupokea maombi hayo *TANESCO* ilifanya tathimini ya gharama za kuunganisha umeme shulenii hapo ambapo ilibainika kuwa kiasi cha shilingi 11,186,000/= kwa wakati ule zingetosha kufanya kazi hiyo. Gharama hizo zinajumuisha ununuzi wa transforma na ujenzi wa njia ndogo ya umeme kutoka katika eneo ambalo transforma itawekwa ikiwa ni umbali wa mita 200 kutoka shulenii hapo. Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea walijulishwa kuhusu kiasi cha fedha kinachohitahika ili kufikisha umeme shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule hii ina vifaa vya gharama kubwa vinavyotumia umeme na kwa kuzingatia umuhimu wa shule hii, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Manispaa ya Songea tutahakikisha shule hiyo inapatiwa umeme ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), inayohakikisha kwamba Watanzania wenzetu wenye ulemavu hawabaguliwi katika kupatiwa huduma za msingi kama vile elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge sana kwa kufuatalia mahitajhi ya umeme katika Shule hiyo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya elimu kwa Watanzania walemaru nchini. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zulekha swali la nyongeza. Ameridhika, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 81

### **Ongezeko la Ushuru wa Kuvuna Mazao ya Misitu**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa ongezeko la ushuru wa kuvuna misitu ya mbao limesababisha kupanda kwa bei ya mbao kwa watumiaji wa mwisho na kwa kuwa hali hiyo imesababisha wananchi wengi hasa wa vijijini kuamua kukata miti walioyopanda majumbani mwao kwa ajili ya kujengea au matumizi mengine ya kila siku:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa ongezeko hilo la ushuru litaongeza upungufu wa miti na hatari ya kuwepo jangwa?
- (b) Je, kwa nini Serikali isitumie sehemu ya ongezeko la ushuru huu kuwapatia wananchi wa vijijini miche bure ili wapande miti ya mbao kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ongezeko la ushuru wa mazao ya misitu linashabihiana na upunguzaji wa matumizi ya mazao ya misitu na hivyo kutosababisha hatari ya kuwepo kwa jangwa. Kimsingi ushuru wa mazao ya misitu ukiongezeka, miti itakayovunwa ni ile tu itakayohitajika katika soko na hivyo kuzuia matumizi ambayo sio ya lazima na hivyo kulinda misitu yetu ambayo ni vyanzo vya maji na huduma nyingine kama kutengamaa kwa hali ya hewa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za usimamizi wa rasilimali ya misitu nchini ni kubwa ikilinganishwa na mapato yanayokusanya kutokana na rasilimali hiyo.

Hata hivyo, Wizara yangu inashirikiana na wadau wengine kama wana mazingira na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa elimu kwa jamii kuwa misitu ni mali na hivyo kuhamasisha upandaji miti kwa ajili ya biashara na kutunza mazingira. Pamoja na hayo Serikali inahamasisha wananchi kuanzisha vitalu vya miche na kuhamasisha mashirika yasiyo ya kiserikali ili yagharamie uoteshaji na utunzaji wa miche hiyo ili miche iweze kupatikana kwa wingi na kwa gharama nafuu.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kulinda misitu yetu na kwa kuwa mahitaji ya mbao nchi nzima yameongezeka ukitilia maanani kwamba tuna mpango wa nchi nzima wa kuendeleza shule za msingi yaani MMEM pamoja na MMES.

Kwa kuwa ongezeko la ushuru maana yake ni kuongeza bei na Mheshimiwa Waziri amesema nia ya kuongeza ushuru ni kupunguza matumizi. Je, Serikali inapunguza matumizi yepi ya wananchi wanaojenga shule za Sekondari ama matumizi ya ujenzi kwa ajili ya mahitaji yao. Hali hii inasababisha wananchi wakate miti yao ambayo katika maeneo ambayo hayana misitu kama Mwanza na Shinyanga inazidi kusababisha jangwa. Je, swali langu la kwanza Serikali haiwezi kuangalia upya ongezeko la kodi ili ipunguzwe kwa ajili ya kulinda misitu katika maeneo ambayo tayari yana upungufu wa miti kama Mwanza?

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jirani zetu Congo wana miti mingi sana ambayo nafikiri hawahitaji kama tunavyohitaji sisi. Serikali haiwezi kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi kwa ajili ya wafanya biashara wanaoingiza mbao ili tuingize mbao kwa wingi kutoka Congo kuziba pengo la mihitaji ya mbao hapa nchini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu ongezeko la ushuru na malengo yaliyokusudiwa. Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba kusudio lilikuwa ni kupunguza matumizi ambayo si ya muhimu sana. Kuna matumizi mengine kama tunavyojua kwa mfano katika ujenzi, unakuta jengo refu linatumia mirunda, ile miti, matumizi kama hayo ndiyo tunaona pengine siyo ya lazima sana.

Kwa hivyo tulikusudia kupunguza matumizi ambayo siyo ya lazima ibaki tu pale ambapo ni lazima kutumia miti. Lakini pia kama tulivyosema lengo lingine la ongezeko hilo ni kuweka thamani kwenye mazao ya miti ielewewe kwamba miti ni tofauti na hewa. Kwa sasa miti kwa kweli ni mali na inamilikiwa na watu na watu hao ndio tunaotegemea ndiyo wapate mapato ikiwemo Serikali. Kwa maana hiyo, kwa mfano misitu inayomilikiwa na kijiji tunategemea kijiji kitapata mapato kutozwa ushuru kwenye mazao hayo.

Kwa hiyo, lengo lilikuwa ni hilo na si kupunguza matumizi ambayo tumesema kwamba ni ya lazima kama ni ya ujenzi wa shule. Hayo yanaendelea kwa kuzingatia hali halisi.

Kwa hiyo, wazo la kuangalia mfumo wa kodi katika *import* ya mazao ya misitu hasa ya mbao. Ningependa kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli wazo hili ni la kweli na tayari kuna maeneo kwa mfano ya kusini mwa nchi yetu tayari wameanza kuagiza mazao ya misitu kutoka nchi za Kusini kama Msumbiji. Kwa hivi Wizara yangu tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha kujaribu kuangalia namna ambavyo tunaweza tukaangalia eneo hili la mfumo wa kodi ili kurahisisha wafanya biashara wanaopenda kuagiza mazao ya misitu kutoka nje.

Na. 82

### **Kesi za Nyara na wanyama waharibifu kwa mazao**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Pamoja na Serikali kujenga mahusiano na ujirani mwema kwa wananchi waishio kando kando ya hifadhi za Taifa. Lakini bado hawanufaiki vema na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni Hifadhi ya *Maswa Game Reserve* iliyoko Wilaya ya Meatu kwani wananchi wana malalamiko ya kuharibiwa mazao yao na wanyama kama tembo na hawapatiwi msaada wa haraka maeneo ya kilimo na ya mifugo, shughuli za utamaduni kuchukuliwa, kukamatwa na kuwekwa mahabusu muda mrefu bila kosa kusikilizwa na huduma za kiuchumi kuboreshwa taratibu mno:-

(a) Je, ni sababu gani zinasababisha wananchi wenye kesi za nyara kukaa muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa mapema?

(b) Kwa kuwa, msimu wa wanyama waharibifu wa mazao kama tembo unafahamika kwa uzoefu wa maeneo mbalimbali. Je, kwa nini Serikali inasubiri mpaka ipokee taarifa za uvamizi na uharibifu ndipo itume askari wa wanyamapori wakati huo hasara kubwa tayari imeshatokea?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli baadhi ya kesi chache za nyara hukaa muda mrefu bila kusikilizwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi hizi huendeshwa na waendesa mashtaka wa Polisi pamoja na maafisa wanyamapori wenyе mafunzo ya kuendesa mashtaka. Sababu kubwa zinazosababisha hali hiyo ni kuwa makosa yaliyo chini ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*The Wildlife Conservaton Act, Cap. 213 as Revised Edition 2002*) yameainishwa kuwa ni makosa ya uhujumu uchumi chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi (*The Economic and Organized Crime Control Act, Cap. 200 Revised Edition 2002*).

Makosa yaliyo chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi yana utaratibu ambao hauna budi kufuatwa kabla ya kesi hizo kuanza kusikilizwa.

Aidha, kuna upungufu wa waendesa mashitaka wa Wizara kwa kesi za nyara, hali ambayo inaathiri ufuatiliaji uendeshaji na kusababisha ucheleweshaji wa kesi za nyara. Vilevile uendeshaji wa kesi hautegemei tu Wizara yangu pekee kwani kwa ujumla wake zinategemea Mahakama na Idara nyngine za Serikali kama Polisi, Mkemia Mkuu wa Serikali, pamoja na Idara nyngine kulingana na kesi yenye. Hata hivyo, Wizara yangu inapitia upya Sheria ya Wanyama pori na pia inatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa maafisa wanyamapori ili waweze kuendesa kesi za nyara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa mazingira ya uharibifu unaotokana na wanayama wakali au waharibifu, hayatabiriki, na pia kutokana na uhaba wa watumishi, hivyo, Wizara yangu imekuwa ikiweka vituo vya askari wa wanyamapori katika kanda maalumu jirani na sehemu zenyе matatizo ikiwemo Meatu kwa lengo la kuzuia uvamizi wa wanayamapori waharibifu kabla ya uharibifu kutokea. Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto hii Wizara yangu inashirikiana na wadau wengine kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa vijiji vya Sembu, Mbugayabanya, Malwilo, Butuli, Ming'ongwa, Mwasengela, Mwanhongo, ndivyo hasa vilivyoathirika na suala la hifadhi; je, Serikali itatenga lini maeneo ya malisho ya mifugo pamoja na uwindaji kiraia kwa ajili ya kitoweo?

(b) Je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu kuwa kutokana na uanzishwaji wa WMA ikakubali kuingia mita 200 kuanzia mpakani ndani ya hifadhi ya pori la akiba ili kutenga eneo kwa ajili ya hifadhi shirikishi? Na hii kwa ajili ya kupunguza migogoro lakini pia pamoja na kuleta manufaa zaidi kwa wananchi walioko pembezoni mwa hifadhi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wazo lake kwamba Wizara yangu iangalie uwezekano wa kutenga maeneo ya malisho, ningependa kufafanua kwamba maeneo haya ya Meatu ya vijiji alivyovizungumzia yako pembezoni mwa Masa *Game Reserve*. Na ikumbukwe kwamba *Game Reserve* hii katika miaka ya karibuni imewahi kupunguzwa mara kadhaa, kwa hiyo, *pressure* inazidi kuongezeka dhidi ya msitu au dhidi ya pori hili la akiba na si kwamba ongezeko la wanyama au eneo la msitu kwamba linaongezeka. Nafikiri kwamba hapa zinahitajika juhudzi za pamoja, kwa upande mmoja kuangalia idadi ya mifugo ambayo tunayo ili iendane na *carrying capacity* ya maeneo yetu. Kwa sababu hata kama tukirudi nyuma bado tena baada ya miaka 2 wale kaka zangu, ndugu zangu, Wasukuma wenzangu kule najua mifugo yao itaongezeka, wataomba tena eneo lingine. Kwa hiyo, nafikiri hili tuliangalie kwa pamoja. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la utaratibu wa WMA, utaratibu huu umekuwepo kwenye maeneo mengi na ni kweli kwamba maeneo anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, ni moja ya maeneo ambayo Wizaya yangu inayaangalia. Kwa hiyo, kuna mpango ambao tayari uko katika Wizara unaoendelea kwa ajili ya kuangalia namna ya kupata utaratibu ulio bora zaidi wa kutumia maeneo haya kwa ajili ya kupata mazao ya wanyama pori kikiwemo kitoweo. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, suala hili avute subira tunalifanyia kazi Wizarani na muda si mrefu patapatikana kitu ambacho pengine kitakuwa ni cha kutumainisha kwa wananchi wake. (*Makofi*).

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na maswali nimewaburuza yamekwisha. (*Makofi/Kicheko*).

Sasa kuna Mheshimiwa mmoja simtaji jina, amesema hivi: "Mheshimiwa Naibu Spika, salamu sana. Mheshimiwa kwa kuwa baadhi ya Mawaziri na Wabunge huuliza maswali marefu na Mawaziri kujibu kirefu; na kwa vile maswali kwa siku yamepangwa kwa idadi maalumu, ni vema hesabu zikapigwa kujua swali ni dakika ngapi, na majibu ya Waziri yasizidi maneno mangapi. Halafu mwisho kwa mfano, anasema maneno 150 labda mpaka 200. Halafu maswali ya nyongeza yasizidi sekunde, kwa mfano, yeye anasema sekunde 10 au 20." Asante sana, naunga mkono hoja ya kusema maswali ni marefu.

Ni kweli swali, jibu, maswali ya nyongeza na majibu ni dakika tano. Sasa kila swali unakuta kwamba linakwenda mpaka dakika 10, 15. Kwa hiyo, hamna namna unaweza kumaliza maswali 15 kwa dakika zile saa moja na nusu. Na zaidi watu wakianza kuhutubia wenzao, ndio maana nikamwambia Mheshimiwa Mzee pale, ndiyo masuala yanayopaswa. Kwa hiyo, nadhani ushauri huu nitapeleka mahali nako tukajadili ili tuone inakuwaje. Kwa kweli, ni kero kwa sababu mtu anaamua kusema ujuzi wake wote. Huhitaji kusema ujuzi wako wowote kuhusu swali, yaani unasema hata maelezo mengine hayakuulizwa, unajibu tu, unaeleza, haiwezekani! Kwa hiyo, tunaomba sana hili

tulizingatie na sisi kwenye Kamati yetu ya Kanuni tutaweza kuliwekea msimamo. Ama sivyo tunapunguza maswali, badala ya 15 yawe 10, sasa yako yote, ndiyo *alternative*.

Kwa hiyo, Waheshimiwa wote tuzingatie muda. Mawaziri jibu lisizidi *page* moja. Maswali ya nyongeza, wewe unaanza kuhutubia, uliza kama lilivyo swali basi. Kwa hiyo, jamani tuzingatие ama sivyo inakuwa mwenye swali ndiye anauliza swali la nyongeza, hakuna maswali mengine ya nyongeza yanayoruhusiwa. Kwa hiyo, tujue hili na tunajilaumu sisi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na wageni wetu leo. Halafu utaratibu mwininge wageni wote wapelekwe Ofisi ya Spika, siku moja kabla. Mkileta kwenye *vinote* hapa baadaye tutakuwa hatusomi.

Kwa hiyo, tuna wageni wetu katika Bunge hili. Wako wageni wa Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa amba ni wanachama wa Umoja wa Vijana CCM. Ndugu Emanuel Ndule, asimame aliko, na ndugu Thomas Nyembelam. Ni wale pale waliokaa! Wageni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, ni ndugu *Dofin Woodford Trust*, hiki ni chama. *Dofin Woodford Trust Representative of Tanzania for the Woodford Foundation Assisting with a Construction of VTC for Deaf Youths in Moshi Rural District*. Hawa ni John Mwashi *Chairperson of the WAVICA* na ndugu Peter Temu, *Secretary* wa WAVICA na mwalimu wa *Mwanga School for Deaf*, asanteni, karibuni sana!

Nina wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Hawa Ghasia. Yeye ana Mheshimiwa Mwadawa Omari, Katibu wa Umoja wa Vijana Wilaya. Wilaya gani sasa? Mtwara Vijijini! Ndugu Halima Mkango, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya hiyo hiyo na Mheshimiwa Hawa Siri, Katibu wa Jumuiya ya Wanawake, Wilaya ya Mtwara Vijijini. Karibuni sana!

Nilikuwa na wageni wa kwangu, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, *University*, wasimame walipo, wapo. Na wapo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *Saint Johns Dodoma*. Nilikuwa nijue *Presidents* wao, wako na Marais wao hapa, bahati mbaya watu wanaoniratibu hapa hawajaleta vyeo, kwa hivi sijawajua. Kwa hiyo, kuna *Presidents* wao kutoka vyuo hivi. (*Makofi*).

Ndiyo hiyo anasema, wageni wa ziara Bungeni, uongozi wa Serikali ya wanachuo *Saint Johns University of Tanzania, Dodoma*. Waziri wa Habari na Mawasiliano, ndio yupi? Joseph Chitinka, ndio yupi? *Ok!* kuna Waziri wa Fedha, Ndugu John Makwara, kuna Mshauri wa Rais, Ndugu Sophia Nchimbi, unaona mambo hayo! Karibuni! Ndivyo mnavyoanza taratibu ndiyo hivi hivi. Kwa hiyo, mmeona Mawaziri wanavyojibu hapa, nafikiri na nyinyi mnajifunza hayo, asante sana. (*Makofi/Kicheko*).

Matangazo ya kazi! Mheshimiwa Dakta Abdala Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 15 kutakuwa na Kikao cha Kamati saa 5:30 katika Ukumbi chumba Namba 231. Halafu Ndugu Gidion Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangazia wajumbe wa

Kamati yake, kwamba leo tarehe 15 kutakuwa na Kikao cha Kamati saa 5:30 katika ukumbi 219. Halafu Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti Kamati ya Miundombinu, anapenda kuwatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 15 saa 5:00 asubuhi watakuwa na mkutano Chumba Namba 227. Halafu Mheshimiwa Dakta Wilbroad Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anawatangazia wajumbe wake kwamba, nafikiri ni leo pia, maana yake tarehe haikuandikwa, saa tano asubuhi wajumbe wa Kamati yake wakutane chumba Namba 133. Halafu Katibu wa Chama Cha Wanawake wa Bunge, anapenda kuwatangazia wanawake wa Bunge wote, kwamba leo tarehe 15 saa 7.00 mchana wanawake wa Bunge wote wanatakiwa kwenye mkutano kwenye ukumbi wa Pius Msekwa. Mwisho wa Matangazo ya kazi. Katibu!

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa  
Mwaka 2008**  
*(The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*The Social Security Regulatory Authority Bill, 2008*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema baada ya kupata ajali mbaya sana ya gari iliyotokea tarehe 24/09/2007 saa 1:04 jioni Kaliwa, Jimbo la Urambo Magharibi katika Wilaya ya Urambo nikiwa pamoja na wenzangu wanne ambaa sasa ni marehemu, Twaha Ramadhani Ngoso, aliyejewa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Haruna Shamsheli, Diwani wa Kata ya Ushokola, Tarafa ya Kaliwa Urambo, *private* Ramadhani Waziri na *private* Hassan Kiloko, wote hawa ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Brigedi ya Magharibi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahala pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru hospitali ya Wilaya ya Urambo, hospitali ya rufaa Muhimbili, pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa jinsi walivyotuhudumia kwa makini na kwa huruma kubwa. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Urambo Magharibi na pia wananchi wa Wilaya ya Urambo na wananchi wote kwa ujumla kwa jinsi walivyoguswa na kusononeshwa sana na ajali hii pamoja na misiba iliyotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa namna ya pekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunitewe wa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, nikitokea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naahidi kutimiza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais, kwa ufanisi na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Wabunge wenzetu wapya amba ni Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani, Zanzibar pamoja na Kamati nzima ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano wao waliounesha katika maandalizi ya Muswada huu ili kuweka katika ubora uliokuwanao sasa. Nawashukuru pia kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, pamoja na timu yake yote ya wataalamu kutoka Wizarani. Vilevile nawashukuru wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa umakini wao wa kuhakikisha kuwa Muswada huu unazingatia misingi bora ya uandishi wa sheria na pia kwa kutilia maanani ushauri wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishesema awali muswada huu unawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili. Chimbuko la muswada huu ni utekelezaji wa sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 pamoja na maagizo ya Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 7 Novemba, 2007, kuhusu kutungwa kwa sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Katika kikao cha Baraza la Mawaziri, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, iliagizwa ishirikiane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa Muswada huu na kuwasilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini (*The Social Security Regulatory Authority Act, 2008*). Madhumuni ya muswada huu ni kuweka utaratibu wa kusimamia na kudhibiti sekata ya hifadhi ya jamii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hii yametokana na kuwepo kwa umuhimu wa kuwa na mfumo wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii unaoendana na wakati wa sasa. Pamoja na mambo mengine muswada huu unapendekeza kuundwa kwa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini itakayokuwa na jukumu la kusimamia mifuko yote ya hifadhi ya jamii ikiwa ni pamoja na mawakala watakaosajiliwa chini ya mifuko hiyo (*managers and custodians*).

Hali ilivyo sasa ni kwamba hakuna chombo cha kusimamia na kudhibiti hifadhi ya mifuko ya jamii nchini. Wigo wa huduma hizi ni mdogo sana ukilinganisha na idadi ya watu. Vilevile idadi na ubora wa mafao yanayotolewa na mifuko hii ni duni. Aidha, haki ya mafao haihamishiki pindi mwananchama anapohama kutoka mfuko mmoja kwenda mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali kurekebisha hali hii. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini hali ya sekta ya hifadhi za jamii. Kazi hii imefanyika kwa ushirikiano wa wataalamu wa hifadhi ya jamii kutoka ndani na nje ya nchi.

(ii) Kufanya mjadala wa pamoja na wadau wa sekta hii juu ya hatua za kuchukuliwa ili kurekebisha mapungufu hayo. Matokeo ya ujumla ya hatua hizi yalikuwa ni kupitishwa kwa sera ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2003 ambayo pamoja na mambo mengine, inaelekeza kutungwa kwa sheria ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya muswada wa sheria hii ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003. Muswada huu umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuundwa kwa Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii itakayosimamiwa na Bodi ya Utatu, yenyewe wawakilishi kutoka Serikalini, vyama vya waajiri na vyama vya wafanyakazi.

(ii) Vyama vya wafanyakazi na waajiri pamoja na wataalamu wa masuala ya hifadhi ya jamii vitahusishwa kikamilifu katika Bodi itakayosimamia chombo cha kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(iii) Kuwa na utaratibu utakaohakikisha kwamba wafanyakazi wote wanakingwa dhidi ya majanga yanayosababishwa na kupungua au kupotea kwa uwezo wa kufanya kazi. Kila mfanyakazi atatakiwa kujiunga katika mfuko wa hifadhi ya jamii ili aweze kukingwa dhidi ya majanga.

(iv) Kuwa na utaratibu wa kupanua wigo wa hifadhi ya huduma za jamii nchini ili kuwafikia wafanyakazi walio katika sekta isiyo rasmi kama vile wakulima, wavuvi, wachimbaji wadogo wadogo wa madini na wafanyabiashara wadogo wadogo.

(v) Kuwa na kiwango cha chini cha mafao yatakayotolewa na mifuko ya hifadhi ya jamii nchini kwa wanachama wake kwa kuzingatia kipato cha mwanachama na uwezo wa kiuchumi wa mifuko ama Taifa kwa ujumla na kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa ya shirika la kazi la dunia (*ILO*), Na. 102 na 128.

(vi) Aidha, muswada huu umezingatia ukweli kwamba mfuko wa bima ya afya, *NHIF*, una jukumu mahususi la kutoa fao moja tu la matibabu kwa wanachama wake.

(viii) Vilevile kuwa na utaratibu utakaohakikisha kwamba waajiri wa wafanyakazi wote wanachangia mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuinua viwango vyao vya mafao.

(ix) Kuweka utaratibu utakaohakikisha haki ya mafao ya mwanachama haipotei anapohama kutoka mfuko mmoja hadi mwagine au nchi moja hadi nyingine.

(x) Kuwekwa kwa mwongozo utakaohakikisha kuwa mifuko ya hifadhi ya jamii nchini inaendeshwa kwa uwazi na inawajibika kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

(xi) Kuipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kutoa miongozo (*guide lines*), kwa utaratibu shirikishi na kusimamia masuala ya kifedha hususan uwekezaji katika mifuko ya fedha ya jamii nchini.

(xii) Taasisi za hifadhi ya jamii katika taratibu za nyongeza (*supplementary schemes*), kuendeshwa kwa mfumo wa soko huria (*liberalized markets*), utakaowezesha sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma za hifadhi ya jamii.

(xiii) Kuipa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii jukumu la kuratibu mageuzi katika katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

(xiv) Taasisi za hifadhi ya jamii kuendeshwa katika misingi ya bima ya jamii (*social insurance principles solidarity and equity*).

(xv) Kuweka utaratibu utakoabainisha mgawanyo wa majukumu ya wadau wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuandaa mswada huu uliwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, mifuko yote ya hifadhi ya jamii nchini, Benki Kuu ya Tanzania, Taasisi za Elimu ya Juu, wataalamu wa hifadhi ya jamii kutoka ndani na nje ya nchi. Wadau wote kwa pamoja walikubali na kuunga mkono uamuvi wa kutunga sheria ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Bunge lako Tukufu litakubali sheria ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini itungwe, matokeo ya jumla yatakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini itaundwa.

(ii) Sheria zinazounda mifuko ya hifadhi ya jamii na benki kuu zitarekebishwa ili ziendane na sheria hii.

(ii) Kujenga mazingira mazuri ya kupanua wigo wa huduma za hifadhi ya jamii kufikia sekta isiyi rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Bunge lako Tukufu litaupitisha muswada huu kuwa sheria, na Mheshimiwa Rais akaridhia, sheria hii itanza kutumika tarehe 1 Julai, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa. Sehemu ya kwanza inajumuisha mambo makuu matatu ikiwa ni pamoja na jina la sheria yenye, tarehe ya kuanza kutumika, sehemu ambapo sheria hii itatumika na tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika ndani ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya muswada inapendekeza uanzishwaji wa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Sehemu hii inajumuisha vifungu mbalimbali kuhusiana na kazi na majukumu ya mamlaka, uteuzi wa bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, na maofisa wengine wa mamlaka hii. Mkurugenzi mkuu pamoja na maofisa wengine watakaoteuliwa chini ya sheria hii inayopendekezwa watakuwa ndio watendaji wa kazi za kila siku za mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu inapendekeza masharti ya usajili wa mfuko wa hifadhi ya jamii pamoja na mawakala watakaosajiliwa chini ya mifuko hiyo (*managers and custodians*). Pia inapendekeza mazingira yanayoweza kusababisha mfuko au wakala wa mifuko kufutiwa usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inapendekeza vifungu vinavyohusiana na kusimamia na kudhibiti hifadhi ya mifuko ya hifadhi ya jamii na mawakala wa mifuko hiyo. Sehemu hii inapendekeza pia kuweka masharti ya kuutaka kila mfuko wa hifadhi ya jamii kuwasajili wanachama wake wote. Pia sehemu hii inapendekeza vyanzo vya fedha vya kila mfuko pamoja na usimamizi wa fedha hizo. Aidha, sehemu hii inapendekeza uwekezaji wowote utakaofanywa na mifuko ya hifadhi ya jamii au mawakala kuzingatia miongozo ya uwekezaji itakayoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inapendekeza utaratibu wa ukaguzi na uchunguzi katika mifuko ya hifadhi ya jamii katika sehemu inayopendekezwa. Utaratibu utakaofuatwa na mamlaka ya kusimamia na kudhibiti pamoja na benki kuu katika kufanya ukaguzi na uchunguzi katika mifuko, mameneja, na mawakala wa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita inapendekeza mfumo wa kushughulikia migogoro. Sehemu hii inapendekeza kuundwa na kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa la hifadhi ya jamii litakalokuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa zote dhidi ya maamuzi ya mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba inapendekeza vifungu vilivyobainishwa na uhusiano kati ya Mamlaka na Benki Kuu katika usimamizi wa masuala ya fedha. Sehemu hii inapendekeza kazi na uwezo wa Benki Kuu juu ya mifuko ya hifadhi ya jamii, mameneja na mawakala katika kusimamia masuala ya kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane ya muswada huu inapendekeza vyanzo vya mapato vya fedha za mamlaka na matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inapendekeza masharti ya jumla, hususan mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na pia mamlaka ya kutengeneza sheria ndogondogo, (*Rules*). Pia sehemu hii inapendekeza makosa na adhabu chini ya sheria inayopendekezwa. Mwisho, namalizia kwa kuwashukuru wadau wote ikiwa ni pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, chama cha waajiri, na mifuko ya hifadhi ya jamii, kwa maoni na ushauri wao uliochangia kuboresha muswada huu. Pia napenda kulishukuru Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), kwa mchango wake wa ushauri. Aidha, napenda kuwashukuru wataalamu na watendaji wa Wizara zingine na taasisi mbalimbali zilizohusika katika hatua mbalimbali za maandalizi ya muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Asante, hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati au Msemaji wake kuhusu muswada huu. Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Masoud. (*Makofi*).

**MHE. HAROUB SAID MASOUD - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 86(5), Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008 (*The Social Security (Regulatory Authority Bill, 2008)*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza kupata nafasi ya kusema hapa Bungeni baada ya kuchaguliwa tena kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kwa heshima ya pekee nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kunichagua kwa asilimia 100 kuwa Makamu Mwenyekiti wao kwa kipindi kilichobaki cha uhai wa Bunge lako. Heshima hii pia ni kutokana na wananchi wa Jimbo la Koani, Zanzibar, nawashukuru sana kwa imani, ushirikiano na upendo wao kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi kuwa Mbunge wa Jimbo hilo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Al-Shayma John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Nawatakia heri na mafanikio katika kazi hii. Aidha, kwa niaba ya Kamati naomba kutoa salamu za rambirambi na pole kwa wananchi wa Jimbo la Simanjiro na Mkoa wa Manyara kwa ujumla kwa maafa yaliyotokea katika migodi ya *Tanzanite-Mererani*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda uliopatikana Kamati iliweza kuchambua Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008. Kwanza ilikutana Dar- es Salaam kwa siku mbili, tarehe 31 Machi na tarehe 1 Aprili, 2008. Katika Vikao hivyo Wajumbe wa Kamati pamoja na Wadau walijadili Muswada huo na kubaini kwamba una upungufu mbalimbali. Hivyo Kamati kwa kushirikiana na Serikali iliomba kupewa muda zaidi wa kuendelea kufanya kazi ya kuchambua Muswada. Kamati pamoja na Wadau tulifanya vikao mbalimbali kuanzia

tarehe 8 - 11 Aprili, 2008, mjini Dodoma. Tarehe 12 Aprili, 2008 Serikali kuptitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iliandaa semina ya wabunge wote kujadili muswada huu muhimu. Baada ya semina hiyo Kamati yangu ilikutana tena kuanzia tarehe 12-14 Aprili, 2008 kuendelea kuchambua zaidi na hasa kujumuisha maoni na ushauri uliotolewa na wabunge wakati wa semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau walioshirikishwa na Kamati katika kuchambua muswada huu ni pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF, PPF, LAPF, PSPF, GEPF, NHIF*), Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), Umoja wa Waajiri Tanzania (*ATE*), Baadhi ya Wabunge, Benki Kuu, wataalamu na wasomi wa masuala ya Hifadhi ya Jamii na wajumbe wa *Task force* (Kamati kazi) iliyoshiriki kuandaa muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyojadiliwa na Kamati, malengo na maudhui ya Muswada, Kamati imekubaliana kabisa nayo ambapo muswada umelenga kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa kuweka utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa sekta hiyo. Muswada huu umelenga kuwapo na Mfumo wa Kisheria wa kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii unaoendana na wakati. Muswada huu ukipitishwa na kuwa sheria, itakuwa na jukumu la kusimamia Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na Mawakala watakaosajiliwa chini ya mifuko hiyo (*managers and custodians*). Kamati hii inaunga mkono suala hili, kwa sababu kuwepo kwa Mamlaka hii itaweza kuweka misingi imara ya kujenga Sekta ya Hifadhi ya Jamii ili iweze kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua hali halisi ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Sekta hii haina Chombo cha Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini. Wigo wa huduma hizi ni mdogo ukilinganisha na idadi ya Mifuko iliyopo na hata mafao yanayotolewa na Mifuko hii bado ni duni ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyopo katika Muswada huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii yenyе lengo la kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Kamati yangu imejadili muswada, na iwapo utapitishwa kitaundwa Chombo au Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii utapanuliwa kufikia Sekta isiyo rasmi. Hii itakuwa ni hatua kubwa na muhimu sana katika kuleta maendeleo katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano kati ya Sera na Muswada, ilipokutana na wadau Mjini Dar es Salaam, walionyesha wasiwasi mkubwa kwamba sera na Muswada wa sheria unaopendekezwa unatofautiana, sera ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2003 ambayo ilitungwa kwa ajili ya kumaliza matatizo ya mfuko wa hifadhi ya jamii yaliyopo sasa haikuzingatia katika Muswada, badala yake umejikita zaidi katika kudhibiti na kusimamia fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili kwa kina Kamati ilibaini kwamba Muswada umezingatia kwa kiwango kikubwa sera ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2003. Sera hii imebainisha maeneo yenyepungufu ikiwa ni pamoja na kutokuwap kwa chombo cha kusimamia na kuweka uwiano ulio sawa. Hifadhi ya jamii imehusisha watu wachache sana yaani chini ya asilimia sita ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi, sera imeanisha wazi kwamba katika mifuko ya hifadhi ya jamii hakuna miongozo ya uwekezaji, kila mfuko unawekeza kwa kufuata sera zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imepitia Muswada huu na kubaina kwamba umeandaliwa kwa lengo la kuondokana na matatizo ya siku nyingi yaliyoikabili mifuko ya hifadhi ya jamii nchini. Hata hivyo, Kamati inapendekeza baada ya Muswada kupitishwa na kuwa sheria na kuundwa kwa mamlaka ya udhibiti zifanyike tafiti mbalimbali ili kuweza kufanya mageuzi makubwa katika sekta hii. Mamlaka ya udhibiti iweke misingi ya kuongeza idadi ya wanachama, sekta hii inazo fedha nyingi sana zikitumiwa vema zitakuwa kichocheo kikubwa katika uchumi wetu hasa ikijikita katika ujenzi wa miundombinu, viwanda na kadhalika, nchi yetu itanufaika sana kutokana na mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado ni maoni ya Kamati yangu kwamba katika siku za hivi karibuni Serikali italeta Muswada ambao sasa utaweka misingi katika sekta nzima ya hifadhi ya jamii. Mamlaka itakayoundwa itakuwa na kazi moja kubwa ya kufanya utafiti wa kina wenye lengo la kufanya mageuzi katika sekta hii ili Muswada utakaolewa na Serikali uzungumzie kwa upana zaidi sekta ya hifadhi ya jamii nchini kuweko mifuko mingi ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojadiliwa na Kamati yangu ni kuwepo kwa mifuko mingi ya hifadhi ya jamii chini ya utaratibu wa Wizara tofauti. Wadau walidhani kwamba ingekuwa ni jambo la msingi kabisa kama Muswada huu ungezingatia kuondoa tatizo hili na ungetamka bayana kuwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kuwa ndiyo wenye jukumu juu ya maendeleo ya mifugo yote ya hifadhi ya jamii badala ya kuwa chini ya Wizara tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili suala hili kwa kina, Kamati yangu ilibaini kwamba Muswada huu unaopendekezwa umefuata tamko Na. 15 la Sera ya Hifadhi ya Jamii ambayo inatambua kuwepo kwa mifuko mingi ya hifadhi ya jamii. Hata hivyo, Kamati bado itaendelea kulifanyia utafiti wa kina suala hili ikiwa ni pamoja na kuingia kwa undani zaidi kujadili sera ya hifadhi ya jamii kubaini upungufu na hatimaye kutoa mapendekezo ya kuiboresha sera kwanza kabla ya kutoa ushauri kuhusu kuwepo kwa mifuko mingi ya hifadhi ya jamii nchini au hapana.

Katika vikao vyote vya Kamati wakati wa kujadili Muswada huu wadau walionyesha wasiwasi kwamba tatizo la uhamishaji wa mafao ya wafanyakazi toka mifuko mmoja kwenda mifuko mwingine bado halijapatiwa ufumbuzi hasa ukizingatia changamoto kubwa iliyopo kuhusu kuundwa kwa jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo hapo baadaye wafanyakazi wataruhusiwa kwenda kufanya kazi katika eneo lolote la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili kwa kina Kamati ilibaini kwamba suala la kuhamisha mafao toka mfuko mmoja kwenda mfuko mwingine pale ambapo mwanachama anapohama kutoka kazi moja kwenda nyingine bado sio suala jema. Kwani kitendo cha kuchangia fedha katika mifuko ni kwa ajili ya mwanachama na wengine ambao wako katika kupata mafao. Kitendo cha kuhama na kuhamisha fedha bado hakifai, hasa ukizingatia kwamba idadi ya wanachama katika mifuko yetu bado ni ndogo yaani chini ya asilimia sita ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhamisha mafao kutoka mfuko mmoja kwenda mfuko mwingine halina faida kwa mwanachama wala kwa mfuko kuhamisha fedha, bado litaathiri mfuko na mwanachama mwenyewe atawezu kupata kile alichokitarajia mpaka pale sheria na taratibu za mifuko yote itakapoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati yangu ilipendekeza kwamba pale mwanachama anapohama basi ahamishe mafao yake na kuwe na utaratibu kati ya mfuko na mfuko ili mwanachama aweze kupata mafao yake katika mfuko alikohamia na sio kuhamisha fedha. Katika Muswada kifungu cha 52(2)(h) kimetamka wazi kuwa uhamishaji wa mafao utashughulikiwa katika kanuni, hivyo kanuni zitakapoandaliwa ziwe na lengo la kuboresha mazingira hayo kuboresha mafao ya mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilichukua muda mwingi kujadili lilikuwa ni suala la namna gani Muswada utawezu kuboresha mafao ya mwanachama badala ya kuzingatia zaidi katika kudhibiti fedha za mfuko. Sera ya sekta ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 inayo malengo mazuri ya kupanua huduma hii. Katika kuboresha mafao kwa mwanachama baadhi ya wadau walibaini kwamba lazima kuwepo na mikakati na taratibu za mwanachama kunufaika na mafao kabla ya kufikia kustaafuli. Mfano kupata sehemu ya mafao yake kabla ili aweze kuwekeza au kujenga nyumba kabla ya kustaafuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili suala hili Kamati ilibani kwamba mwanachama kupata sehemu ya mafao yake kabla ya kustaafuli linaondoa maana halisi ya hifadhi ya jamii. Hifadhi ya jamii ni kumkinga mwanachama baada ya kustaafuli ikiwa ni pamoja na mafao mengine kama yanavyotolewa na mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipendekeza kwamba katika kuboresha mafao lazima mipango mingine iandaliwe katika kumjenga mwanachama kabla ya kustaafuli. Mfano mifuko yenye inaweza kuanzisha programu inayojitegemea katika kumkopeshwa mwanachama kwa kutengewa asilimia 20 kwenye fedha za mfuko kuendesha zoezi la mikopo ya nyumba kama nchi nyingine zinavyofanya. Lazima mifuko itafute namna ya kumsaidia mwanachama kwa sasa kabla ya kustaafuli. Ni maoni ya Kamati kuwa kumkopeshwa fedha mwanachama kutoka katika mafao yake bado si jambo zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sote tunajua kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii inajenga majengo mengi yenye thamani, hii ni mojawapo ya njia katika kuboresha mafao ya mwanachama. Ukweli uliopo ni kwamba fedha zinazokatwa katika michango kwa

mwanachama haziwezi kuboresha mafao hivyo kuwekeza katika vitega uchumi ni muhimu sana. Ni maoni ya Kamati kwamba mifuko iangalie namna mwanachama mmoja mmoja atakavyopata mafao kulingana na hali halisi ili mafao hayo yaweze kukidhi mahitaji ya kila siku. Lazima tuangalie thamani ya shilingi wakati huo kanuni za mafao lazima zizingatie hilo, mfanyakazi aliyestaafu ni muhimu apate kiwango cha fedha kulingana na halisi ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kodi linaathiri sana mafao ya mfanyakazi na linaludisha nyuma juhudi za kuboresha mafao. Kamati inashauri kwamba suala la kodi liwekewe katika kanuni zitakazoangaliwa na Waziri ili kubainisha namna ya kuleta unafuu katika mafao ya mwanachama. Hata hivyo, ni imani ya Kamati kwamba suala la uboreshaji wa mafao ya wafanyakazi limezingatiwa sana katika vifungu vya 31, 34, 35, 36 na 37 vya Muswada huu. Kamati inaunga mkono kuwekwa kwa vifungu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wadau mbalimbali kushirikishwa katika mchakato wa kuandaa Muswada huu lilijitokeza kwa kiwango kikubwa tulivyokutana Dar es Salaam. Baadhi ya wadau walieleza kwamba hawakushirikishwa katika mchakato huo hasa *LESCO* ambacho ni chombo kilichoundwa kisheria kwa ajili kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana masuala yote yanayohusu kazi, uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili suala la ushirikishwaji katika mchakato wa kuchambua Muswada, Kamati ilibaini kwamba wadau muhimu walishirikishwa kikamilifu katika mchakato wa maandalizi ya Muswada katika hatua za kukusanya maoni yaliyotumika kuuandaa. Wadau mbalimbali walishirikishwa hadi katika ngazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu, hata hivyo, sote tunajua baada ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri taratibu zinazojulikana ni lazima zizingatiwe. Katika hatua hii haiwezekani kuwashirikisha wadau kwani ni kazi Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ielewewe kwamba baada ya rasimu ya Muswada kukamilika katika hatua ya Baraza la Mawaziri kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuandika Muswada, uandishi wa Muswada unapokamilika hupelekwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na hatimaye kuletwa Bungeni kusomwa mara ya kwanza. Hatua ya kusomwa mara ya kwanza Bungeni inatoa fursa kwa wadau wote kujadili kwa lengo la kuboresha Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mazungumzo kuhusu suala hili Kamati ilibaini kwamba wadau walidhani wangeshirikishwa pia katika hatua za kuandika Muswada au baada ya kukamilika kwa kazi ya kuandika Muswada kabla ya kusomwa mara ya kwanza. Ni maoni ya Kamati kwamba ni muhimu kufuata taratibu zilizowekwa katika kutunga sheria. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali na Bunge ili wadau wawewe kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kutunga sheria muda wa kutosha utolewe wa kujadili na kuchambua Muswada. Wadau wahuishwe kikamilifu kupitia katika Kamati husika, utaratibu wa kutenga siku moja au mbili kujadili Muswada na wadau umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Benki Kuu na Sekta ya Hifadhi ya Jamii, wadau walionyesha wasiwasi kwamba Muswada unaopendekezwa umejengwa kuwepo kwa wadhibiti wawili yaani mamlaka ya udhibiti itakayoundwa na Benki Kuu. Hii ilionekana wazi kwamba italeta hali ya migongano katika utekelezaji wa majukumu, hivyo ingekuwa ni busara kuwe na mdhibiti mmoja au mamlaka. Benki Kuu iwe mshauri kwa mamlaka na kutoa miongozo na masuala ya fedha na uwekezaji kupitia mamlaka ili kuondoa migongano ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kutoka Serikalini ilielezwa kwamba mshauri mkuu wa Serikali katika mambo ya fedha na uwekezaji ikiwa ni pamoja na fedha za sekta hifadhi ya jamii ni za Benki Kuu. Hivyo hakuna suala la migongano katika utekelezaji, Benki Kuu itakuwa inafanya kazi yake kama mshauri mkuu wa Serikali katika masuala ya fedha na uwekezaji kwa kutoa miongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 26 mpaka 27 vinaelezea kwa uwazi kabisa uhusiano kati ya mamlaka ya Benki Kuu. Hivyo katika kufafanua ilielezwa kwamba suala la kudhibiti ni sehemu ya uboreshaji wa mafao ya wachangiaji kwa mujibu wa tamko la sera ya 12,13 na 14 na hii imezingatiwa katika vifungu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ndiyo iliyoweka dhamana ya fedha za wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii endapo mambo yakienda vibaya mafao ya mwanachama yasipotee. Hivyo Benki Kuu ni muhimu kutupitia macho katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mjadala mrefu Kamati iliona si muhimu sana Benki Kuu kwenda moja kwa moja katika mifuko ila inaweza kutoa miongozo ya uwekezaji na fedha kwa mamlaka ili iweze kufuutilia utekelezaji. Suala la kuweka vyombo viwili kusimamia mifuko litaleta matatizo sana katika utekelezaji. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwamba Benki Kuu majukumu yake yataishia katika mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilijadiliwa kwa kina ni kuhusu uandikishaji wa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ya lazima. Wadau wengi walionyesha wasiwasi kwamba kitendo cha kuandikishwa upya mifuko ya hifadhi ya jamii kinatoa nafasi ya migongano. Hivyo Miswada ni muhimu iweke wazi uandikishwaji wa mifuko wa jamii na ule wa hiari ili kuwezesha sheria kuwa wazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wadau walionyesha wasiwasi kwamba suala la uandikishwaji wa mifuko na mawakala lina upungufu kwa sababu hairuhusu mwanachama kupewa nafasi ya kuondoka na kuijunga na mifuko mingine baada ya kujiandikisha hata kama akibaini kwamba kuna upungufu katika utendaji kazi wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29 kinachomtaka kila mwajiri kuandikisha wafanyakazi wake katika mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima kilijadiliwa kwa kina na

Kamati yangu. Kifungu hiki kinatamka wazi kwamba mfanyakazi ana uhuru wa kuchagua mfuko anaoutaka. Katika hili wadau wengi walibaini kwamba litaleta matatizo, kifungu kingewahusu tu wanachama wapya lakini kwa wanachama ambao wako tayari kwenye mifuko waendelee kuwepo katika mifuko hiyo bila kuandikishwa upya au kuchagua mifuko. Wanachama wa sasa wa mifuko wasiruhusiwe kubadilisha uachama badala yake uchaguzi wa mifuko kujiunga ufanyike pale tu mwanachama mpya anapojiunga kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili Kamati inaona si vyema wanachama walioko katika mifuko ya lazima kujiandikisha upya au kuwaambia kuchagua mfuko wanaoutaka. Ni muhimu kifungu hicho kingesitiza kwamba mwanachama anawenza kuwa huru kujiunga katika mifuko ya hiari. Kamati inashauri kwamba kifungu hicho kibadilishwe na kanuni zitakazoandaliiwa lazima ziweke utaratibu wa wazi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojadiliwa kwa kina na Kamati ni pamoa na mamlaka na majukumu ya utendaji mkuu wa mamlaka ya udhibiti itakayoanzishwa. Wadau walionyesha wasiwasi kwamba mamlaka na majukumu yanayopendekezwa kwa mtendaji mkuu ni makubwa sana. Mfano mtendaji mkuu atakuwa na uwezo wa kufuta mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima ambayo imeundwa kwa mujibu wa sheria za Bunge. Hivyo mtendaji mkuu wa mamlaka amepewa uwezo mkubwa zaidi kuliko hata bodi yenewe, aidha, akiteuliwa lazima amalize miaka mitano. Mapendekezo yaliyopo katika Muswada yanamzuia kuondolewa hata na Rais aliyemteua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili kwa kina Kamati ilibaini kwamba kifungu 11(2) hakuna sababu ya kuweka vikwazo vyenye nia ya kumlinda Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka. Hakuna sababu yoyote Muswada kuweka vifungu kwamba Mkurugenzi Mkuu atakaa kwa muda wa miaka mitano na ikilazimika atakaa tena miaka mitano. Kamati inashauri kwamba Mkurugenzi Mkuu asiwekewe muda wa kukaa ili aliyemteua awe na uwezo wa kumwondoakionainafaa. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya mamlaka itakayoundwa yalijadiliwa kwa kina na Kamati yangu. Baada ya kujadili Kamati ilibaini kwamba majukumu ya mamlaka yawe wazi ili kuondoa migongano, mfano, katika kifungu cha 5(k) mamlaka imepewa jukumu la kuteua pale ambapo itaona mambo hayaendi vizuri. Kifungu hiki kingewekwa katika mifuko ya watu binafsi itakayoanzishwa kwa sababu haitakuwa busara kufuta uongozi wa mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima ambapo Mkurugenzi Mkuu na Mwenyekiti wa Bodi huteuliwa na Rais. Baada ya kujadili Kamati inashauri kwamba katika kazi ya majukumu ya mamlaka kiongozwe kifungu cha 5(1) cha elimu kwa umma ili kuelimisha watu kwa lengo la kuongeza wanachama na kuboresha mafao ya mwanachama. Vilevile Kamati inashauri kwamba kifungu 6(2) kingeondolewa hapo kilipo na kuhamishiwa katika kifungu cha 9 na kuwa kifungu cha 9(f) ili kutoa uzito wa kazi ya Bodi badala ya kuweka chini ya majukumu ya mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kufutwa na kuandishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii limezungumzwa sana na wadau na wajumbe wa Kamati. Wadau walibaini kwamba kimsingi hakuna sababu ya kufutwa na kuandikisha tena mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima ambayo tayari ipo kwa mujibu wa sheria za Bunge. Kujiandikisha kutumike kwa mifuko ya watu binafsi inayotarajiwa kuanzishwa. Mfano nchi ya Kenya walipoanzisha mamlaka ilitambua moja kwa moja mifuko iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufafanua Waziri aliwaelezea wajumbe kwamba sehemu ya tatu ya Muswada imeweka taratibu za uandikishaji na usajili wa mfuko, mameneja na wasimamizi ili kuona shughuli za uendeshaji wa hifadhi zinaendeshwa kwa kufuata taratibu. Hivyo lazima kuwe na maombi na baada ya kuandikishwa lazima kila mfuko upate cheti kuwezesha kuanza kufanya kazi. Aidha, ni kawaida katika kuanzisha mifuko ni lazima kuwe na masharti yaweze kufuatwa kabla ya kuanzisha kufanya kazi iliyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uandikishaji mamlaka litaweka viwango vinavyostahili kufuatwa. Kifungu cha 14 kinasisitiza kwamba hata mifuko iliyopo lazima ijisajili ili iweze kuendesha shughuli zake. Taratibu za uandikishaji zitawekwa kwenye kanuni zitakazoandalika na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Kamati ilikubaliana na Serikali na kuishauri kwamba katika kanuni lazima mambo muhimu ya kujiandikisha yawekwe wazi ili kuzuia migongano hasa katika mifuko iliyopo. Mwanachama aruhusiwe kujiandikisha mfuko anaotaka lakini baada ya kuandikishwa iwe hakuna kuhama mfuko ili kuimarisha mafao yake. Kifungu cha 30 cha Muswada kinaruhusu mifuko mingine ya watu binafsi kuanzishwa, hivyo basi ni bora kuzingatiwa kifungu hiki ili wale wenye uwezo wa kuchangia waweze kujiunga katika mifuko hiyo mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wajumbe wa bodi ya mamlaka lilijadiliwa kwa kina. Muswada unaopendekezwa ulikuwa unaonyesha kuwa kuna wajumbe wengi wa bodi wengi wao wanaotoka Serikalini, kuna Makatibu Wakuu watano, Gavana wa Benki Kuu, Naibu Mwanasheria Mkuu. Jumla wajumbe 14, hii ni idadi kubwa sana na itakuwa ni gharama kubwa katika kuihudumia bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadiliana Kamati ilipendekeza idadi ya wajumbe wa bodi kupunguzwa angalau ifikie 9. Lengo la idadi hii kuwa 9 ni katika kutekeleza suala la utatu yaani wawepo wajumbe kutoka Serikali, Vyama vyta Wafanyakazi na Umoja wa Waajiri Tanzania. Aidha, kuwepo kwa wataalamu wa masuala ya hifadhi ya jamii ni muhimu. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya majukumu ya bodi zlijadiliwa na Kamati yangu na kubaini kwamba kazi na majukumu yaliyopendekezwa katika Muswada huu ni mepesi na hayana uzito wa bodi kama hii. Hivyo Kamati ilishauri kwamba kazi zinazohusu sera na maamuzi ya mamlaka lazima zipate kibali cha bodi badala ya kuachiwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka. Katika hili Serikali ilikubalana na ushauri wa Kamati. Hivyo vifungu mbalimbali vinavyohusiana na hili vilirekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la baadhi ya maneno kutopata tafsiri sahihi lilijadiliwa, wadau walibaini kwamba katika maana ya maneno yaliyotumika katika Muswada huu kifungu 3, maana ya neno Waziri haionyeshi kuwa ni Waziri gani anayehusika na masuala ya wafanyakazi au anayehusika na masuala ya hifadhi ya jamii kwa sababu mifuko mingine ya hifadhi ya jamii ipo chini ya Wizara zingine. Hii italeta mgongano mkubwa hasa pale Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka anapohitaji kushauriana na Waziri ataenda kwa Waziri yupi kwa sababu kila Mfuko uko chini ya Wizara tofauti. Tafsiri sahihi ya neno Waziri isipoeleweka vizuri Mamlaka itakapoanzishwa itashindwa kuelewa iwjajibike kwa nani. Kamati ilishauri kwamba tafsiri ya neno Waziri lazima iwekwe wazi, kwamba Waziri ni yule anayehusika na masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na matumizi ya neno *may*. Katika baadhi ya vifungu Kamati ilibaini kwamba neno *may* linapunguza uzito wake hivyo neno *shall* linatakiwa litumike ipasavyo pale panapohitajika. Aidha, Kamati ilibaini kwamba kuna maneno yamewekwa katika tafsiri lakini hayajatumika mahali popote katika Muswada huu, hivyo hakuna sababu yoyote ya kuyaweka katika tafsiri. Kwa mfano, maneno *contribution, credits*, hayatumika kabisa katika Muswada hivyo hakuna haja ya kuonekana katika tafsiri. Maneno hayo yaondolewe. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuandika upya tafsiri ya maneno hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau walibaini kwamba katika kifungu 27(2) kuna sababu ya kurekebisha muda wa kufanya kazi ya ukaguzi wa mahesabu na kuwasilisha taarifa katika mamlaka husika. Baada ya kujadili Kamati ilishauri kwamba upo umuhimu wa kuongeza muda kutoka miezi 3 hadi 6 ili Mifuko iweze kuwa na muda wa kuwasilisha taarifa. Aidha, katika kifungu 27(2) (a),(b),(c),(d) badala ya kuandika maneno yote hayo basi iandikwe *financial statements*. Serikali ilikubaliana na Kamati kuhusiana na ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 38(1) Kamati pia ilibaini kwamba kufanyika kwa ukaguzi mara mbili kwa mwaka ni gharama kubwa na ni usumbufu wa muda. Kamati ilipendekeza kwamba ukaguzi katika mifuko unaweza kufanywa mara moja kwa mwaka pamoja na kwamba masuala ya fedha na uwekezaji ni nyeti. Kamati bado inaishauri Serikali kuliangalia suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nani apewe adhabu kama itatokea ukiukwaji wa taratibu za uandikishaji wa wanachama lilijadiliwa, kifungu 28(2)(3) kinahusika na uzuiaji wa baadhi ya mwenendo hasa kutokana na usajili wa wafanyakazi kufanywa baada ya uthibitisho wa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili suala hili na ilibaini kwamba itakuwa si rahisi kumshitaki mdhamini, meneja au msimamizi wa mfuko kwa kosa la kumsajili mfanyakazi ambaye atakuwa ni mwanachama wa mfuko mwingine. Kutokana na hiyo Kamati ilipendekeza kwamba mfanyakazi mwenyewe ahusike na mwenendo huo usiofaa. Kumpa adhabu Mwajiri Mkuu kwa kosa lililofanywa na mtumishi wake wa chini si

jambo sahihi, ni bora adhabu iende moja kwa moja kwa mkosaji. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho katika vifungu vinavyohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 28(2) kuhusu adhabu iliyopendekezwa ya shilingi milioni 5 baadhi ya wadau walibaini kwamba adhabu hiyo ni ndogo sana hasa kama tunataka kukomesha tabia ya watumishi wasiokuwa waaminifu. Hata hivyo, suala hili lilizua mjadala pale wadau walipokuwa wanalinganisha na sheria zingine, mfano sheria ya Manunuzi, adhabu ya mvunja sheria ni shilingi laki tano, kwa nini sheria hii isingeweka angalau kiwango kinacholingana na hicho? Hata hivyo, baada ya kujadili Kamati ilipendekeza kwamba kiwango cha adhabu cha shilingi milioni 5 ni kidogo na kupendekeza kwamba kiwango cha shilingi milioni 10 ndicho kitakachofaa. Serikali ilikubaliana na kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mfuko wa Bima ya Taifa kulinganishwa na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii lilijadiliwa na Kamati yangu, wadau walibaini kwamba lazima Mfuko wa Bima ya Taifa uwekewe masharti ya kipekee badala ya kuhusishwa moja kwa moja na Mamlaka ya Kudhibiti itakayoundwa kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Baada ya Kamati kujadili suala hili iliishauri Serikali kwamba Mfuko wa Bima ya Taifa usifananishwe na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri kwamba masuala ya utawala pekee ndiyo yahusishwe katika Mfumo huu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii lakini yale mambo ambayo ni ya kitaaluma (*technical*), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ihusike, ushauri huu ulikubaliwa na Serikali na vifungu kadhaa kuongezwa ili kuleta maana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa Shukrani. Kwanza, nachukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Profesa Juma Athman Kapuya, (Mb.), Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, (Mb.) na Katibu Mkuu wake, Dr. S. Komba, kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati Kamati hii ikifikiria Muswada wa Sheria hii.

Aidha, nawapongeza wataalamu wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha kazi hii. Pia napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa wadau wote walioshiriki katika mchakato huu, wadau walioshiriki ni pamoa na Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), Umoja wa Waajiri Tanzania (*ATE*), Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF, PPF, LAPF, PSPF, NHIF* na *GEPF*), wataalamu na wasomi wa masuala ya hifadhi ya jamii na Kamati iliyoandaa muswada huu. Ushiriki wao katika kuchambua Muswada kwa kiasi kikubwa umeiwezesha Kamati kutumia maoni na ushauri katika vikao vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, (Mb.), kwa kuendesha vikao vya Kamati kwa ufanisi mkubwa hasa katika kujadili muswada huu. Aidha, napenda kumshukuru Ndugu

Lawrence Robert Makigi, na Ndugu Brown Mwangoka, Makatibu wa Kamati hii, kwa kuihudumia Kamati kwa makini na ufanisi ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maandalizi ya Maoni haya.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima sasa naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii walioshiriki kuchambua muswada wa sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008 kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Mheshimiwa Salum A. Khalfani, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Dr. Gertrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, na Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Mheshimiwa Spika, wewe binafsi, Wenyeviti wa Bunge na Kaimu Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wenu mnaotupa katika kutekeleza shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naunga mkono hoja. (*Makofit*)

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA HIFADHI YA JAMII:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuwa hapa ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwako kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008 (*The Social Security Regulatory Authority Bill, 2008*) kwa mujibu Kanuni ya 53(6)(c) na 86(6), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa salamu za pole kwa wale wote walioguswa kwa njia moja ama nyininge na maafa yaliyotokea kwenye migodi ya machimbo ya *Tanzanite*, Mererani. Naomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira kwani mambo yote ye ye ndiye mtoaji na mtwaaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua nia ya Serikali kutaka kuunda mamlaka ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia hifadhi ya jamii, kwani kulikuwepo na malalamiko mengi toka kwa wanachama jinsi hifadhi hizo zinavyofanya kazi zake au zinavyowekeza akiba za wanachama wao. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani ina matatizo makubwa na maeneo kadhaa ya Muswada huu kama tutakavyoeleza hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kambi ya Upinzani ilitarajia Muswada huu ungeleta msawazisho baina ya mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii. Badala yake kuna mkanganyiko mkubwa baina ya mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii ya umma (*public*

*schemes) kama vile NSSF, PPF na kadhalika na ile ambayo itaanzishwa na waajiri (private schemes).*

Muswada huu haukutenganishwa baina ya *public* na *private schemes*, kutokana na upungufu huo inasababisha hata baadhi ya vifungu kukinzana na sheria za uajiri zilizopo. Kifungu cha 39(1), mamlaka inapewa madaraka ya kutengua ajira ya watendaji wakuu wa mifuko ya umma wakati watendaji hao ni wateule wa Mheshimiwa Rais. Tunavyoolewa sisi kuwa chombo kinachofanya uteuzi ndicho chenye mamlaka ya kutengua uteuzi huo na si vinginevyo. Utata huu usipowekwa sawa sheria hii haitatekelezeka au itazalisha mtafuruku kati ya mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 3 kinachohusu tafsiri ya maneno, Muswada umetumia neno “*Minister*“ means the Minister responsible for social security. Kwa kuwa hifadhi ya jamii kwa mfumo wetu wa Tanzania imegawanyika takriban katika Wizara nne, hivyo basi Kambi ya Upinzani inataka ufanuzi kuhusu ni nani Waziri mwenye dhamana ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(c) kinacho sema, nanukuu: “*the board shall:- receive any grants, gifts, donations or endowments on behalf of the authority....*“ hapa neno *gifts* linaweza kupenyezwa hata kusababisha kuvunjwa kwa maadili ya utawala bora. Aidha, mgongano wa kimaslahi kwa baadhi ya watendaji vilevile unawenza kuleta upendeleo wa maamuzi kwa baadhi ya hifadhi toka kwa mamlaka ya udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20 kinaipatia mamlaka uwezo wa kufuta usajili wa mfuko wa hifadhi iwapo baadhi ya mambo yaliyoanishwa katika kifungu hicho yatatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo usajili wa mfuko utakuwa umefutwa, ina maana mfuko husika hautakuwepo tena kwa mujibu wa sheria. Lakini mifuko ya Umma kama vile *NSSF, PPF, LAPF, PSPF* na kadhalika imeanzishwa kwa sheria za Bunge, hivyo kama mamlaka itakuwa na uwezo wa kufuta mifuko hiyo maana yake ni kuwa hata sheria za Bunge za uanzishwaji wa mifuko hiyo itakuwa imevunjwa. Jambo hili ni kinyume cha utaratibu wa sheria ambapo kilichoanzishwa kwa sheria ya Bunge hufutwa tu kwa marekebisho ya sheria, kinyume na hapo ni kuvunja kabisa utawala wa sheria.

Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atupe ufanuzi juu ya hili kama kweli mamlaka ya udhibiti inayoundwa itaweza kuchukua kazi ya Bunge ya kutunga au kufuta Sheria, vinginevyo Kambi ya Upinzani inawashawishi Waheshimiwa Wabunge waikatae Sheria hii mpaka itakapokuwa imeiva na haipingani na Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 23(5) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 25(1), Kambi ya Upinzani inaona kuwa hapa kuna mkinzano wa dhahiri kuhusiana na vifungu tajwa hapo juu. Tunaitaka Serikali iweke wazi ni kifungu kipi kitatumika kati ya hivyo hapo juu. Kifungu cha 29 kinachozungumzia wigo wa uanachama kinasema kuwa: “kila mwajiri katika sekta rasmi ya ajira anaweza kujiunga na mfuko wowote

ambao umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria". Kwa kweli hili linatakiwa kuangaliwa kwa kina kwani kuna Sheria ambazo zipo zinazoelekeza kuwa kila mwajiri anatakiwa kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake wajunge na mfuko fulani wa hifadhi vinginevyo itapelekeea mtafaruku wa wanachana kuhama kutoka mfuko mmoja kwenda mwingine jambo ambalo litasababisha utendaji kazi wa mifuko hiyo kuwa mgumu sana pamoja na wanachama kukosa mafao yao kwani mafao hayahamishiki kama ambavyo wanachama watakavyohama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa hali hii ni matukio yaliyotokea ndani ya Bunge ambapo kampeni ya kuvutia wanachama kati ya *PPF* na *NSSF* ilianzia hapa hapa ndani ya Bunge na kwa bahati mbaya wasimamizi wa Semina akiwemo Mheshimiwa Waziri hawakuweza kuidhibiti hali hiyo. Kama hali hiyo imeanza ndani ya Bunge, je, nini kitatokea huko nje kama si vurugu badala ya malengo tarajiwa ya Sheria hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 38(1) kinachohusu ukaguzi limetumika neno *may* katika mstari wa kwanza wa sentensi. Kambi ya Upinzani inaona neno hilo haliipi ulazima wa kutosha Mamlaka kufanya ukaguzi, hivyo basi tunashauri litumike neno *shall* litakaloipa Mamlaka ulazima wa kufanya ukaguzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 41 kinachohusu uanzishwaji wa Baraza la Rufaa ya Hifadhi ya Jamii litakalokuwa na Mamlaka ya kusikiliza rufaa zote dhidi ya maamuzi ya Mamlaka, Kambi ya Upinzani inaona hapa itakuwa ni kuongeza Mamlaka nyingine ambayo si ya lazima. Tunashauri Mahakama ya Kazi iimarishe kwa nyanja zote, watendaji na vitendea kazi na ifanyiwe marekebisho yanayostahili ili iweze kufanya kazi ambazo zingefanywa na Baraza la Rufaa. Uhushishwaji huo utaokoa fedha nyingi za walipa kodi, isitoshe kwa mtindo huu kila jambo litahitaji kuundiwa Mahakama yake ya Rufaa wakati hata zilizopo zinashindwa kufanya kazi kutokana na ufinyu wa bajeti, vitendea kazi na rasilimali watu. Pendekeso hili ni dhahiri halikufanyiwa utafiti wa kina wa hali halisi katika Mahakama nyingine za aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 46 (b)(c) cha Muswada juu ya majukumu na nguvu za Benki Kuu kinaonyesha kuwa kutakuwa na wadhibiti wawili yaani Mamlaka ya Udhhibit na Benki Kuu ambavyo vinapewa madaraka kamili kuhusu mambo yote ya fedha ya mifuko ya hifadhi ya jamii. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kwa kuweka wadhibiti wawili ni kuweka mianya kwa watendaji kutowajibika. Wajibu wa Benki Kuu uishie katika miongozo ya uwekezaji tu kama kifungu cha 46(a) kinavyoeleza na usimamizi wa miongozo hiyo uwe ni jukumu la Mamlaka ya udhibiti. Dhana hii haizingatii mabadiliko yanayotokea ndani ya Benki Kuu sasa baada ya kupata uzoefu wa matukio makubwa kama *EPA* ambapo Benki Kuu inajiondoa kwenye shughuli zote ambazo kimsingi si shughuli za Benki Kuu (*core activities*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sera ya Hifadhi ya Jamii iko wazi na wataalamu wamejaribu kuieleza na kutoa upungufu uliomo kwenye mifumo ya hifadhi za jamii hapa nchini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuboresha Muswada huu kabla ya kuitishwa na kuwa Sheria kwani ni dhahiri hata semina iliyoendeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge haikuzingatia kabisa upungufu na badala yake ikajikita zaidi

katika manufaa ya Mamlaka hii mpya. Jambo hili ni hatari sana lisipozingatiwa kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikitaka kupitisha inaweza ikaendelea lakini itabaki katika kumbukumbu ya *Hansard* kuwa tuliwaeleza upungufu mkubwa na kwamba Muswada huu haujafanyiwa kazi vya kutosha na haujaiva.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ninayo orodha fupi sana ya wachangiaji, tena wako sita tu, kwa hiyo, yupo Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Felister A. Bura na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami. Kwa hiyo, ninamwita Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa ili aanze.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niseme machache katika Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mimi kwa kutoa pole nyngi sana kwa maafa mbalimbali yaliyowapata watu katika kipindi hiki kilichopita. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzetu wapya wawili waliojiunga nasi na niwatakie heri katika kazi zao muhimu sana za Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pole maalumu kwa wananchi wa Kisiwa cha Pemba kwa sasa kutokana na balaa jipya linalowakumba la ujambazi wa kutumia silaha. Hali hii kwa watu wa kule ni ngeni na hawakuizoea na ningeomba sana kuchukua fursa hii kuiomba Serikali na Wizara zinazohusika ziwawezeshe Watendaji ili watu angalau waishi kwa amani na utulivu. Baada ya kusema hayo sasa nije kwenye hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhana nzima ya chombo hiki kinachotaka kuundwa kudhibiti vyombo hivi vya mifuko ya hifadhi ya jamii. Si vibaya, lakini tatizo linajitokeza wakati wa utekelezaji. Uzoefu unaonyesha kwamba vyombo vingi vinavyoundwa wakati wa kutekeleza majukumu yake hutokea migongano na ndiyo sababu na sisi tukaanza kutahadharisha kabisa hapa, pamoja na nia nzuri labda iliyopo Serikalini lakini utekelezaji unawenza ukakwamisha. Mimi labda nitoe mifano midogo tu.

Sasa hivi inaeleza wazi kuwa Mifuko ya Hifadhi ya jamii, Wizara au Wafanyakazi mbalimbali wapelekewe mafao yao pale, lakini hali halisi inaonyesha kuwa waajiri wengi hawapeleki hizo fedha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na matokeo yake watu wanapostaafu inakuwa ni vita kubwa baina ya mifuko husika na wale waliokuwa waajiriwa kwani wao wanataka mafao yao lakini kumbe hayakupelekwa, sasa utekelezaji ndiyo usumbufu uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa inaelelezwa kuwa hiki chombo kinachotaka kuundwa ambacho mimi naona kazi zake kubwa ukiziangalia zinafanana fanana na hii bodi iliyopo sasa hivi, kwa kweli mimi naona sijui Serikali imefikiri vizuri katika kuleta

chombo hiki kwa wakati huu kwa sababu unaposema kuwa chombo hiki kitapaswa kuwa labda kumdhibiti kwa namna fulani Mkurugenzi, Mkurugenzi ni mteuliwa na Rais. Sasa ni vizuri basi Mamlaka hiyo inayomteua ikawa pia na majukumu ya moja kwa moja katika kumshughulikia. Siyo kuwa unampangia *time* afanye kazi kwa kipindi fulani, inawezekana Mheshimiwa aliyemteua anaona baada ya kumteua muda mdogo tu hafai anataka kumwondoa au anaona anafaa kwa muda mrefu anataka aendelee. Sasa nafikiri hilo lingangaliwa kwa upana wake pia.

Jambo lingine ambalo nilipenda niliseme ni hiki chombo cha rufaa. Sijui hii rufaa inakusudiwa nini hapa na ni nani wanaokata rufaa kwa sababu inawezekana ndani ya chombo chenyewe watendaji wanaofanya kazi ndani ya chombo wana malalamiko yao, watakata rufaa kwenye chombo hicho au watu ambao wamewekeza katika mifuko hii watakata rufaa kwenye chombo hicho? Na hiyo rufaa yenyewe au hicho chombo kitakuwa na mamlaka gani hasa? Ni nini hasa uwezo wa chombo hicho labda na mahakama ambazo sasa hivi zipo? Ni vizuri labda na mambo hayo yakaweza kuelezwa.

Lakini labda na sasa niseme kidogo kuhusu mifuko ule wa Bima ya Afya. Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inaundiwa chombo, hivi huu mifuko wa Bima ya Afya ambao ukiutazama majukumu yake yanafanana fanana kidogo na mifuko hii ya hifadhi ya jamii je, na wao wataingia katika chombo hiki au kama mifuko huu hauingii ni lini basi Serikali nayo inafikiria kuiundia chombo? Kwa sababu hapa napo pana uwezekano wa kutumika vibaya mafao haya kwa sababu sote tunajua ni binadamu na binadamu wanapofanya kazi zao mara nyingi wanatawaliwa na huo ubinadamu.

Sasa tungeomba sana mambo haya yaangaliwe ili ile dhana ya msingi ya kuleta uboreshaji ipatikane isije ikawa ni mgongano wa madaraka kwamba chombo hiki kinataka kushindana na bodi iliyopo, kinataka kukomoa baadhi ya watu. Hilo nafikiri halitatuifikisha mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikutaka kupoteza muda wako mwangi nilitaka nilitanabahishe hilo ili Serikali katika lengo lake la kufanikisha utendaji kazi wa mifuko hii iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita msemaji anayefuata, Mheshimiwa Athuman S. Janguo.

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie machache katika muswada huu.

Nianze kwa kusema kwamba nauunga mkono moja kwa moja, kinyume na vile ambavyo tumeambiwa na Kambi ya Upinzani kwamba ucheleweshwe, kwa kuwa tayari kuna upungufu ambao umekwishaonekana ukishauchelewesha ina maana ni kwamba yale makosa yaendelee na wafanyakazi waendelee kukosa yale mafao yao kama msemaji aliyekaa alivyosema. Kwa hiyo, nasema ni vizuri muswada huu tukaupitisha ili kusudi

yarekebishwe yaliyokuwapo na yale mengine ambayo hayajatimia yatakuwa yanarekebishwa kila tunavyokwenda na kuyatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo niseme tu kwamba mengi yameonyesha upungufu ambao umekwishatajwa hata katika semina ile iliyopita. Sasa ni vizuri kuwa na Sheria hii ambayo inaunda Mamlaka ambayo itasimamia ili kusudi upungufu huo uondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niende moja kwa moja kwenye Muswada. Ninapenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba katika kifungu cha 6(1)(b) pale pamesemwa kwamba mamlaka itakuwa inakasimu madaraka yake kwa mtu yeoyote. Mimi nafikiri ni wazi mno siyo kwa mtu yeoyote hata kwa Katibu Kata, ni vizuri yangewekwa maneno kama vile walivyofanya katika Ibara ya 10 walipokuwa wanazungumza kukasimu madaraka kwa Kamati kwa kusema: '*The Authority shall delegate to any person within its establishment*'. Hapo ina maana kwamba wanakasimu madaraka ndani ya mamlaka.

Katika kifungu cha 7(1) nashukuru kwamba kimerekebishwa, bodi ilikuwa kubwa sana na ilikuwa imeweka watu wazito yaani watu ambao walikuwa wana majukumu mengi ambayo naamini kabisa ingekuwa kila mara inaathiri mahudhurio katika vikao. Kwa hiyo, mabadiliko yaliyofanya nakubaliana nayo. Bali ningependa kuongeza tu kuwa hapa haionyeshi wazi kama kwamba bodi hii itakuwa na Katibu ingawa huko mbele *by implication* ametajwa. Nafikiri wangeongeza kifungu kinachosema kwamba kutakuwa na Katibu ambaye ama atakuwa mteuliwa binafsi au sivyo, Katibu ambaye atakuwa vilevile ni Mshauri wa Sheria ndani ya Mamlaka au sivyo kutamka kwamba Mkurugenzi Mkuu ndiye ambaye atakuwa Katibu. Ukifanya hivyo muundo wa hiyo Bodi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyiningine ambayo ningependa kuitolea maoni ni kifungu cha 9 pale ambapo kinazungumzia majukumu ya bodi. Nashukuru kwamba kuna marekebisho yamefanywa lakini wangeongeza kifungu kinachozungumzia kuthibitisha hesabu za Mamlaka (*Approved Audited Accounts*) ambayo mle ndani kunakuwa na *statements* zote zile nyiningine pamoja na ile *reserve* ya *authority*.

Pia vilevile ningependekeza kwamba kifungu cha 12 katika ukurasa wa 12 ambacho kwa kweli kinazungumzia kazi ya Bodii kingejamishwa na kuja katika eneo hili ili iwe ni sehemu ya (e) *Appointment of Staff other than the DG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoka hapo ningependa kutoa maoni vilevile katika kifungu cha 11 ambacho kinaelezea kazi za Mkurugenzi Mkuu. Hapa ningependa iongezwe kazi nyiningine yaani kazi yake itakuwa ni "coordinate the authority's activities kwa sababu huyo ndiye coordinator other than supervision" lakini vilevile ana-coordinate kazi za Idara mbalimbali. Vilevile kungeongezwa kifungu kingine kinachosema advise the board on policy matters maana yeye ndiye anayeishauri Bodii wanapotaka kuweka mikakati na policies.

Vilevile Mkurugenzi Mkuu ana jukumu la kuteua *staff* ambao wako chini lakini hawako chini ya Kamati ya Uteuzi. Kwa hiyo, kingeongezwa kifungu kinachosema *Appoint Junior Staff who do not fall under the Appointment Committee*. Hii nadhani itakuwa imekamilisha kazi za Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoka hapo nina maoni katika kifungu cha 15. Ukisoma katika kile kifungu cha 1 halafu ukienda katika kifungu cha 2 naona kama kuna mwanya pale. Haiwezekani wazungumzie kwamba Bodi itaamua muda ambapo watu wanaweza wakakagua ile *register*. Nafikiri ingekuwa vizuri baada ya kile kifungu cha kwanza kungewekwa kifungu kingine kipy cha 2 kinachosema: “*such a register shall be open for inspection by the public or by anybody*”. Halafu ukishaleta hiki kifungu cha pili kikawa kifungu kidogo cha (3) kinaleta *meaning* kwamba tayari kumesharuhusiwa watu waende wakakague.

Katika kifungu cha 16 nafikiri kuna neno dogo tu, baada ya neno *scheme* katika mstari wa kwanza kungekuwa na maneno “*act as a Manager*” na kuendelea. Lakini katika kifungu cha 6(2) kunasemekana kwamba kutakuwa na ada, mimi nafikiri ingetajwa kwamba ni ada ya aina gani. Ukiacha wazi tu namna hii maana yake unaiambia Bodi kwamba yenyewe tu ndiyo itakuwa inaanua, leo wanaamua hivi na kesho wanaamua vingine.

Katika kifungu kidogo cha 16(3) vilevile pangewekwa muda ambao Bodi ingelikuwa inapitia maombi kisha wakarudisha majibu, vinginevyo wanaweza wakaamua kukaa na maombi kwa muda mrefu sana bila ya kuwajibu walioomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niende katika kifungu cha 20(1)(a), pale mwisho pamewekwa maneno *for public interest*, nafikiri ingekuwa vizuri maneno haya yanageainishwa katika sehemu ya kwanza ya Muswada ili ijulikane *public interest* ni nini *otherwise* itakuwa ni *too wide*.

Katika kifungu cha 21 (2) kuna maneno pale kuanzia mstari wa 3 mwishoni kuendelea na wa nne *take over the distribution or transfer of the assets under the supervision of the scheme in order to protect the interest of the member*. Mimi nafikiri inamaanisha kwamba Mamlaka sasa itakuwa ina-subsidize wale ambao hawana uwezo. Hapa nataka kutahadharisha tu kwamba isije ikatokea mifuko mingi ambayo inakuwa katika hali hii ya kutokuwa na uwezo halafu ikawa Mamlaka kila wakati inakuwa ina-subsidize, kama hivyo ndivyo kuna hatari ya kuafilisi hii Mamlaka ambayo tunaiunda kuwa na *endless subsidization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo nataka kuitolea maoni ni Ibara ya 50 kifungu cha (1) na kifungu kidogo cha (2), inasemekana kwamba Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndiye atakayekuwa anakagua vitabu hivi. Mimi nauliza kulikoni? Mbona Mamlaka nyingine nyingi sana zinakaguliwa na wakaguzi wengine ambao wanatambulika na Serikali na ambapo tunajua kabisa kwamba Mkaguzi Mkuu wa Serikali kazi yake ni kukagua vitabu nya Serikali. Labda pengine Mheshimiwa Waziri

angependa kueleza kwa nini Mamlaka hii *specifically* iwe inakaguliwa na Mkaguzi wa Serikali ambaye tayari ana kazi nyingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika jedwali kile kifungu cha 5 kuna maneno yanayoishia mstari wa pili yanayosema *shall be authenticated by the signature of the Secretary and the Director General.* Vilevile kifungu kidogo cha (2) kinasema *signatures of the Secretary and the Director General.* Mimi nafikiri hapa ni mali ya Mamlaka, inayohusika na mwenye mali ya Mamlaka ni Bodi. Kwa nini *authentication* isifanywe katika sehemu zote mbili na Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Mkurugenzi Mtendaji? Kuwaachia Watendaji pekee kuwa wao ndiyo wanao-authenticate mambo mazito kama haya yanayotaka *seal* ya Mamlaka, nafikiri ni kuruhusu *management* kufanya yale wanayoyataka wakati wajibu huu ni wa Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika madhumuni na sababu ile *section* ya Kingereza katika ukurasa wa 33 namshauri *professor* kweli kingereza siyo lugha yetu lakini akisoma vizuri *paragraph* ya kwanza inahitaji masahihisho, *paragraph* ya pili inahitaji masasahisho, ya tatu inahitaji masahihisho na ya nne pia inahitaji masahihisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni kengele ya kwanza hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Ni ya kwanza!

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Bado ninao muda basi!

**NAIBU SPIKA:** Usi-indicate basi hayo masahihisho.

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Kwa hiyo, mapendekezo yangu ingekuwa kwanza lile neno la kwanza katika *paragraph* ya kwanza “*too*” liondoke na halafu maneno yanayofuata baada ya *powers to give* yaondoke na badala yake tuweke neno “*of*” ili sentensi isomeke: “*This part proposes powers of the Bank of Tanzania to inspect and examine the scheme .....*!” mpaka mwisho.

Katika *paragraph* ya pili napendekeza mstari wa pili baada ya neno *proposes* lile neno “*for*” liondoke na liwekwe neno “*the*” halafu italeta maana nzuri. Katika *paragraph* ya tatu mstari wa mwisho baada ya Tanzania *on* lile neno *matter* liondoke ili sentensi isomeke *It also sets out the powers and responsibilities of Bank of Tanzania on Financial related matters.*

Mwisho, *paragraph* ya mwisho nilikuwa napendekeza katika mstari wa pili baada ya neno *regulations* ondoa ““ weka and halafu baada ya neno *authority* ondoa neno *of* weka to sentensi itakuwa kamili na inayolewewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita msemaji anayefuata, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu mzuri wa Muswada wa Kudhibiti Hifadhi ya Jamii.

Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Watendaji wa Wizara chini ya Katibu Mkuu, na wadau wote ambao walishiriki kikamilifu katika kuandaa na kuujadili Muswada huu. Aidha, niipongeze Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kuupitia, kuuchambua Muswada huu na kuuleta mbele yetu kama ambavyo tunavyoona leo una marekebisho mengi sana ambayo ni matokeo ya kazi nzuri ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba nauunga mkono Muswada huu pamoja na marekebisho yake na mimi vilevile nitatoa maeleo au mapendekezo mengine ya kuuboresha Muswada wetu. Nataka nisisitize kwamba tumeanza vizuri lakini bado kuna safari ndefu mbele yetu ya kuirekebisha Sekta hii ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Jamii na hasa taasisi zake zina uwezo mkubwa sana wa kifedha, uwezo ambao haujatumika vizuri katika kusaidia maendeleo ya nchi hii na hasa kwa sababu bado ni *fragmented*. Leo Shirika hili linaamka, linajenga nyumba huku, lingine linaamka, leo linafanya jambo hili na kadhalika. Mawazo yangu hapa ni kwamba wakati sasa umefika kwa Serikali kutumia uwezo mkubwa wa taasisi hizi kwa kununua dhamana za Serikali za muda mrefu ambazo zinaitwa Hati Fungani; za muda wa miaka saba mpaka kumi halafu pesa zile ziingizwe katika mpango wa nchi wa maendeleo katika maeneo ambayo yatatuletea maendeleo sambamba na kuyaachia au kuziachia taasisi hizi nazo kuwa na fursa ya kuchagua maeneo yale ambayo wanadhani wakiwekeza wataweza kuboresha mafao ya wanachama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo au dibaji hiyo ya jumla sasa nije kwenye maeneo *specific*, nianze na *section* ya 24(5) ambayo inazungumzia juu ya haja ya *ku-create reserves* kama ambavyo zitaelekezwa na Benki Kuu. Kwa utaratibu wa kimahesabu ninayo nakala ya taasisi moja hapa ambayo inaonyesha jinsi wanavyoweka mahesabu yao, hii ni nakala ya hesabu za mwaka yaani taarifa ya mwaka.

Ukweli ni kwamba mwisho wa mwaka baada ya kutoa gharama zote kutoka kwenye mapato yote ya mwaka, fedha zinazobaki zinaingizwa katika mfuko kwa ajili ya kuziwekeza tena ili ziweze kuboresha mafao ya wanachana. Sasa inapokuja *section* hii wakasema wanataka kuwe na *reserve fund*, napata tatizo hii ni *reserve fund* ipi?

Wasiwasi wangu ni kwamba kabla ya marekebisho makubwa hayajafanywa, katika Muswada huu kulikuwa na sura inayojitokeza ya Benki Kuu kuhusika kama msimamizi wa kwanza wa shughuli za mifuko ya hifadhi ya jamii na kwa maana hiyo dhamira hii ya *reserve* mimi ilikuwa inaniogopesha isije ikawa ni dhamira ile ya *reserve*

ambazo zinatumika kwenye benki zinazojulikana kama *minimum statutory reserve* ambayo benki yoyote ambayo inakusanya *deposits* inapaswa iweke *minimum statutory reserve*.

Benki Kuu na hiyo inakua *prescribed* na Benki Kuu na kwa sasa hivi nadhani kiwango hicho kiko kwenye *around 12.5%* na kama kimebadilika masahihisho yanaweza kufanywa ila ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba *reserve* ambayo kama ilikuwa inakusudiwa *minimum statutory reserve* basi hizo ni kwa ajili ya benki tu na siyo kwa vyombo vya Hifadhi ya Jamii kwa sababu vyombo hivi vya Hifadhi ya Jamii havina uwezo wa ku – *create money* kama vile benki zinavyoweza ku-*create money* kwa kutumia *deposits* za wateja wao.

Benki zina – *create money* kwa kutumia *deposits* za wateja wao na kwa maana hiyo ndiyo maana wanawekewa *statutory reserve* kupunguza uwezo wao wa ku-*create additional money* kwenye *economy*. Hizi taasisi za Hifadhi ya Jamii hazina hiyo *capacity* kama vile wanavyofanya benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo pamoja na marekebisho ya *section* hii bado mimi sioni kama kuna haja hata kuwepo, maana yake sasa hata *section* hii imerekebisha ili isomeke kwamba *reserve* hizo ziwepo na zitakuwa *available* kwa taasisi hizo kwa ajili ya ku-*invest* kwa ajili ya mafao ya wanachama wao. Sasa hali hiyo ndivyo ilivyo na kama hali hiyo ndivyo ilivyo kuna haja ya kuzungumza ziwe *created reserves* ambazo zitakuwa *available* kwa ajili ya re-*investment*? Mimi ninavyoiona hii ni *redundant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunataka kufungua sekta hii kwa wawekezaji binafsi, yaani wawepo wawekezaji binafsi ambao wataanzisha *schemes* zao za pensheni. Nasema pamoja na nia nzuri ya kufanya hivyo lakin tuwe waangalifu sana kwa sababu tusipokuwa waangalifu sana na tusipojitarisha kiasi cha kutosha tutaifungua sekta hii kwa matapeli, wataanzisha mifuko ya pensheni muda si muda watafunga na watapotea na tusiwajue walipopotelea.

Hayo yametokea, kuna *case study* moja ilitokea Uingereza, Kampuni inaitwa *Maxwell*; huyu *Maxwell* alifungua *scheme* yake ya pensheni akawa anaitunza, lakin alivyopotea kiajabu ajabu walioumia ni wanachama wake. Kwa hiyo, tuwe waangalifu sana, kama azma yetu ni kufungua sekta hii kwa sekta binafsi ni lazima tuiwekee taratibu nzuri na za uhakika ili tusije kupata madhara ya watakaofungua Mfuko ya Pensheni wakati ni kampuni ambazo hazina viongozi waadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ambayo nilifikiri tungeifanya sasa pamoja na kuanzisha Mamlaka ya Taasisi ya Hifadhi za Jamii ni kuangalia kwa kiasi gani hizi Hifadhi za Jamii zingepunguzwa, kwa maana ya kuunganishwa zile ambazo ukiziacha kama zilivyo, zitaendelea kushindania wateja wale wale na kwa maana hiyo, wanachama waliopo katika taasisi hizo, hawatoshi kuvifanya vyombo hivyo viweze kutoa huduma zao katika hali ambayo gharama zao zingeweza kuteremka kama zingeunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ninataka nitoe mfano wa Shirika letu la *PPF*, ilianzishwa kwa ajili ya kushughulikia pensheni za wafanyakazi wa Mashirika ya Umma na jina lake ndiyo linasema hivyo hivyo *Parastatal Pensions Fund*. Sasa kwa sababu ya mageuzi yetu ya kiuchumi, mashirika yetu ya umma yamekuwa yakibinafsishwa siku hadi siku, matokeo yake tumejikuta kwamba, Shirika hili tulilolianzisha kwa ajili ya Mashirika ya Umma sasa wateja wake wamepungua sana nalo limeingia kwenye sekta binafsi. Sekta binafsi ilikuwa ni eneo la Shirika la *NSSF*, kwa hiyo, unakuta mashirika mawili ya umma yanapigania wanachama, ninadhani hapo hoja yangu nimekwishaieleza ya ku-*rationalize* Mifuko yetu ili isishindane *unnecessarily*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section 36(1)*, kama tukiweza kufungua au kuruhusu wanachama wapewe dhamana kwa ajili ya kujenga nyumba basi twende mbele zaidi turuhusu wanachama waruhusiwe kupata mikopo mingine kwa kutumia dhamana yao kama wanachama wa *pension fund* na isiwe kwenye nyumba tu, kwa sababu mahitaji ya wanachama ni mengi, wanahitaji *school fees*, wanahitaji kuuguza watu wao na kadhalika. Kwa hiyo, kama tunakubali kuruhusu dhamana itumike kwa kujenga nyumba, basi waruhusiwe na kwa mambo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section 45(3)* bado inazungumzia *creation of reserve funds* ambayo nimekwishaizungumzia hapo mwanzo inahitaji marekebisho. Nafasi ya Benki Kuu *Section 46(a)* ni sawa lakini (b) na (c) ni *redundant*, kwa utaratibu kama vile zilivyo sasa hivi ni *redundant*, ni lazima zibadilishwe iingizwe matumizi ya *authority* hapo na siyo Benki Kuu yenewe moja kwa moja. Tarehe ya kuanza matumizi ya Sheria hii ikiwa itapita, itakuwa vizuri kama itaendana na marekebisho ya Sheria ya Mifuko iliyopo.

Ukianza kuitumia sheria hii kabla hujarekebisha Sheria za Mifuko mingine ni sawasawa na kumuweka farasi nyuma ya mkokoteni; mkokoteni hauwezi kwenda. Sheria hii imekuja ili isimamie Mifuko. Mifuko ina sheria zake, kuja kwake kama hujarekebisha zile sheria nyingine wale wenye Mifuko ile wanaweza kusema hatukutambui kwa sababu sisi Sheria yetu imetuunda hivi na utaratibu wetu ni huu. Kwa hiyo, *effective date* ilinganishwe na jinsi gani hizo Sheria nyingine zitabadilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaona niende haraka haraka kwa sababu kuna mambo mengi ya kuzungumza na kengele ya kwanza imekwishalia, sasa ninaweza kurudi nikaanza kuelezea kwa nini hasa ninadhani sheria yetu au kazi tunayoifanya kusema kweli ingekuwa nzuri zaidi kama tungetafuta njia ya kuifungua Sekta ya Pensheni ili iweze kuwapata Watanzania wengi zaidi kuliko ilivyo sasa. Sasa hivi Watanzania wanaohudumiwa na sekta hii ya Hifadhi ya Jamii ni kidogo sana, tunazungumzia asilimia mbili ya Watanzania ni ndogo sana. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia namna ambavyo Watanzania wengine asilimia tisini na nane na ambao hasa ni wakulima na wafugaji wanawezaje na wao kufaidika na Sekta hii ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize tu umuhimu wa Sekta hii ya Hifadhi ya Jamii na hasa vile vyombo na fedha walizonazo kwa maendeleo ya uchumi wetu. Hatujawenza

kufanya vizuri katika eneo hilo, kwa sababu hatuna utaratibu mzuri wa kuweza kutumia *resources* hizi nyingi kwa ajili ya kuzielekeza kwenye maendeleo ya nchi. Hivi karibuni tulikuwa tunasikia shirika moja lilikuwa lijenge daraja kubwa la Kigamboni, wale wana fedha; kujenga daraja Kigamboni ni sehemu ya maendeleo ya nchi hii, lakini inasikitisha kuona kwamba mpaka leo uamuzi wa Serikali kutumia uwezo wa shirika hili ili kuondoa matatizo ya wananchi pale Kigamboni bado unasuasua.

Sasa haya ndiyo maeneo ambayo Serikali ingeayaangalia kwa ajili ya maendeleo na kwa jinsi gani tunaweza kutumia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuendeleza maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa nami ili nichangie katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana. Mifuko hii hukusanya fedha nyingi sana kutoka kwa wananchi na hizi pesa zikipangiliwa vizuri, zinaweza kuwa za msaada mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Katika ajira kwenye shughuli za kibiaashara, unaweza kukusanya pesa za kupeleka katika Mifuko ya Ustawi wa Jamii kuliko pesa ambayo unakusanya kupeleka katika mamlaka ya *TRA* kutokana na mishahara ya wafanyakazi. Hii ni kwa sababu kodi ya wafanyakazi huwa ina kiwango cha kuanzia, lakini malipo ya kwenda katika Hifadhi za Jamii huwa yanaanzia mwanzo kabisa wa mshahara wa mfanyakazi. Kwa hiyo pesa nyingi hukusanywa na pesa hizi zingeweza kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuundwa kwa mamlaka hii, kuweka sheria hii ya kusimamia Mifuko hii ni jambo muhimu kabisa na ambalo lingekuwa limewekwa mapema kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Mifuko kadhaa ya Ustawi wa Jamii ikitoa mikopo hata kwa wale ambaio si wanachama wake, tunashuhudia Mifuko hii inajenga na kuwekeza katika majengo lakini hatuna uhakika Mifuko hii katika kujenga majengo mengi, imefanya *diversification* ya kutosha kujilinda na *risk* ya kuporomoka kwa thamani na mapato kutoka katika majengo. Tumeona hata kwa siku hizi za karibuni thamani za majengo na uwekezaji katika majengo kwa nchi kubwa kama Marekani zinaporomoka kabisa na zinatikisa uchumi wa nchi hizo. Kwa hiyo, uundaji wa sheria hii utaweka usimamizi mzuri katika Mifuko hii ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada ambaio tunao mbele yetu, ukienda katika *Section* ya 7(1), Bodi inaundwa ya mamlaka hii, suala ambalo lina shida pale ni kuweka watu wazito mno kutoka Serikalini. Niseme na kumshauri Waziri kwamba ni vizuri kuweka Makatibu Wakuu na Gavana katika Bodi hiyo, lakini mara nyingi watu wa namna hii ni watu ambaio wapo *very busy* na mara nyingi kinachotokea si kwamba, Katibu Mkuu anakuja katika Mikutano ya Bodi ni kwamba kila mara mtaishia kuletewa mwakilishi wake, ambaye hana uwezo mzuri kama ambavyo mmeutegemea kutoka kwa Katibu Mkuu mwenyewe au kutoka kwa Gavana mwenyewe. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, badala ya kuweka Makatibu Wakuu kadhaa, ilikuwa ni vizuri kwamba

tunaweka *members* wengine ambao siyo Makatibu Wakuu wala siyo Gavana wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika *Section* ya 25 imeshaongelewa; juu ya *investment guidelines* imeelezwa katika sehemu hiyo na inasemwa kwamba, *I quote: "The Banks shall in consultation with authority issue investment guidelines regarding scheme funds"* kama ambavyo imeelezwa ni kwamba, ingekuwa ni vizuri sisi tunaipatia mamlaka uwezo wa kutoa *guidelines* pekee, kushirikishwa mamlaka mbili ambazo ni Benki Kuu na Mamlaka ambayo tunaiunda lakini pia ni mategemeo yetu kwamba, mamlaka ambayo tunaiunda itasimamia vizuri Mifuko hii ya Hifadhi za Jamii. Ninasema hivyo kwa sababu uzoefu umetuonyesha kuwa, unakuta Mfuko fulani kila mwezi unakusanya pesa za wafanyakazi, mnazipeleka na mkikosa kupeleka mwezi mmoja au miwili hata mkichelewesha tu basi wafanyakazi wake watafika kuja kukagua na kufuutilia na hata kutoa adhabu kwa nini mmepeleka zimechelewa au hamjapeleka kabisa na hii haiendi vizuri.

Ningeshauri hii mamlaka inayoundwa isimamie hii Mifuko ili itende kazi yake vizuri. Si sahihi kwa mfanyakazi ambaye kila mwezi anakatwa pesa na wakati mwingine pesa nyingi, sasa fedha zake zinapelekwa, anakaa miaka mitano au sita, hata mara nyingine hajui ni kiasi gani cha fedha ambazo zipo katika akaunti yake kule katika Mfuko wa Jamii. Ingekuwa ni vizuri hii mamlaka ikishaundwa, isimamie hata haki za wachangiaji katika Mifuko hii. Ni muhimu kwa mfano, mimi wakija kwangu kukagua wanauliza mmepeleka pesa, tumepeleka pesa za miaka miwili au mitatu. Je, huyu mwanachama wenu mnamateera taarifa gani kwamba makusanyo yake katika Mfuko wenu ni kiasi kadhaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona ni muhimu sasa hii Mifuko iwe inaleta *statement* kwa hawa wanachama wake, kama ambavyo mabenki yanafanya na sasa hivi ni rahisi unaweza kutumia *internet* au kupeleka kwa mwajiri hizo *statements* ili huyu mwanachama pamoja na ninyi kuja kukagua kwamba kiasi gani kimekusanywa kwa ajili ya kuleta katika Mfuko wenu wa Hifadhi, lakini pia mwanachama awe anafahamu baada ya miaka kadhaa ana makusanyo gani katika Mfuko wenu wa Hifadhi ya Jamii. Suala hili pia litawasaidieni ninyi wenye Mfuko, kwa sababu huyu mwanachama wenu akipata ripoti yake akafahamu kwamba pesa zake hazijakwenda, atakuwa ni chombo muhimu cha kuwasaidieni kumchagiza yule mwajiri wake kwamba, kumbe miaka miwili pesa hazijakwenda na atawasaidia kufuutilia, kuchagiza na kusukuma kwamba sasa makusanyo yake ambayo yamekatwa na waajiri ambao si wazuri na wamekosa kuyapeleka, wayapeleke katika Mfuko wetu wa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninadhani pia ni haki yake kwa sababu waajiriwa wengine wanakatwa pesa asilimia ishirini zinapelekwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na wakati mwingine kama ana mshahara mzuri, asilimia ishirini ni pesa nyingi na nzuri kabisa. Kwa hiyo, ni muhimu kabisa aweze kupata *statement* angalau mara moja kwa mwaka na kuweza kufahamu kwamba, amechangia nini katika Mfuko wake wa Hifadhi ya Jamii, aweze kufahamu mategemeo yake wakati akistaifu au akiacha kazi, ateweza kupata pesa kiasi gani. Ukitegemea kwamba yeeye achange na achange bila

kukosea ni muhimu pia na wewe kama Mfuko wa Ustawi wa Jamii, uweze kumfahamisha kila mara michango yake inavyokwenda. Kwa hiyo, ninategemea suala muhimu pia ambalo litasimamiwa na mamlaka hii ni kusimamia haki za wale wachangiaji katika Mifuko hii kwa kuchagiza mamlaka hizi ili Mifuko hii iweze kuwataarifu wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba ni mategemeo yetu kwamba, baada ya kuunda mamlaka hii sasa itaweza yenye wekuweka chagizo kuangalia jinsi ambavyo Watanzania wengi wataweza kunufaika na kuweza kuwekeza katika Mifuko hii ya Ustawi wa Jamii. Isiwe kwamba ni wafanyakazi peke yao, tunao wakulima wengi wenye mapato mazuri.

Kwa mfano, kule katika Mkoa wa Kagera tuna wakulima wa kahawa, anataka naye akizeeka na hawezi kulima tena aweze kuwa na mahali ambapo amewekeza na anaweza akatunzwa na kupata pesa za matumizi, pesa za kwenda kujitibia na kutumia uzeeni na hiyo inawezekana tu kuitia katika Mifuko hii ya Ustawi wa Jamii.

Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba, mamlaka hii ikiundwa sasa itakuwa *organized* vizuri na itaangalia kwa mapana kabisa na itaweza kufanya wachangiaji katika Mifuko hii wawe wengi. Hii pia itasaidia katika kuweza kufanya Mifuko hii iwe na pesa nyingi zaidi na kama kutakuwa na pesa nyingi zaidi za makusanyo na *savings* katika nchi yetu, itakuwa ni mtaji mkubwa sana wa kuweza kusaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikushukuru kwa kuniruhusu na ninasema kwamba, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada ya leo, ambayo inahu Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini na kuweka utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa sekta hii. Kabla sijachangia, ninapenda kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu, pamoja na timu yote ya Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa muda mrefu sasa Sekta ya Hifadhi ya Jamii haikuwa na chombo cha kuwaunganisha au chombo cha udhibiti. Kwa hiyo, Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003, haijatekelezwa mpaka sasa tangu ilipoundwa. Kwa hiyo, sheria hii imekuja kwa muda mzuri kwamba, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii itakuwa na chombo cha kudhibiti na kuweka utaratibu ambao utafuatwa na Mifuko yote. Kwa sasa kuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayolipa pensheni aina tatu za mafao, kuna inayolipa aina moja na kuna inayolipa aina saba za mafao. Kwa hiyo, kila Mfuko unalipa mafao kutohana na sheria iliyotungwa na Bodi yao. Kwa hiyo, ninaamini kabisa sheria hii itasaidia na itawawezesha wanachama wengi kunufaika na Mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya na hasa kuhusu Mfuko wa Mkopo wa Ujenzi kwa Wafanyakazi. Wafanyakazi wengi kama tunavyojuwa kwamba, mishahara ya Watanzania au wafanyakazi

ni midogo mno, kwa hiyo, wafanyakazi hawana mahali pa kukimbilia ili wapate mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao na utakuta walio wengi baada ya kustaafuli na kupata hiyo pensheni ndogo wanayoipata, ndiyo wanakimbilia kujenga. Kwa hiyo, kama kuna Mfuko ambao utawasaidia kupata mkopo kama Kamati ilivyopendekeza kwamba, asilimia ishirini ya fedha za Mfuko ziende katika kuwakopesha wafanyakazi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba; ninaona ni jambo zuri.

Kutokana na ugumu wa masharti ya mabenki yetu, wafanyakazi wengi wanashindwa kukopa kwa ajili ya kujenga, kwa hiyo, Mfuko huu utawasaidia sana wafanyakazi walio wengi kuijandaa kabla hawajastaafu na ukishafika muda wa kustaafuli, pensheni watakazopata zitawasaidia kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niungane na Kamati kwamba, suala la kuhamisha michango au mafao kutoka Mfuko huu kwenda Mfuko mwingine ni utaratibu usiofaa sana, ambao utawapa tabu sana Mifuko hii na hata wanachama wenye kudhibiti mafao yao; kwa sababu Mifuko hii ambayo wachangiaji wengi ni waajiri kwa mfano, Mfuko wa *NSSF* na hata *PPF*, wachangiaji wengi ni wafanyakazi na waajiri binafsi na utakuta waajiri wengine hawapeleki michango kwa muda unaotakiwa, kwa hiyo, mwanachama anakaa kwa miaka hata miwili au mitatu, michango yake haijapelekwa katika Mifuko hii. Sasa tukisema kwamba mwanachama anapopenda kuhamisha michango yake kutoka Mfuko mmoja kwenda Mfuko mwingine, italeta matatizo makubwa na italeta migogoro mikubwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa hiyo, ninaungana na Kamati kwamba, michango au mafao ambayo yameshapelekwa katika Mifuko husika, basi ibaki vile vile katika Mifuko hiyo, hata kama mwanachama atapenda kuhama lakini asihamishe pesa katika Mfuko aliojisajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda sasa kwenda katika Muswada wenye kuna hadi katika Kifungu cha 7(1) katika *Schedule of Amendments*, ambayo tumeipata asubuhi ya leo. Mheshimiwa Waziri amefanya marekebisho katika Wajumbe wa Bodi na amewatoa Makatibu Wakuu, ambao wangkuwa Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka husika. Amemtaja Msajili wa Hazina kwamba, atakuwa mmoja wapo wa Wajumbe wa Bodi na *Labour Commissioner* atakuwa Mjumbe wa Bodi ya Mamlaka. Tatizo langu siyo Wajumbe wa Bodi, lakini tatizo langu ni kwamba, kuna baadhi ya Mifuko ambayo Makatibu Wakuu ndiyo Wenye viti wa Bodi, sasa ninapata wasiwasi kwamba, Kamishna wa Hazina yuko chini ya Katibu Mkuu wa Hazina na Katibu Mkuu wa Hazina ni Mwenye kiti wa Bodi ya *PPF* na Bodi ya *PSPF* na hata ukirudi katika Mfuko wa *LAPF*, Mwenye kiti wa Bodi ni Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapata tabu inapokuja kwenye uwajibikaji kwamba, Mfuko utakapotakiwa kuwajibishwa na mamlaka kwamba, hawakufanya vizuri katika utendaji, ina maana na Katibu Mkuu ambaye ni Mwenye kiti wa Mfuko ule atawajibishwa. Sasa ninaona ni aibu au siyo vizuri kwamba, Katibu Mkuu amewajibishwa kutokana na utendaji wake katika Bodi ya Mfuko. Nilikuwa ninadhani kwamba ni vizuri Makatibu Wakuu ambao ni Wenye viti wa Bodi ya Mifuko hii, waachie hiso nafasi na wateuliwe Wenye viti wengine ambao Bodi hii ya Mamlaka itafanya nao kazi kwa uwazi zaidi. Ukiniambia kwamba Msajili wa Hazina amwajibishe Katibu

Mkuu ambaye anawajibika kwake, ninaona kwamba Bodi haitakuwa na ufanisi katika utendaji wake. Kwa hiyo, ninaomba Sheria iliyounda Mifuko hii ambayo Wenyeviti ni Makatibu Wakuu wa Wizara husika, basi nafasi hizo wapate Wenyeviti ambaio sio Makatibu Wakuu ili mamlaka iwe na ufanisi zaidi katika kutenda kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 31(a), ninaomba ninukuu: “*Pension benefits the authority may where necessary.*” Sasa ile *may* inanipa tabu kwamba, Mfuko wowote unaweza kufanya kwa muda unaotaka, lakini likiwekwa neno *shall* ina maana lazima atekeleze, kwa hiyo, ninaomba lile neno *may libadilishwe* liwe *shall* ili Mifuko hii iwe na wajibu kama sheria inavyosema katika Kifungu cha 31(a).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaipongeza Kamati kwa kuona kwamba ni wajibu wa kila Mfuko, kumlipa mwanachama kulingana na hali halisi ya kifedha. Sasa hivi mafao yanayolipwa kwa wanachama hayalingani na hali ya maisha, kwa mfano, *accounts* za wanachama ambazo zimekuwa *dormant* kwa muda mrefu, mwanachama analipwa pale alipokoma kuchangia. Mwanachama hapendi kuwa *dormant* au kama mwajiri wake hapeleki michango yake kwenye Mfuko siyo tatizo la mwanachama ni tatizo la mwajiri, kwa hiyo, mwanachama asiadhibiwe kutokana na makosa ya mwajiri wake.

Kifungu cha 32 kinazungumzia suala la kodi; Wafanyakazi wa Tanzania wanapata mshahara mdogo sana na katika mshahara huo mdogo wanakatwa kodi hata kabla michango haijkwenda kwenye Mifuko hii na pesa ambazo zinatokana na *investment* pia zinakatwa kodi. Ni kweli mfanyakazi anaonewa. Mimi ninadhani sheria hii iangalie uwezekano wa kuboresha mafao ya mwanachama na sio kila pato la mwanachama au pato la mfanyakazi likatwe kodi; akatwe kodi katika mshahara wake, lakini pesa zinazotokana na vitega uchumi lisikatwe kodi ili kuboresha mafao ya wanachama au wafanyakazi kwa sababu vitega uchumi vinaongeza riba au *interest* kwa mafao ya wanachamaau wafanyakazi. Kifungu cha 16(1), nina sahihisho dogo, ninaomba ninukuu: “*A person intended to establish a Scheme Act.*” Mimi ninaona kuna ukosefu wa neno moja hapo, wanaweza kuandika “*a scheme or Act*”, nilikuwa ninapendekeza neno “*or*” liwe katikati ya *scheme* na *act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**NAIBU SPIKA:** Ninadhani Mheshimiwa Janguo alipendekeza hilo kwa hiyo, mnasisitiziwa Wizara. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kifungu cha 29 kinatamka kwamba, mwanachama ana uhuru wa kuchagua Mfuko anaotaka. Ninadhani kifungu hiki kiwe kwa ajili ya wanachama au wafanyakazi ambaio ndiyo kwanza wanapata ajira katika maeneo yao au kwa waajiri wao, kwa sababu ukisema kwamba mwanachama ambaye alishawahidi kuandikishwa aandikishwe tena, italeta migongano mikubwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia katika kifungu cha 28(3)(a) na (d) na kifungu cha 29, ninaona kuna *contradiction* kidogo. Ninaomba Sheria itamke wazi kwamba, sehemu hii inawahusu wafanyakazi ambao ni wapya, ambao ndiyo wanaanza ajira na ambao ndiyo wanaanza kuchangia, wao ndiyo waruhusiwe kuchagua kwamba achangie Mfuko wa NSSF, PPF, PSPF au Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo itaundwa. Tukisema kwamba wafanyakazi wa zamani wawe na uhuru wa kuchagua waandikishwe wapi au wahamishe michango yao iende wapi, italeta matatizo makubwa kwa waajiri, kwa wafanyakazi na hata kwa Mifuko yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kifungu cha 29 kitamke wazi kwamba, siyo wale ambao walikwishaandikishwa mwanzo kama Kamati ilivyopendekeza kwamba ni wale ambao wanaanza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake yote, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pili, nipongeze Kamati kwa uchambuzi wake na mapendekezo ambayo wameyatoa kwa maana ya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimefarijika sana na ninaomba niwapongeze wachangiaji wote waliochangia na kilichonipa faraja zaidi ni jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameanza kuchambua vifungu. Hii inaonyesha kwamba, wanasoma Miswada. Hiyo imenipa faraja, kwa hiyo, panapotakiwa kurekebishwa wamesema paweze kurekebishwa. Ninawapongeza sana wachangiaji wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapounda Mfuko huu kwa maana kwamba utajaribu kusimamia Mifuko mingineyo ni jambo la busara sana, kwa sababu wadau wamekuwa wakichanganyikiwa, hawaelewi utendaji, mfumo wa ukusanyaji pengine na ulipaji au ni nani anayetakiwa awe katika Mfuko fulani. Kwa mfano, tunaposema Mfuko wa NSSF anaweza akaingia mtu mwengine ye yote yule wa jamii, mtumishi, watu binafsi na kadhalika. Mfuko kama vile PPF unahitaji wale wa Mashirika ya Umma tu, wafanyakazi waliopo katika Mashirika ya Umma. Mfuko wa PSPF unataka watumishi wa Serikali Kuu. *LAPF* inataka watumishi wa Halmashauri (*Local Government*). Utendaji wa kazi wa Mifuko hii unatofautiana wakati ambapo PSPF unashughulikia Watumishi wa Serikali Kuu, wao wanakusanya mapato yale kupitia kwa mtumishi mwenyewe, kwa jinsi wanavyolipwa mishahara, *pay roll* wakati huo huo tunamwona mtumishi wa *Local Government* mwajiri wake ndiye anayekusanya na kupeleka *LAPF*. Wakati yule aliyepo NSSF ana hiari ya kupeleka yeye na kama pengine ameajiriwa kwa mtu binafsi na mwajiri wake achangie pale kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaona mkanganyiko huu ndiyo ule ambao katika kulipa unamkosesha haki huyo mwanachama. Kwa maana kwamba, kama huyo Mtumishi wa Serikali Kuu kwa kupitia *Pay Roll* yake anakatwa moja kwa moja, siyo rahisi akashindwa kuchangia kwa mwezi kwa sababu kila mwezi anapata mshahara. Lakini huyo anayechangia *Local Government* licha ya kusema na yeye anapata mshahara kila mwezi, hana fursa ya mshahara kukatwa moja kwa moja kupitia *Pay Roll*, bali mwajiri wake ndiye anakusanya zile fedha anazipeleka na anaweza akazila ama asizipeleke. Unapokuta PSPF wanapokuwa na utaratibu mzuri sana wa kutaka *data* za mtumishi anapokuwa kazini kabla hajastaafu zifike kwao ili waweze kumwekea utaratibu wa kila mwezi kama amelipa ama hakulipa na kumwandalia *chart* maalum. Baadhi ya Mifuko mingine haifanyi kazi ya namna hiyo na kwa hiyo, mwishoni mwanachama ndiye anayekuja kuhangaika kupata mafao yake. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sasa Mfuko huu uweze kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, Mifuko yote angalau inalingana katika utendaji wa kazi ili kutenda haki kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba kuhakikishiwa kwamba, wale waajiri wote ambao wanatakiwa kupeleka michango kwenye Mifuko inayohusika wapeleke na siyo kupeleka tu kwa sababu inawezekana wakawa wazembe zaidi. Sasa Mifuko iweze kurekebisha Sheria na kuweka adhabu kali kwa wote wanaoshindwa kwa sababu kushindwa kufanya hivyo, maana yake pia ni kuikosesha Serikali mapato ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa waajiri binafsi, bado sijaona kama Sheria imetenda haki, kwa sababu naona hapa imekaa kimya ni kama inamteteta yule mwajiri binafsi kuliko kumtetea mwajiriwa, ambaye analazimika kuwa mwanachama katika baadhi ya Mifuko hiyo. Vilevile mwanachama hapewi haki wala haangaliwi yeye kwamba kama huyo mwajiri binafsi anashindwa kupeleka michango yake kunakohusika, sijaona mahali ambapo amepewa haki huyo mwajiriwa kuweza kwenda kushtaki na anaposhtaki chombo maalum kinachohusika kumsaidia Kisheria ili aweze kupata haki yake na kama kipo, mara nyingi huwa vipo wanakwenda Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na mara nyingi sana wanapata shida na hata hukumu zinapotolewa, yule mwanachama katika Mfuko huwa hapewi haki. Mahali gani ambapo mwanachama ana uwezo wa kuushtaki huu Mfuko kama anasumbuliwa, anayanyaswa au ambapo amepunjwa mafao yake ya haki? Nilikuwa ninaomba pawepo na sehemu inayompatia fursa mwanachama mwenyewe, kuweza kuushtaki Mfuko na ikiwezekana kudai fidia anayoitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana katika Mifuko mingi kumekuwa hakuna uaminifu wa kutosha na kumekuwa na usumbufu wa kutoa hayo mafao wanayoyasema. Hakuna taratibu za wazi zinazomfanya mwanachama achukua hatua ili aweze kupata haki hiyo. Kwa hiyo, taratibu za wazi ziwekwe na elimu itolewe kwa kila mwanachama ili aweze kufahamu kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kukaguliwa Mifuko kwenye kifungu cha 38(1); kama Kamati ilivyopendekeza ni vizuri ikaguliwe mara moja kwa mwaka. Kukagua mara mbili kwa mwaka tusidanganyane itakuwa ni ngumu sana na kwa hiyo, kama itashhindikana na kama leo hii maeneo mengi ukaguzi wake unakwenda kwa mwaka

mzima, mahesabu yanatolewa kwa kila mwaka, ukisema wafanye ukaguzi wa mara mbili kwa mwaka na wakashindwa kufanya hivyo, watakuwa wanavunja Sheria na mnafahamu mlolongo wa ku-*amend* Sheria unavyokuwa mgumu. Kwa hiyo, itakuwa ni ngumu sana kulitekeleza hilo.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kama nilivyosema, wengi wamenifilisi maana yake vifungu vingi walivyokuwa wamevisema na mimi baadhi nilikuwa navyo, sikuwa na haja ya kuvirudia. Kwa hiyo, ni kweli Miswada inapoletwa mara nyingi haiwashirikishi wadau wengi, inakuwa kama vile ni siri. Ninawaomba hao watu wenye taaluma ya Sheria, wajitahidi sana kuleta Lugha ya Sheria.

Mimi ninashangaa umesomea taaluma ya Sheria, anayekuja kukusahihisha Kiingereza cha Kisheria ni mtu ambaye amesomea Uchumi au Mahesabu siyo vizuri! Wale mnaoandaa hii Miswada, muiandike Kisheria ili kuepuwa masahihisho madogo madogo ya *may, the, a*, na vyovyyote itakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa ninaomba wadau waweze kushirikishwa kwa pamoja ili kuepuwa *amendments* zisizokuwa za lazima sana za mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mse maji wetu wa mwisho kwenye orodha yangu niliyonayo na kama nilivyosema, sina mchangiaji mwingine aliyeomba. Huu ni wakati mzuri Wizara ikaenda kupidia haya machache waliyozungumza Waheshimiwa Wabunge, hasa mabadiliko madogo madogo yaliyotolewa na wachangiaji hapa tulipo.

Kwa sababu wametumia haki yao ya Kifungu cha 86(9), ambacho kinasema mto hoja au mchangiaji anaweza kumshauri mto hoja kufanya mabadiliko katika ibara mbalimbali.

Kwa hiyo, ninadhani wamezingatia na tukija ibara kwa ibara ikifika kipindi hicho ama wale waliotha hoja wataongea tena au Wizara kama itakuwa imejandaa, basi itaeleza panaporuhusu kubadilika. Kwa hiyo, ningependa kutoa nafasi kwa Wizara waendelee kutafuta majibu turudie saa 11.00 jioni wakati wa kupidisha ibara kwa ibara.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.43 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha kikao mchana, nilieleza kwamba, wasemaji wangu waliokuwa wameomba wote walishapata nafasi. Kwa hiyo, sasa ninaingia upande wa kutoa hoja; nitaanza na Naibu Waziri.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE: MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, NIInaomba nami pia nichukue nafasi hii kuchangia muswada huu muhimu ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kweli kwamba, wafanyakazi na wananchi wote kwa ujumla, wamekuwa wakipata tabu sana juu ya huduma ya Mfuko wa Afya, kwani wanapofika hospitalini huhudumiwa kwanza wagonjwa wa kawaida, ambao hawajajiunga na mfuko wa Bima ya Afya mwisho huhudumiwa wao na majibu huwa hakuna dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imekuwa ikikatisha tamaa wanachama wa Mfuko huo na wakati huo huo pesa inakatwa kama kawaida katika mishahara yao ili wapate huduma kama kawaida! Inakuwa haina maana kabisa Mfuko huu kuwepo lakini pia wanachama wa Mfuko huo hawatendewi haki kabisa.

Ningependa kuishauri Serikali, ipitie upya utaratibu na huduma ya Mfuko huu ili uweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina faida nyingi kwa wanachama pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu matumizi ya fedha za Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. Kwa maoni yangu, wanachama wa Mifuko hii hufaidika tu pale muda wao wa kuchangia unapoisha (kama ameajiriwa), kwa kulipwa mafao na *pension* yake, lakini fedha nyingi za Mifuko hii hutumika katika uwekezaji katika miradi mikubwa yenye kulipa faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza faida inayopatikana kutokana na uwekezaji itolewe pia kwa wanachama. Ninakubaliana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kusimamia Mifuko hiyo kisera ili kuleta uwiano wa aina fulani. Hii itaondoa uwezekano wa Mfuko mmoja kutoa marupurupu tofauti na Mifuko mingine, kiasi cha kuwafanya wanachama wapende kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza wanachama waitumie Mifuko hiyo kuboresha hali zao za maisha kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuwakopesha pesa kwa madhumuni ya maendeleo
- Kuwakopesha vifaa kama sementi na bati ili kuboresha makazi yao.

- Mifuko hiyo ijiingize kwenye shughuli za karadha (*Financial Leasing*) kwa Sheria ya Ukodishaji Rasilimali, ambayo imepitishwa hivi karibuni, inawagusa Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Wengi wa wanachama hao wakistaafu hurudi vijijini ambako ukodishaji wa rasilimali kama zana za kilimo, unaweza kuwa wa manufaa ya ziada kwa wanachama.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na timu nzima iliyoandaa Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kwa kweli umechelewa kutohana na uundwaji wa Mifuko hii kutokuwa na Sheria Mama ya Udhibiti wa Mifuko hii. Kukubaliwa Muswada huu na kuwa sheria ni ukombozi wa Mifuko na nguzo imara itakayoboresha huduma nzuri na kuipa uhai Mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imeelezwa ni idadi ndogo sana ya Watanzania waliojiunga na Mifuko hii, Muswada huu utaleta changamoto ya Watanzania kujiunga na Mifuko watakayopenda, lakini hata hivyo, Mifuko haina budi kujitangaza kwenye vyombo vyaya habari ili Watanzania wafahamu Mifuko hii, pamoja na faida ya Mifuko hiyo .

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ni Mifuko inayokusanya michango ya wafanyakazi na hivi sasa inawekeza kwa kujipatia fedha ili iweze kuboresha mafao kwa wafanyakazi na wastaafu. Katika kulitekeleza hili, Serikali huitoza fedha (kodi); ninaiomba Serikali kupunguza kodi au kufuta kabissa kodi kwa Mifuko. Pia naiomba Serikali kuitumia Mifuko hii katika kuinua hali ya uchumi wa nchi, pamoja na kujenga Miji Mikuu ya Manispaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FLORENCE E. KYANDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma na kuangalia Muswada huu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii, nina maoni ya ujumla kama ifuatavyo:-

Moja, kuwepo Mifuko mingi ya Hifadhi. Kwanza, ninaipongeza Serikali kwa utaratibu mzuri iliyoweka wa kuwepo kwa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, ambayo inawasaidia sana wafanyakazi au wanachama. Kama inavyofahamika, hapa nchini ipo Mifuko mingi iliyo chini ya Hifadhi za Jamii katika Wizara tofauti. Mimi ninashauri kuwa ni vyema Mifuko hii iwe katika Wizara moja tu, ili kusaidia mamlaka tunayounda iweze kufanya kazi yake vizuri na kuepuka migongano isiyokuwa ya lazima ambayo inaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa wapo wanachama wengi wa Hifadhi ambaeo ni wastaafu watarajiwa na wanaitegemea sana michango yao iliyopo kwenye Mifuko hiyo ili walipwe mapema kabla ya kustaaafu kwa ajili ya maandalizi ya maisha

yao ya baadaye lakini wanabanwa na sheria iliyopo kwamba, mpaka watimize umri wa kustaaifu; je, tatizo hili tutawasaidiaje katika sheria hii tunayounda ili waweze kukopeshwa na pesa hizo zikakatwe kwenye malipo yao ya mwisho?

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza wote walioandaa Muswada huu kuanzia kwa Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri; Naibu Waziri, Mheshimiwa Chibulunje; Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na hoja nyingi zilizofafanuliwa na Kamati iliyochambua Muswada huu, lakini nitachangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 10, sehemu (7), vipengele (a - j), Muswada umefafanua muundo wa mamlaka inayotarajiwa kuundwa. Kwanza, ninaipongeza kwa kupunguza idadi ya wajumbe hasa Watendaji wa Serikali ambao ni Makatibu Wakuu wa Wizara zilizotajwa, kwa vile vinginevyo kungetokea mgongano wa kimaslahi ikizingatiwa kuwa, Makatibu Wakuu hao ni Wajumbe wa Bodi wa Mifuko mbalimbali tuliyonayo kwa sasa hivyo, uwezekano wa kuathiri maamuzi ndani ya Mamlaka. Hata hivyo, ninashauri kuwa, suala la uteuzi wa Bodi ya Mamlaka itakayoundwa, lizingatie jinsia na kipengele hiki kiwekwe wazi katika kanuni zinazotungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya 2003, inayoelekeza umuhimu wa kuratibu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tuliyonayo na kwamba, wanachama wa Mifuko iliyopo (ya lazima), hawatalazimika kujiandikisha upya. Ninaomba ufanuzi endapo Mwanachama wa Mfuko wowote, akipata kazi nchi za nje; uchangiaji wake utakuwaje na hivyo mafao yake yatachanganuliwaje?

Kwa kuwa sheria inayopendekezwa inahitaji marekebisho ya Sheria za Mifuko mbalimbali tuliyonayo, ninashauri marekebisho hayo yaletwe Bungeni haraka ili muda wa mpito uwe mfupi, kuepusha mkanganyiko ambao unaweza kujitekeza kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Muswada huu umechelewa kwa vile suala la Hifadhi ya Jamii ni nyeti, linalohusu wananchi kwa ujumla, kwa vile Mifuko yake hufaidisha wanachama kukuza uchumi wa nchi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya, ninaunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja. Baada ya hapo ninayo machache:-

Kwanza, waliokuwa wafanyakazi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, waliostaifu kabla ya mageuzi ya uchumi wana mafao duni sana, kiasi cha kupelekea wengi kutomudu maisha yao. Ninaomba mifuko ya pensheni iboreshe mafao ya wastaafu hao, kwani mifuko inawekeza na kupata faida kubwa sana.

Pili, Mifuko ya Pensheni iwekeze kwenye maeneo yanayolenga kuboresha maisha ya wanachama na kama ni katika ujenzi wa nyumba au viwanda yalenge kuboresha maisha ya wanachama.

Tatu, Mifuko ya Pensheni iache kabisa kukopesha watu binafsi, taasisi na makampuni binafsi. Mifuko ya Pensheni siyo mabenki na hivyo hao watu na makampuni wakakope kwenye mabenki. Kwa tabia ya Watanzania wachache, mikopo mingi hailipiki kwa sababu riba ni kubwa mno, hivyo, kukopesha watu binafsi na makampuni ni kupoteza fedha za wanachama bure; kama ni uwekezaji, yapo maeneo mengi sana ya kuwekeza; ujenzi, hati fungate na kadhalika.

Wanachama; Sekta isiyo rasmi ina wajasiriamali wengi sana ambao wakipata elimu tosha watajiunga katika Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii na kujipatia kinga katika maisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Kwanza, ninapenda kukupongeza sana kwa kuleta Muswada huu muhimu sana. Pili, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninaomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Mifuko hii inachangiwa na mwajiri na mwajiriwa, ninashauri Sheria hii iwabane waajiri ambao wanakata mishahara ya watumishi kwa ajili ya kuchangia Mifuko hii kwa mfano, *LAPF, NSSF* na kadhalika lakini fedha hizo hazipelekwi kwenye Mifuko badala yake zinapangiwa matumizi mengine na watumishi wanapostaifu hawapati mafao yao.

Je, ni fedha kiasi gani ambazo zimekatwa kwenye mishahara ya watumishi lakini hazikupelekwa kwenye Mifuko kwa mfano, *LAPF, NSSF* na hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika?

Je, Serikali imeweuka mikakati gani kuhakikisha kwamba idadi ya wanachama inaongezeka badala ya asilimia mbili tu?

Je, kwa nini *NHIF* ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya imewekwa pamoja na Mifuko mingine kwa mfano, *PPF, NSSF, LAPF*; je, ina uhusiano gani? Ninaomba kuelimishwa.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii, kutoa mchango wangu mdogo kuhusu Muswada huu katika maeneo yafuatayo:-

Serikali ijitahidi kadri iwezekanavyo, kuharakisha kukamilika mipango yote inayohusu Muswada huu, ili utekelezaji wa kuboresha malipo ya mafao ya wastaaifu wa zamani, ambao malipo yao ni duni sana, kulingana na gharama kubwa sana za maisha hivi sasa. Utekelezaji ukikamilika mapema, ahadi ya Ilani ya CCM ya 2005 itakuwa imetekelizwa kwa wakati muafaka.

Mamlaka kuu itakayopewa jukumu la kusimamia mifuko ya hifadhi ni vema zaidi ikawa chini ya usimamizi wa Waziri wa Fedha, kwa sababu mifuko hii ni vitega uchumi. Wizara ya Fedha itatoa uzoefu na utaalal mtambuka ili kuhakikisha vitega uchumi vyta mifuko ya fedha, vinawekezwa katika miradi itakayoharakisha upatikanaji wa faida stahili. Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ibaki kusimamia masuala ya utawala wa kumbukumbu muhimu zinazohusu mtiririko wote wa kila mwajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio siri kuwa wastaafu wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi sana kufuatilia malipo yao baada ya kustaaafu. Katika uboreshaji wa uendeshaji wa Mifuko hii ni lazima Serikali ibuni mfumo utakaohakikisha wastaafu wanatumia muda mfupi uwezekanavyo. Ni vyema taratibu ziweke malengo yaliyo wazi, yanayotamka kwa mfano, tangu kustaaafu, malipo yamfikie muhusika si zaidi ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huu ninaunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko hii ilenye hifadhi kwa wananchi wote kwani hakuna mtu asiyehitaji hifadhi.

Muswada uangalie zaidi wananchi walio wengi ambao hawako katika Sekta Rasmi na ajira zao ni za msimu, vipi wataweza kuijwekea hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada umewashirikisha na kuweza kutoa ushiriki wao, wajasiriamali ambao wanafanya kazi kubwa lakini hatma ya hifadhi yao inakuwa mbaya, kutokana na kukosa mfumo maalum wa kujianaa na hifadhi.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Ninawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwenu na Mheshimiwa Rais, kwa nyadhifa mlizopewa.

Niwapongeze pia Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara, kwa utendaji wenu wa kazi. Vilevile ninaipongeza sana Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuchambua Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko kwenye Bima ya Afya; Mfuko huu ni muhimu sana kwa wananchi hapa nchini. Mfuko wa Bima ya Afya (*NHIF*) ni muhimu uwe kwa wananchi wote, isiwe kama ilivyo sasa hivi; Sekta isiyo rasmi lazima nao wahusike. Mfano, wakulima walio wengi hawako katika Mfuko na wafugaji wamesahaulika kabisa. Njia za kuwapata ni kutumia Waheshimiwa Madiwani wa kila Kata, kwa kushirikiana na Viongozi wa Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa vizuri zaidi endapo dhamana ingekuwa ni mashamba yao au mifugo yao, hata michango yao ingetokana na mifugo na mazao ya kutoka kwenye mashamba yao.

Wakulima au wafugaji wahesabike kama wafanyakazi ambao nao mwisho wao huwa wanastaifu wanapozeeka. Hivyo, wadhamini wao yafaa wawe Viongozi wa Vijiji kwa vyeo ili wafaidike na Mifuko hii kwani Sera ya Serikali ni kila kijiji kiwe na Zahanati na kila Kata iwe na Kituo cha Afya. Mpaka sasa wananchi walio wengi hapa Tanzania, wanateseka sana na huduma za afya hasa akina mama wanapojifungua, watoto na waathirika wa UKIMWI.

Ninaunga mkono kuwa mdhamini au meneja asishtakiwe kwa kosa la mfanyakazi la usajili wake; ni bora adhabu iende moja kwa moja kwa mkosaji, kwani mfanyakazi atafanya kosa kwa makusudi huku akijua kuwa yeye hatahusika. Serikali irekebishe vifungu hivyo lakini hata hivyo, meneja au mdhamini awajibike endapo mkosaji hatakuwepo au kutoroka, kwani ni wajibu wa meneja au mdhamini kuhakikisha mkosaji anakuwepo au anatoa ushirikiano kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninashauri Mifuko hii muhimu ya Hifadhi ya Jamii, yaani *NSSF*, *PPF*, *LAPF*, isambae nchi nzima isiwe kwenye miji mikubwa tu, ifike hata kule vijijini waliko wananchi wengi.

Elimu pia itolewe kwa njia za redio, televisheni, magazeti na vipeperushi vifike hadi vijijini ili wananchi walio wengi (wanyonge), wafaidike isiwe kwa matajiri tu au wale wenye uwezo wa kipato.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Waziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutamka kwamba, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko hii ina uwezo wa kuwekeza maeneo mbalimbali, lakini ninapenda kutoa mchango wangu katika eneo moja tu la kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunayo mazao ambayo yanawasaidia wananchi au Serikali katika kukuza uchumi wetu kwa mfano, kahawa, tumbaku, korosho na kadhalika. Pamoja na kuwa ununuzi wa mazao hayo ni hafifu zaidi; kwa nini kwa kipindi hiki Serikali kupitia Mifuko hii, wasinunue mazao haya na kuweza kuwalipa wakulima na pia kuwakopesha pembejeo; na bado pia Mfuko huu utatafuta bei nzuri na kuuza vizuri zaidi na kupata pato kubwa kuliko hivi sasa wananchi au wakulima wa Urambo wanavyoyauzia Mashirika hayo tumbaku na kipato wanachokipata ni kidogo zaidi? Mfuko uangalie kuwekeza katika kuinua kilimo cha Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya waajiri kuchelewa kupeleka michango ya wafanyakazi wao; hivi sasa kuna kesi ngapi ambazo Mifuko hii hushtaki Mashirika au viwanda ambavyo havijapeleka michango ya wafanyakazi katika Mfuko huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ya udanganyifu wa kutumia hospitali zetu kuhusu utumiaji wa dawa na hata kupitia wale wanaochagua hospitali zao na huko kutumia nafasi hiyo kuandika dawa hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Mheshimiwa Juma Kapuya, Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamati ya Bunge iliyojadili Muswada huu, pamoja na Watendaji walioshiriki kuandaa Muswada huu, wenyewe lengo zuri la kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilianzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa watumishi wote nchini, ninaiomba Serikali kuangalia upya huduma ya Mfuko huu ili uweze kutoa huduma kwa asilimia mia kwa mia kuliko ilivyo sasa, baadhi ya vipimo havilipwi na Mfuko huu, kitendo ambacho mtumishi hushindwa kujihudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama wanachama wote wanaochangia Mfuko huu, hutumia michango hiyo. Hivyo basi, fedha hizo ziwe fidia kwa wale wenyewe vipimo vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kuwa na utaratibu wa kutunza fedha za watumishi za pensheni na kadhalika kwa kuwa wapo waajiri ambao hawapeleki fedha au makato ya watumishi kwenye Mifuko husika na kusababisha watumishi kupata shida pindi wanapostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matumaini makubwa, Sheria hii itafanya kazi nzuri ya kutunza na kudhibiti Mifuko hii kwa maslahi ya wafanyakazi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bima ya Maisha (*NIC*); upo uzembe mkubwa kwenye hii bima ambayo lengo lake ni zuri, watumishi kujiwekea akiba hivyo, Shirika hili kupitia Sheria hii itasaidia kupata haki zao kwa wakati muafaka, kwani huchelewa sana kupata mafao yao bima zao zinapoiva.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mifuko mingi Sheria zake zimepitwa na wakati ni vyema Sheria hii ikaenda sambamba na Sheria za Mifuko yenyewe ili iweze kutoa huduma nzuri na iwe rahisi kuisimamia na kuidhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya mchango wangu, ninapenda kuunga mkono Muswada huu. Ninaitakia Serikali utekelezaji mwema.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa uamuza wa kuleta Muswada huu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja muda muafaka na utasaidia katika suala zima la Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Mheshimiwa Waziri, suala ambalo ninataka kuchangia leo ni kuhusu Mashirika na Taasisi nyingi kutopeleka fedha katika Mashirika ya Hifadhiya Jamii.

Ninaomba Muswada huu uhakikishe kuwa, tatizo hili halitokei kwani kumekuwepo na malalamiko mengi kuwa, watu wanakatwa fedha na waajiri wao lakini hazifkishwi kunakohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, Mifuko hii ambayo itaunganishwa, iangalie pia utaratibu wa kuwaingiza wakulima katika utaratibu huu na kukatwa fedha katika kuweka hifadhi lakini pia waweze kukopeshwa na Mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa ushauri kuwa, Wizara hii sasa iwahimize wafanyakazi kuwa na tabia ya kufuutilia michango yao katika Mashirika hayo ya Hifadhi, kwani Watanzania wengi wanalamika kuwa fedha hazipelekwi; je, ni wafanyakazi wangapi wana tabia ya kufuutilia kujua kama michango imepelekwa, wahimizwe wawe wanafuutilia michango yao na si kulalamika tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, siungi mkono suala la Makatibu Wakuu kuwa Wajumbe wa Bodi. Wana kazi nyingi hivyo, dhamira ya kutumia *experience* zao haitawezekana, kwani mara nyingi watakuwa wanatumia wasaidizi wao au watu wengine. Watafutwe watu wenye nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kwa Muswada huu. Katika kifungu (5) *Functions and Duties of the Authorities;* 5(d) imesema, *protect and safeguard the interests of members.*

Mfuko ujitalidi sana kuanda malipo ya watu mapema, mara baada ya mkatuba *member* au warithi wake wasitumie gharama nyingi kufuutilia haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mfuko pia huwa unakopesha *members* na watu wengine, ninashauri utaratibu wa kukopesha utoe kipaumbele kwa *members* hata nyumba za kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makatibu Wakuu wa Bodi kwa mfano, *LAPF* wasiwe Wenyeviti wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanachama asiadhibiwe kwa makosa ya mwajiri kutopeleka michango. Muswada au *regulation* itoe *penalty* kwa mwajiri asiyepeleka michango. Aidha, wafanyakazi wa *National Milling Corporation – Iringa*, hadi leo hii wanadai mafao yao na shirika limebinafsishwa bila ya wao kupewa haki zao. Ninaomba Wizara ilizingatie hilo.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono Muswada huu. Mimi ninasema Muswada/Sheria hii imechelewa kuleta Bungeni.

Historia inaonyesha kwamba, Tanzania tumeanza na chombo cha Hifadhi ya Jamii kimoja tu, wakati ule kilifahamika kama *NPF*. Hiki chombo kilikidhi katika Tanzania ya watu milioni nane wa 1961 hadi miaka ya 70 na 80. Lakini kasi ya kuongezeaka kwa Watanzania ni kubwa na ukuaji wa uchumi huafanani sana na kasi hii. Matokeo yake bei zipo juu sana. Mila zinabadilika tena haraka sana. Sasa tuna wazee wasiolelewa na jamii, watoto wa mitaani, walemaru na kadhalika, ambao zamani jamii ilichukua jukumu la kuwalea huko huko vijijiini kwao. Sasa watu hawa wametapaka mitaani na nchi nzima, hasa mijini ambako wengi wao wanaishia kuwa omboomba.

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nayo imeongezeka hadi kufikia zaidi ya mitano, kwa bahati mbaya sana ni kwamba, kila Mfuko una mwelekeo wake tofauti na mwingine. Sera ya Mifuko hii ya mwaka 2003, pamoja na kuzingatia upungufu kadhaa, haikuelezea jinsi gani ya kuidhibiti Mifuko hii. Kwa bahati mbaya kabisa, fedha ambazo zipo kwenye Mifuko hii ni nyingi sana. Hizi ni fedha za umma; bila kuwepo chombo mahususi cha kudhibiti mienendo ya fedha hizi, Mifuko hii haitaweba kutumika katika kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi.

Wakati tunajadili Mifuko hii labda ingekuwa vyema vilevile kuangalia sura mpya ya uchumi katika Tanzania. Katika muda wa miaka kumi iliyopita, kumekuwepo na mabadiliko makubwa ya uchumi. Hii imesababishwa na utekelezaji wa mageuzi ya uchumi katika miaka isiyopungua 20. Kwa juu juu mtu anaweza asione mabadiliko hayo, hasa akipima Mfuko wake na hali ya sasa ilivyo. Lakini mtu akiangalia kwa makini mfumo, vyanzo vya ukuaji wa uchumi, vyanzo vya mauzo ya nje na hasa Sekta ya Fedha, atawea kuona ukuaji huo. Kwa bahati mbaya sana katika miaka kumi iliyopita, mchango wa kilimo umeteremka toka asilimia 30.3 mwaka 1998 hadi asilimia 25.4 mwaka 2006, lakini viwanda na ujenzi mchango wake umeongezeka toka asilimia 16.7 mwaka 1998 hadi asilimia 20.5 mwaka 2006. Pamoja na hivyo, huduma zimeongezeka toka asilimia 45.2 hadi asilimia 46.9.

Jambo kubwa sana lililotoka ni ukuaji wa uchumi ambao ulisababishwa na ukuaji sekta zifuatazo: Madini (asilimia 15.9), ujenzi (asilimia 11.0); huduma za kifedha (asilimia 9.7); viwanda (asilimia 8.2); mawasiliano na uchukuzi (asilimia 8.0).

Kwa madhumuni ya Muswada huu ni vyema kuangalia kwa undani, ukuaji wa Sekta ya Fedha. Kuimarisha kwa mfumo imara wa mabenki na taasisi za fedha, kwa kupitisha sheria mbalimbali za fedha, pamoja na karadha ya pesa, kumewezesha kuanzishwa Taasisi za fedha 34 zenye matawi 338. Hali kadhalika, asasi nyingine za fedha zimeanzishwa. Kufuatana na Benki Kuu, mikopo kwa sekta binafsi imekua kwa asilimia 4.4 hadi kufikia asilimia 13.9 katika Pato la Taifa. Hivyo, kuziachia taasisi hizi za Mifuko ya Jamii ziendelee kuijendesha kama ifanyavyo sasa ni kuudumaza uchumi wa nchi. Kama nilivyosema awali kuwa, hifadhi hizi ni za umma na zinahodhi fedha nyingi sana. Kwa misingi hiyo basi, chombo cha kudhibiti mwenendo na mwelekeo wa kila Mfuko ni muhimu.

Chombo hiki cha kudhibiti na kusimamia vyombo hivyo, kitawajibika kuhakikisha kuwa hifadhi hizi zinasaidia sana kukuza uchumi wa Tanzania. Tutaona sasa Mifuko hii ikiwekeza kwenye miradi ya maendeleo ambayo wananchi wanaweza kufanya; barabara; vivuko na madaraja; viwanda katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ambako vinginevyo visingeweza kuanzishwa; na usambazaji wa umeme kule ambako *TANESCO* wamekwama kifedha.

Kwa namna hii, Mifuko itakuwa na maana sana katika kukua kwa uchumi na chi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Kwanza kabisa, ninaunga mkono asilimia 100 kupitishwa Muswada huu wa Sheria ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008.

Muswada huu tutakapoupitisha na kuwa sheria, itaweza kuleta maendeleo makubwa kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Tunafahamu kuwa Mifuko yetu haiendani na wakati uliopo. Mara nyingi mwanachama anapofikia umri wa kustaafuli, mafao yake huwa hayaridhishi kulingana na wakati.

Utaratibu huu utaleta wigo mkubwa kwa wanachama walio wengi, waajiriwa na wale wa sekta binafsi kuijunga na Mifuko hii. Ni vizuri Mifuko kuwa na uwiano ulio sawa ili wanachama kuweza kuendelea kuwepo ndani ya Mfuko alioanza nao.

Hadi sasa takwimu za wanachama wa Mifuko yetu nchini ni ndogo sana ukilinganisha na wafanyakazi waliopo. Urasimu unaofanyika wakati wanachama wanapofikia kipindi cha kustaafuli kwao ni mkubwa mno; ni vyema mamlaka zitakazoundwa ziweze kulifikiria sana suala hilo ili wanachama waweze kuipenda Mifuko waliyojingga nayo.

Kuongezeka kwa huduma za kunufaisha wanachama ni jambo litakalovutia sana wanachama wa Mifuko; ni vyema chombo kitakachoundwa cha mamlaka ya kusimamia Mifuko kuweza kuweka misingi imara ya kuwanufaisha wanachama kabla ya kufikia wakati wa kustaafuli.

Lazima zifanyike tafiti mbalimbali baada ya kuundwa kwa mamlaka hiyo ili kuweza kufanya mageuzi makubwa ndani ya Mifuko iliyopo nchini, kwa sababu sekta hizi zina fedha nyingi na zitakapotumiwa vyema, zitaweza kuleta maendeleo makubwa nchini kwetu.

Ninaongeza kusema kuwa, suala la kuboresha mafao ya wanachama kabla ya kufikia umri wa kustaafuli ni zuri sana, kwani litapelekea wanachama kujiimarisha na kujiwekeea rasilimali kabla kustaafuli. Lazima mipango mingine iandaliwe katika kumjenga mwanachama; hii itaongeza kuleta wigo mpana kwa wanachama wengine kujitokeza zaidi.

Baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008.

Pamoja na kuunga mkono Muswada, yapo mambo mawili ambayo ingefaa yazingatiwe katika Muswada huu:-

Kwanza, Taasisi za Hifadhi ya Jamii zinatofautiana sana katika mafao ambayo zinatoa kwa wanachama wake. Tofauti hizi zinafanya kuwepo ugumu wa wanachama kuhama kutoka Mfuko mmoja kwenda mwingine. Aidha, hakuelekei kuwapo utaratibu maalum uliowekwa wa kurahisisha kuhama huko. Mamlaka itakayoundwa iliangalie suala hili kwa lengo la kuboresha mafao ya wanachama, kwa kupunguza tofauti zilizopo na pia kurahisisha uhamaji kutoka taasisi moja kwenda nyingine.

Suala la pili, linahusu hifadhi kwa wananchi ambaio sio waajiriwa (*wage earners*), wakiwa ni pamoja na wakulima. Itabidi taasisi husika, ziweke utaratibu utakaowawezesha wakulima kuchangia hifadhi zao baada ya kuvuna mafao yao. Kwa sasa hakuna mpango mkakati wa kuwawezesha wakulima kuiwekeea akiba itakayowasaidia uzeeni, watakapokuwa wamepungukiwa na nguvu za kuzalisha.

Kundi lingine ni lile la watu wanaojajiri wenye kwenye viwanda, biashara za ukubwa mbalimbali, wavuvi na kadhalika, ambaio tofauti na wakulima, hupata mapato nyakati zote, ijapokuwa viwango vinaweza kutofautiana katika vipindi mbalimbali vya mwaka. Mifuko hii inaweza kuweka utaratibu wa kuchangia mafao, ambaio utazingatia upatikanaji wa mapato ya wanachama katika vipindi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Kwanza, ninapenda kuipongeza Wizara hii kwa sheria hii; kuna matatizo mengi yaliyokuwa yanawakumba wananchi hasa wafanyakazi wanapotaka kuhama. Sheria hii ikipita na ufuatiaji uwepo sio kuitisha tu.

Kuhusu Bima ya Afya, wananchi wengi ambaio ni wanachama wao wanapata manyanyaso mengi wakifika hospitali wakiwa wanaumwa. Hawashughulikiwi wanahudumiwa wengine wanaolipa pesa hapo hapo, kwa hiyo, wananchi wengi wanakata tamaa ya kuwa na Bima ya Afya.

Pamoja na sheria hii, vijana hujianzishia ajira zao, matokeo yao wanapata manyanyaso kama Kagera hasa Bukoba Mjini, vijana walianzisha ajira ya baskeli na walikuwa na ajira nzuri tu matokeo yake walikamatwa wakanyng'anywa balskeli zao zimelundikwa polisi. Sasa vijana hao wako mitaani wanazurura, tuliambiwa sheria hii ya baskeli kubeba abiria italetwa Bungeni, mpaka leo haijaletwa, ninaombwa kujuua kuna matatizo gani. Kilio hiki ninakiletaga hapa Bungeni mara kwa mara; ni ajira ya vijana

tena ajira nzuri zipo nyingi tu ila sheria inawabana. Ninaomba nipewe majibu hayo nitashukuru.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Waziri na Naibu wake, kwa kuleta Muswada huu kuhusu Hifadhi ya Jamii. Ninashauri Mfuko wa Bima ya Afya usiwe chini ya chombo hiki, kwa sababu Mfuko huu (*NHIF*) siyo fao ila ni Mfuko unaowahusisha wafanyakazi wachache *specifically*. Kwa suala la afya, Mfuko huu ni wa kitaalam, unaofuatilia huduma ambazo mteja anapatiwa katika sehemu za kutolea huduma na hivyo kusaidia kisera, kuleta dhana nzima ya ubora wa huduma. Tofauti na Mifuko mingine ambayo ina mafao kadhaa na kutumia fedha hizi kupata faida.

Ninashauri Mfuko wa Bima ya Afya ambao unaendeshwa kutokana na Sera ya Afya ya Kuboresha Huduma usiingizwe katika usimamizi wa chombo hiki na badala yake *solely* uwe chini ya uangalizi wa Wizara husika (WAUJ), kwani utendaji wake ni wa kitaalam na unahudumia fao moja tu la afya ya mteja. Ni vyema basi *at the end of the day* ripoti na utendaji wake udhibitiwe na Wizara yenye dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasilisha.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watumishi wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Serikali kwa ujumla, kwa kuleta Muswada huu.

Muswada huu ni muhimu sana kwa kuanzisha chombo cha kusimamia Mifuko hii isiwe ya kitapeli; kushinikiza Mifuko ya Hifadhi iweze kuanza kufikiria kwa ufanisi zaidi katika kuboresha mafao ya wateja wao; na Chombo hiki kikianzishwa ni bora kikaelekeza kila Mfuko uboreshe mafao ya wastaafu na wale waliostaifu zamani, kwani ndiyo waliochangia katika hali nzuri ya Mifuko hii kwa sasa hivyo, hawana budi kufaidi matunda ya michango yao. Vilevile uangalie uwezekano wa hifadhi ya wafiwa na wajane wanapofiya na mlezi wa familia.

Kama si kuelekeza uanzishwaji wa Mfuko Maalum kwa ajili ya hifadhi ya wakulima, basi Mifuko iliyopo iangalie ni kwa namna gani inaweza kuchangia kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Wakulima.

Ninaunga mkono hoja ya Muswada huu, kwa kuwa utakuwa msingi kwa sekta hii ya Hifadhi ya Jamii.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuwafahamisha watu wengi kwa njia ya semina au kuwatemeblea makazini ili waelewe kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Lazima kuwe na elimu ya kutosha, watu wengi wanachanganyikiwa kulipa *NSSF, PPF* na kadhalika; lazima waelezwe tofauti zake. Malalamiko ni mengi kutoka kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, *NSSF* ina vitegauchumi vingi sana hivyo, wakati wa malipo wazingatie kuwalipa wafanyakazi makato yao na riba ya kutosha na walipwe kwa kuzingatia thamani ya pesa kwa wakati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29 kinazungumzia mwajiri kuandikisha wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini hapo hapo mfanyakazi anaweza kuchagua Mfuko anaotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri wafanyakazi ambao ni wanachama wasiombe upya ila wanachama wapya ndio wachague Mfuko wanaohitaji kujiunga. Hili litasaidia watu wasijiunge mara mbili, jambo ambalo linaweza kusababisha utendaji wa kazi wa Mifuko hiyo kuwa nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni kwa jinsi gani chombo hiki kitawezwa kuwasaidia wastaifu wanaopata tabu kupata mafao yao; kwa mfano, mpaka sasa hivi wastaifu wa *East African Community* suala la mafao yao limefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha pili na tatu vinavyozungumzia kuhusu adhabu kwa atakayekiuka masharti ya uanachama; ushauri wangu adhabu ilekezwe moja kwa moja kwa wanachama na siyo kwa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya hasa kutoka kwa walimu; wengi wanakatwa lakini hawapati huduma hii ipasavyo.

Wakifika hospitalini, wakionyesha kadi zao za uanachama, wale wahudumu wanawaambia wakae pembeni kwanza; hii inawavunja moyo sana. Hivyo, kuna umuhimu wa kupeleka *instruments* hasa kwenye Hospitali za Wilaya wawajali hawa walimu, wengine hawaoni umuhimu wa Bima hii.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote, kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka na kuwasilisha kwa ufasaha.

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwepo kwa muda mrefu, lakini ni michache sana ambayo imeweza kuwafaidisha wanachama wao na kuchangia katika uchumi wa taifa letu. Ukiondoa *NSSF*, ambayo matunda yake yameonekana wazi, mingine mingi wala haijaonyesha mafanikio makubwa yaliyotegemewa. Kwa upande mwagine, waajiri wengi hawatimizi masharti ya Mifuko hiyo hasa kwa kutowasilisha makato yao kwenye Mifuko husika. Matokeo yake, Mifuko hiyo inadumaa na kufanya wanachama kukosa mafao yao. Kwa hiyo, sheria hii ikisimamiwa vizuri, wanachama wa Mifuko mbalimbali watafaidika na Mifuko hiyo itachangia katika maendeleo ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza, ninapenda kushauri yafuatayo ili kuboresha zaidi Muswada: Katika kifungu cha 6(2)(d), kati ya maneno “*person*” na

“any” yaingizwe maneno *within its establishment* ili kuondoa dhana kwamba, madaraka hayo yanaweza kukasimiwa kwa mtu yeoyote nje ya mamlaka. Angalia mfano wa kifungu namba kumi.

Mheshimiwa Nasibu Spika, kifungu cha 7(1), ongeza neno “*be*” kati ya “*shall*” na “*composed*.” Kifungu 7(2), Bodi ya watu 13 ni kubwa sana; ninashauri ipunguzwe na iwe na wajumbe kumi, akiwemo Mwenyekiti. Watolewe wafuataao: Katibu Mkuu wa Afya, Naibu Mwanasheria Mkuu na Gavana wa Benki Kuu. Kwa ufupi, michango yao inaweza kupatikana kuitia Makatibu Wakuu watakaobaki.

Bodi hii itakuwa na *Ex-Officials* wengi ambao wana majukumu mengi makubwa. Wasipopunguziwa patakuwa na shida ya kupata akidi kwenye vikao au vikao vitaendeshwa na wawakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri pawe na Katibu wa Bodi, ambaye anawenza akawa wa kudumu au awe Katibu na Mshauri wa Mambo ya Sheria au Mkurugenzi Mkuu atamkwe ndani ya Sheria kuwa ndiye Katibu wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9; kazi za Bodi zimetajwa chache. Ninashauri mpangilio ufuataao:-

- (i) (a) iwemo;
- (ii) (b) iwemo iishie kwenye *recurrent expenditure*;
- (iii) Ongeza (c) mpya “*approve audited accounts*” ndani yake zitakuwemo *Financial Statements* mojawapo ikiwa *Appropriation Statement* ambamo ndani yake zitaonyeshwa *Reserves of the Authority*;
- (iv) Kifungu (c) cha sasa kiwe (d) ;
- (v) Hamisha kifungu 12 kutoka ukurasa wa 12 kiwe (e); na
- (vi) Kifungu (d) kiwe (f) na (e) kiwe (g).

Mheshimiwa Nasibu Spika, katika kifungu 11(3) ongeza vifungu vifuatavyo: (3)(c) *coordinate Authority’s activities*, (3)(d) *advise the Board on policy matters*, (e) *appoint junior staff who are not appointees of the appointment committee*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15 inaelekea kuna pengo; haiwezekanai Bodi iweke muda na viwango vya watu kukagua *register* bila ya kusema kwamba, watu wanaruhusiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo, ninashauri kiingizwe kifungu cha 5(2) kitakachosema, *such a register shall be open for inspection by public (anybody)*. Kifungu cha 15(2) cha sasa kiwe 15(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16(2), hiyo ada itajwe hata kwa kutumia maneno *not less than*. Kifungu cha 16(3) muda wa kushughulikiwa maombi pia uwe na kikomo. Kifungu 20(1)(c), maneno *public interest* yaainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 50(10) kinaleza kuwa hesabu za mamlaka zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; kwa nini asiwe Mkaguzi yeyote anayekubalika?

Mkaguzi Mkuu wa Serikali hukagua hesabu za Serikali, si kawaida kukagua hesabu za Mamlaka na Mashirika; mbona Mamlaka nyingine kama *TP*, Mamlaka ya Kahawa, Tumbaku na kadhalika, hukaguliwa na Wakaguzi wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiingereza; ninaomba Waziri aangalie tena ukurasa wa 33 na yafanyike marekebisho katika ibara za 1, 2, 3, na 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kuleta Muswada huu ambaa ulikuwa unashiribiriwa kwa shauku kubwa na wajasiriamali wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali itoe elimu kwa umma, kuhusiana na Muswada huu ili kila mwananchi au mjasiriamali aelewé kabla ya kuomba mikopo hiyo. Hii itasaidia kupata uelewa katika suala hili la ukopaji wa vifaa vya kutendea kazi au vya kuzalishia (mali), mazao na kuleta tija. Pili, kuwepo na utaratibu mzuri wa kulipa riba ndogo katika mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wenye kuleta unafuu katika kulipa uzingatiwe; malipo yaanze kulipwa baada ya miaka miwili au mitatu ya uzalishaji. Vikundi vidogo vidogo vilivyoko vijijini vielimishwe na kusimamia kwa ufasaha, kwa lengo la kuviwezesha kupata vifaa hivyo na hasa matrekta ya bei nafuu na utaalami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utapunguza vijana wetu kukimbilia mijini; ni muhimu upelekwe vijijini, ndiko kwenye malighafi (mazao).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono Muswada huu muhimu sana kwa uchumi wa wananchi na hasa kwa wananchi/wajasiriamali wetu wadogo wadogo.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri leo asubuhi. Ninapenda nianze kwanza kwa kutamka kwamba, ninaiunga mkono hoja na ningeomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, tuiunge mkono hoja hii ili Muswada huu uwe sheria tuweze kuifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa vile ni mara yangu ya kwanza toka Bunge hili lianzé kusimama hapa kwa kuzungumza, nitumie fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyoendelea kuwa nayo juu yangu, kwa kuendelea kunitua kwa mara nyingine

tena kuwa Naibu Waziri katika Serikali yake aliyoienda hivi karibuni. Ninapenda nimshukuru sana kwa imani aliyoionyesha juu yangu na ninaahidi kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu aliyonipa kwa uwezo wangu wote na kadri Mwenyezi Mungu atakavyonielekeza na kunijalia. (*Makofî*)

Ninamshukuru pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda kwa uongozi na maelekezo yake ya mara kwa mara, yanayotusaidia sana katika utekelezaji wa shughuli za Wizara. Pia ninapenda nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Professa Juma Kapuya, kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika shughuli za Uongozi wa Wizara. Baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba nijielekeze kuchangia hoja ya Muswada huu kwa kutoa maelezo machache ya ufanuzi kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii hapo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa ujumla wake, ninapenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliopata nafasi ya kuchangia hoja yetu hii kwa kusema, pamoa na kuandika. Ninatambua wazi kabisa, mtoa hoja atakapokuja hapa atawatambua kwa majina, lakini mimi kwa ujumla wake tu ninapenda niwashukuru kwa sababu wengi wao waliunga mkono hoja hii, ukiacha ndugu yetu mmoja Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye alionyesha wasiwasi. Kwa kweli na sisi tulishangaa kidogo kwa sababu Msemaji huyo wa Upinzani ni Mjumbe wa Kamati na tumekuwa naye, hayo aliyoyleza pengine aliona iwe hivyo, lakini wengine wote ninapenda niwashukuru sana kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa, lakini moja la jumla ambalo ningependa nilisemee hapa ni hili suala la Mfuko wa Bima ya Afya, ambalo limesemewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na hasa nitambue mchango wa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Naibu Waziri wa Afya, pamoa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, ambao walionyesha wasi wasi kusema kwamba, pengine katika sheria hii, Mfuko wa Bima ya Afya usingweza kuhusishwa kwa sababu Mfuko huu una majukumu mahususi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hata katika maelezo ya utangulizi ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa Waziri leo asubuhi yalieleza hivyo hivyo kwamba, Mfuko wa Bima ya Afya ni maalum kwa sababu unatoa fao moja tu la ile Bima ya Afya. Kwa hiyo, angalizo tulilokuwa tumelielekeza kwenye sheria na hata katika *schedule of amendment* ambayo tumeitoa kwenye kifungu kile cha 36, imeelezwa wazi kabisa kwamba, masuala yote yanayohusiana na Mfuko wa Bima ya Afya, yatasimamiwa kiutaalamu na Waziri wa Afya isipokuwa tu inapokuja katika masuala yale ya uwekezaji, maana yake mifuko yote hii inakusanya fedha ambazo inafika zinakwenda kwenye uwekezaji. Ni katika kipengele hicho tu ambacho Sheria hii imesema kwamba, itakapokuwa imefika wakati wa kujielekeza katika uwekezaji, hapo ndiyo suala la huyu *regulator* atatoa miongozo ambayo itakuwa inaelekeza utaratibu mzima wa uwekezaji. Ni katika suala hilo tu, lakini kimsingi utendaji wa kazi wa shughuli zote za ule Mfuko wa Bima ya Afya, zitaendelea kuwajibika kwa Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameli semea ilikuwa ni kuhusiana na Mifuko yenyewe yote hii kwa ujumla. Waheshimiwa Wabunge, walizungumzia kwamba, Mifuko hii kwa sasa hivi inasimamiwa na Wizara mbalimbali. *NSSF* inasimamiwa na Wizara yetu ya Kazi, *PPF* inasimamiwa na Wizara ya Fedha, ule Mfuko wa Serikali vilevile Wizara ya Fedha na *LAPF* inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (*TAMISEMI*). Hata hilo limetambuliwa hata kwenye sera ambayo imetuelekeza kuandaa Muswada huu, lakini sheria hii ambayo tutaipitisha hapa itakuwa sheria, kuna kipengele ambacho kimeelekeza kwamba, sheria zilizounda Mifuko hii ambayo sasa hivi inasimamiwa katika maeneo mbalimbali, nazo itabidi zianze kurekebishwa taratibu kuhakikisha kwamba, zinajiweka katika usimamizi ambao utakuwa ni bora zaidi. Kwa hiyo, sheria hii itakapopitishwa, itakuwa ndio mwanzo wa kufanya marekebisho kadha wa kadhaa ambayo itatufikisha sote tunakotarajia kwenda.

Kwa hiyo, kwa kweli sheria hii inakuwa kama ni ufunguo. Kama ambavyo sote tunafahamu kwamba, chimbuko la sheria hii ni sera ambayo ilionyesha kwamba upo upungufu ambao hauunganishi utekelezaji wa shughuli za mifuko hii. Sababu ya kutungwa hii sheria ya *regulator* ambayo kazi yake itakuwa kusimamia na kuratibu Mifuko hii. Waziri mhusika pia ataweka taratibu za uendeshaji wa shughuli na taratibu hizo nina imani kabisa zitasaidia kuhakikisha kwamba, uendeshaji wa Mifuko hii unakwenda vizuri na unapangwa kwa utaratibu ambao utazingatia Sera na Sheria nyingine zitakazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wametaja upungufu wa utekelezaji katika Mifuko hii. Lilikuwepo moja ambalo lilijitokeza waziwazi kwamba, wakati mwingine inapofika wakati wa kustaa fu, baadhi ya waajiri wanakuwa hawajawasilisha michango ya wafanyakazi katika Mifuko inayohusika na kwa hiyo, ukifika wakati wastaafu wamemaliza muda wao, upatikanaji wa mafao yao unakuwa wa shida kwa sababu fedha zile zinakuwa hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili tumesema kwamba, kazi mojawapo ya *regulator* itakuwa ni kuelekeza utekelezaji wa wale wote watakaokuwa wanahuksika kwa namna moja au nyingine kuhakikisha kwamba, Mifuko hii haiathiriki kiasi cha kuhakikisha kwamba, wafanyakazi wanapata athari wakati watakapokuwa wanafuatilia mafao yao. Vilevile hata sheria zile za Mifuko yenyewe ambayo inatoa mafao kwa wafanyakazi, nayo inajielekeza hivyo hivyo kuhakikisha kwamba, wafanyakazi wasiweze kupata matatizo wakati wanastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge, ninaona hapa mchango wa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, pamoja na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa; wamejaribu kuulizia Mifuko hii inasaidiaje maeneo ya pembezoni katika uwekezaji. Kwa mfano, ujenzi wa majengo mbalimbali yanayojengwa kama kitegauchumi katika maeneo mbalimbali. Katika hili ndiyo sababu ya kumuweka huyu *regulator* au msimamizi. Kazi mojawapo ya msimamizi kwa kutumia Benki Kuu itakuwa ni kuhakikisha kwamba, uwekezaji unaelekezwa kutegemeana na mahitaji ya nchi badala tu ya kuwekeza kwa kadri Mfuko utakavyokuwa

unafikiria. Kwa hiyo, itafika mahali mathalani kama uwekezaji utakuwa unahitaji kujielekeza katika Sekta ya Miundombinu kwa mfano, itakuwa ni kazi ya huyu mtoaji wa *guidelines* kuhakikisha kwamba, *guidelines* hizo zinawaelekeza wenyewe Mifuko katika uwekezaji katika eneo hilo la miundombinu. Hali kadhalika, katika uwiano wa maendeleo inawezekana kabisa kwamba, Mifuko hii ikapewa mwongozo wa kuhakikisha kwamba, inawekeza katika maeneo ambayo maendeleo yake yako nyuma kuhakikisha kwamba uwiano wa maendeleo unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho ningependa nijielekeze nacho ni kile kilichozungumzia suala la mikopo kwa Mifuko hii kwa wanachama wake kutoa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Kilichoelezwa kwenye sheria ni kwamba, endapo mikopo hii itakuwa inatoka katika ule Mfuko wa jumla amba o umekusudiwa kutoa mafao, Mifuko hii itaathirika. Kwa hiyo, tulichopendekeza katika sheria ni kwamba izingatiwe kuwekwa asilimia nyingine pembedi ambayo itakuwa inakusudia utoaji wa mafao ambayo itahakikisha kwamba, mikopo hiyo itakapokuwa inatolewa kuwasaidia wale wanachama waweze kujenga nyumba, pamoja na mahitaji mengine bila kuathiri Mifuko yenyewe.

Kwa hiyo, hilo limezingatiwa kwenye sheria na nina hakika sheria ikipita na ikatekelezwa vizuri, Mifuko yetu itaendelea kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliona nijielekeze katika yale ya jumla ambayo yalikuwa yanazungumzia habari ya Mifuko, lakini nina imani kabisa kwamba, Mheshimiwa mto hoja, atajielekeza moja kwa moja katika vipengele mahususi ambavyo vilikuwa vimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyokuwa nimesema mwanzo kwamba, ningeomba tuiunge mkono hoja hii ili sheria hii itakapoanza kufanya kazi, yale mengine yote ambayo tuna mashaka nayo, kusema kweli tutakuwa tumepata mahali pa kuanzia, kwa sababu itakuwa ndiyo kioo na ndiyo mwongozo wa kutusaidia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuongoza Mifuko yetu, pamoja na hifadhi ya jamii ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ambazo wamezitoa ili kuboresha Muswada huu ambao tuna matumaini makubwa kwamba, baada ya hoja hizi sasa hatimaye itakuwa sheria.

Ninaomba kwanza, nishukuru michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wao, nikianza na shukrani za pekee kwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Makamu Mwenyekiti alivyowasilisha leo. Mawazo yao yanaendelea kutusaidia na tutaendelea kuyazingatia. Vilevile ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kuwasilisha mawazo

mazuri ambayo nina hakika kwamba, baada ya kupata maelezo yetu, ninadhani ataridhika na kuwa nasi na kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuwatambua waliochangia kwa maandishi. Ninaanza na Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya na Mheshimiwa Aziza S. Ally. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopata nafasi ya kuchangia kwa mdomo ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan - Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Ninawashukuruni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokuwa wakati wa Kamati tulipokuwa tukijadili na hatimaye kufikisha kwenye semina na leo katika Bunge, imeonekana kwamba, kulikuwa kuna upungufu mkubwa katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Waheshimiwa Wabunge, pia wameendelea kuashiria hivyo. Ninataka niseme kwa sababu ya upungufu huo, ndiyo maana tukaja na sera na ndiyo maana tukaja na sheria hii. Kama tulivyosema, sheria hii kwa sasa hivi inachokwenda kufanya ni kusimamia na kudhibiti sekta hii ili kuhakikisha kwamba, kule kama kunataka kujitokeza fujo za aina nyingine zozote sasa zitatuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, zinazoashiria mambo ambayo tulikuwa tukiyaona kama upungufu. Kwa mfano, Kambi ya Upinzani inasema; kutokutenganishwa kwa Mifuko ya Fedha za Jamii na Umma na ile ya binafsi tayari kuna ukinzani. Hii ya sasa tayari ipo, ile mingine ndiyo tunafikiria kuiunda. Anasema tayari kuna ukinzani, kwa sababu hii mamlaka itakapoanzishwa, kabla haijaanzishwa Mifuko hiyo ya binafsi, Mkurugenzi Mkuu anachopaswa kufanya kwanza ni kufanya utafiti kamili, halafu aweke mazingira mazuri ndiyo aruhusu uanzishwaji. Vilevile Waziri mhusika wa Hifadhi ya Sekta ya Jamii atakapoweka kanuni, atazingatia kwamba, yanawekwa mazingira mazuri ili hii Mifuko mingine (*Private Pension Schemes*), zinakapokuja kuanza, zianze katika mazingira ambayo hayakinzani. Sasa unapoanza kuashiria kwamba kuna ukinzani kabla hata haijaanza, mimi kidogo inanipa wasi wasi. Lakini Mheshimiwa Mbunge tulikuwa

naye hata kwenye Kamati alichangia na akaelewa. Sasa nina hakika kwamba, alikitia tena hizo *notes* zake alizokuwa nazo, atalielewa suala hili.

Kifungu 39 cha Muswada kinampa Mkurugenzi Mkuu mamlaka kutengua ajira ya Watendaji Wakuu wa Mifuko ya Umma wakati watendaji hao ni wateule wa Mheshimiwa Rais. Kifungu hiki kinazungumzia hatua za kuchukuliwa pale Mifuko ya Wakala au Waangalizi wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao, hakihusiki na suala la utenguzi wa ajira za Watendaji Wakuu wa Mifuko ya Umma kama ilivyokuwa inaulizwa katika swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri yupi mwenye dhamana na hifadhi ya jamii kwa mujibu wa Muswada huu kifungu namba tatu; ninadhani hili tumelizungumza katika Kamati lakini vilevile katika *schedule of amendments* tulizoleta, limezungumzwa wazi kabisa kwamba, kutokana na hali halisi ilivyo, Waziri mwenye dhamana ya hifadhi ya jamii kwa maana ya Muswada huu ni Waziri wa Kazi. Ili kuondoa ule utata kwamba inapofika kwa mfano, kupendekeza Bodi kwa Mheshimiwa Rais sasa kila mtu ataanza kusema labda Waziri wa Afya, labda Waziri wa Kazi na kadhalika. Kwa hiyo, kwa maana ya kuratibu yaliyotokana na Muswada huu ili kumwezesha yule Mtendaji Mkuu kuwa na uwezo wa kwenda bila kusimama, basi imetolewa tafsiri kabisa kwamba, Waziri mwenye dhamana ya hifadhi ya jamii kwa hapa ni Waziri wa Kazi.

Neno chini ya kifungu cha 9(c), linaweza kusababishwa kuvunjika kwa maadili. Kanuni zilizoandaliwa chini ya sheria hii kupitia kifungu cha 52(2)(e), kitaweka utaratibu utakaotumika kupokea zawadi pasipokuvunja maadili ya Utawala Bora ikiwa ni pamoja na suala la upendeleo. Vilevile ninachotaka kusema, kwa sababu Bodi ndiyo inayopokea, ninashangaa Bodi hii ambayo inapokea iweze kutoa upendeleo kwa Mfuko fulani ili hasa iweje? Kwa sababu Bodi hii ndiyo inapaswa ku-*regulate* Mifuko yote, lakini kama tunavyosema, kanuni itatambua tatizo hili na itaweka misingi imara.

Kifungu namba 20 cha Muswada, kinaipa madaraka kufuta usajili wa Mfuko lakini Mifuko ya Umma imeanzhishwa kwa Sheria za Bunge hivyo, kama mamlaka itakuwa na uwezo wa kufuta Mifuko hiyo ya kuwa hata Sheria za Bunge za Uanzishwaji Mifuko ile itakuwa imefutwa. Je, mamlaka inayoundwa itaweza kuchukua kazi ya Bunge ya kutunga au kufuta sheria, hapana; mamlaka kamwe haiwezi kuchukua mamlaka ya Bunge ya kutunga sheria. Ila kama tulivyosema, sheria ikipita; zile sheria zilizounda Mifuko mingine, ambazo zinaonekana kama vilehaziendani na sheria, itabidi zibadilishwe na atakayezibadilisha si mwininge bali ni Bunge hili hili. Kwa hiyo, sisi tutaleta mapendekezo na Wizara mbalimbali zitaleta mapendekezo kwa maana ya *amendments* na ninyi mkiridhia ndio sheria zitabadilika. Haiwezekani mamlaka hii inayoundwa, kujinyakulia madaraka ya kutunga sheria na kuanza kufuta sheria, hiyo haipo ninawahakikishieni.

Kifungu namba 23(5) kikisomwa kwa pamoja na kifungu 25(1), inaonekana kuleta mkinzano, Serikali iweke wazi na kifungu kipi kitatumika katika hivyo viwili. Kifungu namba 25(5) kinazungumzia *reserve accounts* kwa ajili ya utunzaji wa fedha zisizokuwa na matumizi kwa wakati ule. Kifungu namba 25(1) kinazungumzia matumizi

ya fedha hizo na kwa misingi hiyo, vifungu hivi havina mkinzano na vyovyyote viwili vinapaswa kutumika. Kimoja kinazungumzia utunzaji na kingine kinazungumzia matumizi kwa hiyo, *definetly* hivi viwili havina mkinzano wa aina yoyote.

Kifungu namba 29 kinazungumzia wigo wa wanachama kwa kila mwajiri katika sekta rasmi ya ajira kujiunga na Mfuko wowote ambaو umeanzishwa kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, zipo sheria zinazoelekeza kila mwajiri anatakiwa ajiunge na Mfuko gani. Tumezungumzia jinsi ambavyo sheria itabidi ziweze kuwiana na sheria mpya. Vilevile si kwamba tutaruhusu au hii mamlaka itaruhusu kwamba na wale ambaو tayari wapo katika Mifuko, wachague upya, hapana. Tunachozungumzia hapa ni wale waajiri wapya ambaو ndio wanaanza kuajiri wafanyakazi wapya ili kuondoa ile sokomoko. Kwa sababu ukifanya hivyo ni dhahiri Mifuko mingine inaweza ikadondoka siku inayofuata. Vilevile tukumbuke kwamba, kuna baadhi ya Mifuko ina jukumu mahususi kama Mfuko wa Bima ya Afya. Hilo nalo haliruhusiwi, lazima izingatiwe katika mazingira yatakayowekwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hii.

Neno “*may*” kama liliwyotumika katika kifungu cha 38 hakiipi Mamlaka, ulazima wa kutosha kufanya ukaguzi hivyo inashauriwa neno “*shall*” litumike badala yake, pendekezo limezingatiwa katika jedwali la marekebisho. Kifungu namba 41 kinachohusu uanzishwaji wa Baraza la Rufaa la Hifadhi ya Jamii litakalokuwa na mamlaka kusikiliza rufaa zote dhidi ya maamuzi ya mamlaka. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Baraza hilo halina ulazima na badala yake Mahakama ya Kazi iimarishe ili iweze kufanya kazi ambazo zimefanya na Baraza la Rufaa. Jukumu la Baraza la Rufaa la Hifadhi ya Jamii litakuwa ni kushughulikia rufaa zote kabla ya kuwasilishwa katika vyombo vyaa juu. Lengo la utaratibu unaopendekezwa; kuongeza kasi katika kushughulikia rufaa zinazohusiana na masuala ya hifadhi ya jamii kabla ya kupelekwa Mahakamani. Tukiruhusu kila kitu kiende Mahakamani, kule Mahakamani kutatokea mlundikano wa kesi. Kwa hiyo, ile kasi ya kuweza kutatua migogoro hii haitakuwa rahisi. Kwa hiyo, tukaona tuwe na chombo cha kati, kazi yake itakuwa ni kuyachuja yale ambayo yanaonekana kweli yaende Mahakamani, yaende Mahakamani. Kwa hiyo, ninataka nikuhakikishie kwamba, suala la Mahakama hatujalifuta lipo pale pale.

Sasa ninakuja kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Victor Mwambalaswa anaunga mkono, Mifuko ya Pensheni kusaidia wanachama kuboresha maisha. Hilo ni kweli jinsi ambavyo wanajaribu kuwekeza katika vitegauchumi na kwa hiyo wanapokuja kustaa fu wanakuwa wanapata si michango yao tu bali na nyongeza mbalimbali ambazo zimetokana na vitegauchumi hivi.

Mheshimiwa Guido Sigonda, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini isaidie wananchi vijijini kama vile, Mfuko wa *TASAF*, Programu za *MMEM* na kadhalika. Ninadhani ipo haja ya kutofautisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na yale ambayo yanafanya na hii Mifuko ya Jamii mingine ambayo ipo katika kundi la *social assistance*. Hii Mifuko ya Jamii ya hivi sasa ni lazima iingie katika masuala ya kutunza mahesabu, kuhakikisha inatengeneza faida ili waweze kuhakikisha kwamba, wanachama wao wanapata maslahi bora. Tukiisukuma kutoka katika ngazi ya pili ya hifadhi ya jamii, tukaisukuma katika ngazi ya kwanza ambayo ni *social assistance*, kuilazimisha mifuko hii nayo iwe inatoa

*social assistance*, tutakuwa tumeipa hasara ambayo baadaye wanachama wake watakuja kulalamika na utakuta Mifuko hii inaporomoka.

Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, sekta isiyo rasmi kwa dhamana ya hiyo mifugo, mashamba ya kuchangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kutunzwa na mifuko zisambae hadi vijijini, elimu itolewe ili wananchi walio wengi wafaidike. Kama nilivyozungumza wakati ninatoa maelezo wakati ninazungumzia kusomwa kwa mara ya pili kwa Muswada huu; lengo ni kupanua wigo na hayo ndiyo maeneo ambayo tumekusudia, ndiyo maana tunaunda mamlaka ili mamlaka hii sasa ijielekeze katika maeneo haya. Haya masuala hatuwezi tukaamua kwa maagizo.

Mkurugenzi Mkuu huyu na mamlaka hii lazima ifanye utafiti wa kutosha na maandalizi ya kutosha. Kwa sababu ukienda bila ya kujiandaa sawa sawa kwa maeneo yaliyo tete kama haya ni hatari sana, unaweza kujikuta unakula hasara kubwa na Serikali yenu ikabeba mzigo, kwa sababu mdhamini wa mambo yote haya ni Serikali. Mambo yakienda ovyo, Serikali lazima iingilie ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao.

Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, elimu itolewe juu ya malalamiko yanayotoka kwa wafanyakazi kuhusu Mifuko iliyopo hivi sasa, yaani *NSSF, PSPF, LAPF* na *GEPF*. Ni kweli elimu lazima tutaendelea kuitoa na hili halina mjadala.

Mheshimiwa Abdallah Khamis ni vizuri kwa Mifuko kuwa na uwiano ulio sawa, wanachama ni wachache na Mifuko iwe ni ya kuchochea maendeleo. Hii kama tulivyozungumza kwamba ni kweli baada ya mamlaka kuundwa kwa uhusiano utakaokuwepo kati ya mamlaka hii na Benki Kuu sasa mifuko hii itakuwa inapata maelekezo ya uwekezaji na udhibiti wa maamuzi ya uwekezaji kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Kwa sababu tunaamini Benki Kuu ya Tanzania ndiyo inayojua, uchumi huu unapaswa uende vipi na kwa kasi ipi. Utakuwa unatoa maelekezo sahihi ili kuwezesha Mifuko hii sasa kwa pamoja kuweza kujiingiza katika masuala haya muhimu ya uwekezaji kama uwekezaji katika miundombinu, uwekezaji katika viwanda na kadhalika, hilo tumelizingatia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, umuhimu wa kuongeza wigo tumeshazungumza. Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mashirika na Taasisi kutowasilisha michango ya wanachama wake katika Mifuko. Hili Naibu Waziri ameshalizungumza kwa kirefu.

Mheshimiwa Bujiku Sakila, Muswada huu ni muhimu sana. Uanzishwaji wa mifumo maalum kwa wakulima; litazamwe jinsi gani Mifuko inaweza kuwafikia wakulima. Amezungumzia hili Mheshimiwa Sakila kwamba, tunahitaji kufanya maandalizi na utafiti wa kutosha, kazi ambayo itafanywa hivi sasa na mamlaka hii tunayoienda kama sheria itakuwa imepita.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Sera ya mwaka 2003 haikuelezea jinsi ya kudhibiti Mifuko hii. Hizi ni fedha za umma, bila ya kuwepo na chombo mahususi cha udhibiti wa mienendo nje ya fedha, haitaweza kutumika katika kukuza na kuimarisha uchumi. Ukiisoma sera ambayo ndiyo chanzo hasa cha sheria hii, imefafanua wazi wazi upungufu uliomo. Kwanza, kutakuwepo na uwiano wa Mifuko. Pili, uwekezaji kusimamiwa; kila Mfuko una sera yake ya uwekezaji. Sasa haiwezekani ukawa na Mfuko; kila Mfuko unaundwa una mwelekeo wake, ndiyo maana tunatengeneza sheria hii ili tuone mamlaka, ili kwa kusaidiana na Benki Kuu, tupate miongozo sasa wawekezaji wawe *guided*. Kwa hiyo, sera imezingatiwa katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Castor Ligallama, faida inayotokana na uwekezaji wa Mifuko itumike kuboresha mafao ya wanachama; hiyo ninadhani Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalizungumza. Mifuko isimamie hayo yote Mheshimiwa Naibu Waziri amekwisha yazungumzia.

Mheshimiwa Athumani Janguo anasema, Mifuko haijaonyesha mafanikio makubwa yaliyotegemewa; Sheria itakayoundwa italenga kuondoa upungufu uliopo kwa sasa. Ninashukuru kwa maoni yake hayo, ila asilimia ambayo tumeshafikia katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii sio mbili ni asilimia 5.4. Kwa hiyo, tunesonga mbele kidogo lakini si sana, bado Watanzania karibu asilimia 94 hawajafikiwa na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mkanga ukurasa wa kumi, vipengele saba vinafafanua Bodi ya Mamlaka itakayoundwa izingatie jinsia. Mheshimiwa Margreth Mkanga, kwa sababu Bodi hii hasa hasa itajikita katika utaalalm wa suala zito kama hifadhi ya jamii, tunategemea Mamlaka za Uajili na Mamlaka za uundaji wa Bodi zitazingatia hili. Tukiliweka moja kwa moja tunahofu kwamba, inawezekana ukawabana wanawake wenye uwezo au wanaume wenye uwezo. Ninataka nikuhakikishie kwa mfano hivi sasa kama Sheria hii itapita, kwa maana ya Msajili wa Hazina awe ni Mkurugenzi katika Bodi hii na Kamishna awe ni Mkurugenzi katika Bodi hii, Kamishna tunaye mwanamke na Msajili wa Hazina ni mwanamke; kwa hiyo, tayari wanawake wapo. Wanaingia pale si kwa sababu ni wanawake, wanaingia kwa sababu wanaweza na wanajua taaluma hizi na kwa sasa hivi hakuna anayeunda Bodi akaacha kufikiria wanawake. Kwanza, lazima afikirie akishahakikisha kabisa kwamba hapatikani na hana la kufanya, ndipo ambapo anaweza kuweka wanaume watupu. Ninataka nikuhakikishie kwamba, kwa sasa hivi kwa jinsi ambavyo tumehamasika hilo ninakuhakikisha kwamba, litazingatiwa. (*Makofii*)

Ninaomba ufanuzi endapo mwanachama wa Mfuko wowote akipata kazi nchi nyingine mafao yatachambuliwaje; hii kama tulivyozungumza, kuhamisha kwa mafao hasa Mfuko hadi Mfuko bado ni kazi ngumu, hatujapata *formula*. Kwa sababu ukizungumza na watu wa Mifuko hii wanakwambia kuna kitu kinaitwa *defined benefits* na *defined contribution*. Sasa hii wanazungumza wao ni *defined benefits*; huwezi ukasimama katikati ukasema hebu nipigie hesabu hivi mali yangu ni kiasi gani mpaka utakapokuja kustaafu miaka yako sitini ndipo zinapigwa hesabu. Ndiyo maana inakuwa vigumu sana kumhamisha mtu kutoka *NSSF* kwenda *PPF and vice versa*. Kwa sababu utakapomhamisha hajui ni kiasi gani abebe kutoka Mfuko anaotoka kupeleka katika Mfuko anaoingia au afidiane vipi Mifuko hii. Sasa tunaipa nafasi mamlaka, tumeliweka

kama tatizo achunguze namna ambavyo inaweza ikatekelezeka kwa namna moja au nyingine, lakini ni kitu ambacho kinapaswa kwenda kwa uangalifu sana.

Mheshimiwa Savelina Mwijage; Bima ya Afya ya wanachama wanaopata manyanyaso wanapofika hospitalini wakiwa wanaumwa, wanaopata huduma haraka ni wale wenye fedha halali. Mheshimiwa Waziri yupo hapa analisikia na mimi nina hakika atalifanya kazi. Sasa kuna suala la baiskeli ndiyo sijalielewa sawasawa; anasema kuna vijana pale wamejajiri wanabeba abiria kwenye baiskeli wanapata manyanyaso. Sasa sina hakika inahusianaje na hii hifadhi ya jamii hapa, lakini kama nilivyosema ni kwamba, tulikuwa na taratibu za kutaka kuunda Sheria ya kuwaruhusu wale wanaobeba abiria kwa baiskeli na pikipiki waruhusiwe. Ninadhani tukisubiri mchakato ule ukamilike, itakuwa *ime-take care* hilo suala.

Mheshimiwa Charles Keenja, mafao ya Mifuko iliyopo sasa ni tofauti na imekuwa kikwazo. Hilo ninadhani Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu. Mheshimiwa Clemence B. Lyamba; utekelezaji wa Sheria hii uharakishwe ili uboreshwaji wa mafao ya wastaafu uharakishwe na kuboresha Ilani ya Chama cha Mapinduzi; pendekeso limezingatiwa. Mamlaka ya kusimamia hifadhi ya jamii iwekwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha; Mamlaka hii inawahusu wafanyakazi na akiba yao kwa maisha yao hivyo ninaona itakuwa vyema zaidi iwe chini ya Wizara ya Kazi inayohusu wafanyakazi. Hata hizi fedha zenyewe Waheshimiwa Wabunge, tutofautishe fedha kwa maana ya zinazokwenda katika Benki na zinazokwenda katika Mifuko hii ya hifadhi ya jamii ina sura mbili; ina sura ya fedha lakini zaidi inatakiwa iwe na sura ya hifadhi.

Sasa hata katika zile kanuni za uwekezaji, utakuta wanatofautiana vilevile kwa maana ya fedha kama fedha, kama ni benki kwa mfano, wao wanachoangalia ni faida tu, lakini katika Mifuko wanachoangalia ni faida lakini vilevile na usalama wa fedha za wanachama wao. Kwa hiyo, malengo kidogo yapo tofauti kwa hiyo, tusiipachike sana tukadhani hii fedha nayo ni sawasawa na benki nyingine yoyote.

Mifuko ibuni utaratibu wa wastaa fu kupata pensheni zao bila usumbufu wakati wa kufuutilia kwa muda mrefu; hili limeshaanza kushughulikiwa kwa muda mrefu sana lakini ni changamoto ambayo tunasema kuboresha hakuna kikomo tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Pindi Chana amesema, malipo ya mafao yasicheleweshwe kwani wanachama wanatumia gharama nyingi kufuutilia haki zao. Hili tunalichukua kama changamoto nyingine, tutaendelea kulishughulikia.

Mheshimiwa Meryce Emmanuel anasema Mfuko wa Bima ya Afya hauna maana wala hauwatendei haki wanachama wake na hali hii inatokana na ukweli kwamba, wanaopata huduma ya kwanza ni wale wenye fedha mkononi na wakati mwingine wanachama wanakwenda kununua dawa na hali wanakatwa katika mishahara yao. Ninashauri Sheria ipitiwe upya, uwepo utaratibu mzuri. Hili ninaomba niunganishe na mchangano wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally anasema, Mfuko wa Bima ya Afya wakipelekewa zile risiti ambazo wanasema wamenunua dawa wakati mwingine watu wanaandikiwa dawa hewa. Sasa ninadhani Mheshimiwa Waziri wa Afya amelisikia

atalichukua na kwenda kulifanyia kazi. Si malalamiko ambayo tunayapuuza kama Serikali, kwa sababu hata sisi ndugu zetu wanaathirika. Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie kwamba, Serikali itakuwa makini kuwahakikishia kwamba, upungufu katika Mfuko wa Bima ya Afya unafanyiwa kazi ya kutosha na matunda yapatikane.

Mheshimiwa Athumani Janguo; marekebisho ya vifungu ili Sheria imtaje Katibu wa Bodi. Sasa ukiangalia kifungu namba nane kinaleza uteuzi wa Mwanasheria wa Mamlaka ambaye vilevile haiishi tu kuwa Mwanasheria wa Mamlaka, vilevile anakuwa ni *Secretary to the Board*. Kwa hiyo, ndiyo maana tulipokuwa tuktaja Wajumbe wa Bodi watakaoteuliwa kwa maana ya mamlaka za uteuzi wa Bodi, hatukumtaja pale. Kama vile ambavyo hatukumtaja Mwenyekiti kwa sababu tunajua atateuliwa na Mheshimiwa Rais, baada ya mapendekezo ya kutoka kwa Waziri. Kwa hiyo, *Board Secretary* yupo. Kifungu namba tisa kuhusu kazi ya Mkurugenzi wa Mamlaka, mawazo yake ni mazuri na yamezingatiwa ndani ya vifungu vya Sheria hii.

Kifungu cha 15 kutoa nafasi ya mtu kukagua *register*. Kifungu cha 51(2) kinatoa haki ya ukaguzi baada ya kulipa ada iliyowekwa na Bodi. Kutozwa kwa ada na ukomo wa muda ndani ya Sheria. Mambo haya yatazingatiwa wakati wa kutunga kanuni. Wakaguzi wa Mahesabu kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali; Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndiye mwenye Mamlaka ya kuteua Mkaguzi maeneo yanayohusiana na fedha za umma. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, hata ukiangalia Mamlaka nyingine zote zilizoundwa, iwe ni *EWURA* iwe ni *TICRA* kwa sababu ni *Public Institution, then mwenye dhamana ya kukagua pale ni Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. Ndivyo wanavyofanya kwenye mamlaka hizo na kwa sababu nayo hii inakuja kuwa ni Mamlaka, kwa hiyo, ile *Public Finance Act* ina-*apply* hata kama tusingesema hapa hii Sheria inge-*apply*. Kwa hiyo, hakuna kipyä ambacho tumekifanya.

Mheshimiwa Ameir Ali Ameir; Mifuko haina budi kujitangaza kwenye vyombo vya habari ili Watanzania wafahamu Mifuko hii pamoja na faida zake. Suala la kutoa elimu limezingatiwa katika Sheria inayotungwa, Mifuko hii inakusanya michango ya wafanyakazi na inawekeza kujipatia faida ili kuboresha mafao ya wafanyakazi.

Serikali kufuta kabisa kodi kwa Mifuko; sasa haya ni masuala ambayo yanahitaji mazungumzo makubwa ndani ya Serikali. Kufutwa kodi si suala ambalo linawenza likaamuliwa haraka haraka, kwa sababu unapofuta kodi athari zake lazima ujiandae kuongeza kodi mahali pengine. Sasa ninadhani hili tulichukue kama wazo zuri, ambalo Serikali italiangalia na kuona kama itawezekana. Je, ni fedha kiasi gani ambazo zimekatwa kutoka kwenye mishahara ya watumishi, lakini hazijapelekwa kwenye Mifuko na ni hatua gani zimechukuliwa na wahusika. Hili si lingekuja kama swali, likija kama swali sisi tutalijibu, lakini kulileta katika mchango hapa sasa hivi si rahisi swali hili kujibiwa pengine; tutapata majibu mazuri baada ya kuwasiliana na Mifuko husika. Kwa hiyo, kama likija kama swali ninakuhakikishia tutalijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga amesema, maneno ya jedwali yaondolewe kwa sababu hayana maana, kifungu hiki ni muhimu kiwepo ndani ya sheria hii mpya kama kinavyotumika katika Sheria za Mifuko. Kwa kuwa Sheria hii ni

mpya, kifungu hiki kinatoa msingi kwa sheria hii inayosimamia na kudhibiti sekta hii. Hicho ni kifungu namba 24(5), kinachomaanisha hapa ni ile *reserve* yenyewe. Tunachotaka kusema ni kwamba, katika Mifuko hii ambayo tayari ipo, ina utaratibu wake, lakini ipo Mifuko ambayo itaanzishwa sasa ni vyema wakajua kwamba wanahitaji kuwa na *fund reserve somewhere* ili waweze *ku-operate* sawasawa. Vinginevyo, tutakuwa tunaanzisha Mifuko mingi ya utapeli kama ilivyokuwa na kuna Mbunge ameshauri hapa kwamba tujiepusha na zoezi ambalo lilishafanyika kule Uingeleza kwa Bwana mmoja anaitwa Maxwell; alianzisha Mfuko halafu baadae akatoweka akaingia mitini. Sasa ndiyo maana tunaweka kipengele hiki ili kuhakikisha kwamba, tunakuwa na *gurantee* ya Mfuko wenyeve kabla *gurantee* ya Serikali hajingia.

Kifungu namba 36 kinahusu matumizi ya sehemu ya mafao kama dhamana kwa ajili ya nyumba ya mwanachama. Mafao ya pensheni ni kwa ajili matumizi wakati mwanachama hatakuwa na uwezo wa kufanya kazi. Hata hivyo, nyumba ni hitaji muhimu kwa kila binadamu na hivyo kukubalika katika utaratibu huu. Ninachowea kusema kwanza, tuanze na hili kwa sababu kama tulivyokubaliana katika Kamati hata hizi hazitatoka katika ile *fund* yenyewe, hasa hasa kitatengwa kifungu kidogo ili kuhakikisha kwamba kinajaribu ku- *accommodate* maombi mbalimbali ya watu kukamilisha nyumba zao au kujenga nyumba zao ili waweze kujihifadhi. Sasa tutoe kwanza muda tuone mafanikio ya kile kinakwendaje.

Tarehe ya kuanza Sheria iendane na Sheria ya Mifuko. Maandalizi makubwa yatahitajika ili kuwezesha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti kuanza utekelezaji wa majukumu yake. Mojawapo ni uteuzi wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu hivyo, hoja ya Sheria hii kuanza kutumika mapema iwezekanavyo. Kifungu namba 58 kinatoa miezi 12 kwa Mifuko kurekebisha Sheria. Kwa hiyo, tunaposema ianze mara moja angalau utafutaji wa ofisi uanze kwanza kutafuta watu ambao tunadhani wana sifa zinazostahili, kama ni ku-*appoint Director General* aanze, lakini si kwamba akishapatikana *Director General*, maana yake kazi imeanza moja kwa moja. Tunajua kuna upungufu huo ndiyo maana katika kurekebisha Sheria hizi za Mifuko hii ambayo ipo kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tumetoa kipindi cha miezi 12 ili kuhakikisha kwamba, mchakato wa Bunge umechukua nafasi yake. Kwa hiyo, hilo tunalitambua lakini tumelizingatia katika maandalizi yetu.

Mheshimiwa Ponsiano Nyami anasema kifungu cha 29 kisitumike kwa wanachama waliopo sasa katika Mifuko iliyopo; hili tumeshalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufafanua hoja hizo, yale ambayo tumekubali katika Muswada huu, yarekebishwe tena baada ya kusikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge ni haya yafuatayo: Katika Clause 6(2)(d) tumesemwa, *by inserting between the word “person” and “any”, the phrase within is “establishment.”* Pendekeso hilo au ushauri huo tumeupokea na tumeuweka kama *amendment* nyingine ambayo tunaiweka katika Bunge lako Tukufu. Halafu katika kifungu 16(1) *by inserting immediately between the word “scheme” and “act” the word “or.”*

Kama alivyoshauri Mheshimiwa Janguo; katika kifungu namba 20(5) by inserting the following new provision ambayo tunaiweka kama kifungu kidogo cha (6), for the purpose of the section, the term public interest shall include unlawful act decision or programs which in its occurrence shall affect the benefits of members and as a result may call for government interventions.

Tuliambiwa *public interest* haijawa defined, sasa hapa ndiyo tumeweka *definition* ya *public interest* kwamba, *things would be done in the public interest*. Katika kifungu namba 36 kama kilivyoandikwa upya, by inserting between the word “fund” and “shall” the following phrase “other schemes providing health services.” Huu ni ushauri tuliopewa katika Bunge hili na sisi tumeupokea kama Serikali na tumeuweka kama *amendment*. Kifungu cha 40 kama kilivyoandikwa upya katika kifungu kidogo cha (13); by deleting the phrase “fund reserve, monitoring and substituting for them the phrase and monitoring of...” Kwa hiyo, kitasomeka kwamba, “control and monitoring of investment and investment decisions.”

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasilisho hayo, ninaomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamualiwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

### **Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008 (*The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008*)**

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 3

(*Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 8

Ibara ya 9  
Ibara ya 10

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 11

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ibara ya 11 yenye marekebisho; kuna marekebisho madogo yaliyofanyika lakini katika maoni yaliyotolewa na Kamati inaonyesha kwamba, kifungu hiki kilipaswa kitoke na Serikali ilikuwa imekubali kwamba, huyu Mkurugenzi asiwekwe katika Sheria kwamba, atakaa miaka mitano kwa sababu akikaa miaka mitano maana yake tunamfanya kwamba hata kama amekosea, basi Rais hatakuwa na uwezo wa kumtoa kwa sababu anatakiwa akae miaka mitano. Kwa hiyo, ilipaswa *section* yote iwe *deleted*. Hiyo 11(2).

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Ni kweli tulikubaliana hivyo, sasa tukaona kwamba tukitoa ile *any for one further term* kama Serikali ikiona imetosheleza, huyu Mkurugenzi ataendelea kuwepo kadiri Mheshimiwa Rais aliyeakteua kuona inafaa, lakini ni kweli tulikubaliana asiwekewe ukomo.

**MWENYEKITU:** Kwa hiyo, mnaondoa maneno yapi?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Ndani ya Kamati tulikubaliana Rais asiwekewe ukomo, kwa sababu ndiyo mteuzi kama jinsi anavyoteua Wakurugenzi wengine wote.

**MWENYEKITU:** Kwa hiyo, *amendment* itasomekaje?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafuta ule ukomo.

**MWENYEKITU:** Tunataka tuwe na *executive words*, tunatunga Sheria sisi hatujui unasema nini?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** *DG should be appointed by the President.*

**MWENYEKITU:** Tunaomba kuwa *specific*, kwa sababu hii mwisho itakuja kuwa Sheria. Soma yote halafu utatuambia.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Tulikubaliana kwamba, asiwekewe ukomo kwa hiyo, ibaki 11(1) “*there shall be the Director General of the Authority who shall be appointed by the President.*”

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tuna *delete subsection two* yote; ndiyo makubaliano ya kwenye Kamati?

**WABUNGE:** Ndiyo.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 12  
Ibara ya 13

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 14

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 15

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 16

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 17

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

**MWENYEKITI:** Mtatambua hapa kutakuwa na *re-organization* iliyokuwa ya 18 ndiyo 15, iliyokuwa ya 17 ni 18, iliyokuwa 15 ndiyo 17.

Ibara ya 18  
Ibara ya 19

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21  
Ibara ya 22  
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 28 ambayo ni mpya, namba (4) “*every scheme shall within six months*”, sio *three months*, tulikubaliana iwe *six months* kwa sababu kawaida Hesabu za Serikali baada ya kufunga miezi mitatu inakaguliwa halafu inapelekwa. Kwa hiyo, tunategemea baada ya miezi sita ndiyo itakuwa imefikishwa kwenye *authority*.

**MWENYEKITI:** Jana tulipokuwa tunapitisha Sheria tulisema, *three months accounts* zinapelekwa kwa Waziri, *six months* ndani ya Bunge; ninyi mlikubaliana vipi ni *three or six?*

**MBUNGE FULANI:** Ni *three*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, baada ya *three* pale tunaweka *six*. Waheshimiwa Wabunge, mmeona?

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 29

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 30  
Ibara ya 31  
Ibara ya 32  
Ibara ya 33  
Ibara ya 34  
Ibara ya 35

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 36

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 37  
Ibara ya 38

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 38

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 39

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 40  
Ibara ya 41

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 42  
Ibara ya 43  
Ibara ya 44  
Ibara ya 45  
Ibara ya 46

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 47

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 48

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 49

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 50  
Ibara ya 51  
Ibara ya 52  
Ibara ya 53  
Ibara ya 54

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 55  
Ibara ya 56  
Ibara ya 57  
Ibara ya 58  
Ibara ya 59  
Ibara ya 60

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Jedwali

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia katika jedwali; nilihoji na nikaomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika Kifungu cha 5(1) na Kifungu cha 5(2) kwa nini mahali ambapo inatumika *seal* ya mamlaka wanaothibitisha ni saini ya Mkurugenzi Mkuu na Katibu na mbaya zaidi katika Kifungu cha (2) ambapo maamuzi ya Bodi yanathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu na Katibu wakati kwa kweli Bodi ni ya Mwenyekiti na Bodi yake? Nilitaka maelezo labda pengine Mheshimiwa Waziri, anaweza akanieleza kwa nini imewekwa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umemuelewa Mheshimiwa Mbunge?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamuelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Athumani Janguo, ninaomba urudie taratibu.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali kifungu cha 5(1) nitaisoma yote jinsi ilivyo: “*The affixing of the common seal of the Authority shall be authenticated by the signatures of the Secretary and Director General and any documents required by law to be made under seal.*” Ninavyoelewa mimi, mara nydingi sana mahali ambapo *seal* ya mamlaka inahitajika, Bodi ndiyo inawajibika. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba, ingekuwa *signature* ya Mwenyekiti au Mkurugenzi na Mkurugenzi Mtendaji au Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha pili kidogo kinasema: “*The decisions of the Board may be authenticated by the signatures of the Secretary and Director General.*” Hapa haya ni maamuzi ya Bodi na Kiongozi wa Bodi ni Mwenyekiti wa Bodi; inakuwaje maamuzi yao yanathibitishwa na Mkurugenzi Mkuu, pamoja na Katibu badala ya Mwenyekiti ambaye ndiye anayeongoza Bodi? Ninataka kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii itakuwa ina-deal na Mifuko mingi sana. Katika kuzingatia *integrity* ya Sector to the Board ambayo ni sehemu ya Bodi, DG ambaye ni sehemu ya Bodi, kwa kuzingatia uharaka wa mambo yanayotakiwa yafanyike, kutoptana na kiasi cha Mifuko ambayo itakuwa imeundwa kama tunavyotegemea, sisi tukaona hawa wanatosha ku-authenticate, labda tuseme tu baadaye watakuja kuripoti, lakini itaingia katika Kanuni, watakuja kuripoti kwenye Bodi kuthibitisha zaidi. Hiyo tutaiweka katika Kanuni.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Bado sijaridhika hata kama ni Mifuko mingi, lakini haya ni maamuzi ya Bodi hii ya mamlaka na kila kitu kina kiongozi; Mwenyekiti ndiye kiongozi, maamuzi ya Bodi kwa sababu inasimamia Mifuko mingi mbalimbali kwamba yawe yanathibitiwa na Mkurugenzi Mtendaji, bado sijaridhika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janguo, ulikuwa unapendekeza?

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninapendekeza ile sehemu ya kwanza yale maneno: “*Shall be authenticated by the signature of the Secretary and Director General yawe shall be authenticated by the signature of the Chairman and Director General.*” Hii ya pili, iseme kwamba: “*Shall be authenticated by the signatures of the Chairman and the Secretary,*” kwa sababu hawa ndiyo wanaohusika katika Bodi na maamuzi yake.

**MWENYEKITI:** Serikali inasemaje?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali mabadiliko hayo. (*Makofi*)

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake?*

(*Bunge lilirudia*)

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008 (The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008)**

(*Kusomwa kwa Mara ya Tatu*)

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008 (*The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008*), kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Hivyo, ninatoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umefikia hatua zake zote; ungojea hatua ya Mheshimiwa Rais kuweka saini tu katika Muswada huu. Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo isipokuwa ninapenda kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.56 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 16 Aprili, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*